*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## Kikao cha Hamsini na Saba – Tarehe 25 Juni, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Leo ni Kikao chetu cha Hamsini na Saba, tarehe 25 Juni, 2018, Katibu.

**NDG. NEEMA H. MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini.

Na. 479

### Ahadi ya Kujenga Kituo cha Afya na Kutoa Gari la Wangonjwa - Tunduru

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Katika kampeni za uchaguzi mwaka 2010 Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kujenga Kituo cha Afya katika Mji wa Nalasi na kutoa gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Mchoteka:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Nalasi?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Mchoteka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Afya - Nalasi ulianza Oktoba, 2013 kwa gharama ya shilingi milioni 80 ambapo awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa msingi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD).* Katika mwaka wa fedha 2017/2018, kiasi cha shilingi milioni 75 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hicho kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka kipaumbele na kutoa shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya nane katika Mkoa wa Ruvuma ambapo kati ya hivyo, vituo vya afya viwili vinajengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ambavyo ni Msakale kilichogharimu shilingi milioni 400 na Kituo cha Afya Matemanga kilichogharimu shilingi milioni 500.

(b) Mheshimwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina gari moja ambalo linahudumia vituo vyote vya afya kikiwemo Kituo cha Afya Mchoteka. Hata hivyo, gari hiyo kwa sasa ni chakavu kwa kuwa ilinunuliwa tangu mwaka 2007. Halmashauri inashauriwa kuweka kipaumbele na kutenga fedha katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya ununuzi wa gari lingine la wagonjwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa ujenzi wa kituo kile cha afya ulitokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alipotembelea katika Kata zile mbili za Nalasi zilizoko katika kijiji kimoja na kuagiza kwamba kipatikane Kituo cha Afya; na kwa kuwa Halmashauri imekuwa ikipanga kila mwaka bajeti ya kujenga kituo kile kwa shilingi milioni 80 na shilingi milioni 75, lakini mpaka leo hii bado wameshindwa kujenga kituo kile. Je, Serikali haioni haja sasa ya kutimiza ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne kwa kutoa fedha kwa ajili ya kujenga kituo kile cha afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina gari moja ambalo ni bovu tangu 2007, mpaka leo ni zaidi ya miaka 11; na kwa kuwa eneo la Tunduru ni kubwa sana, lina Majimbo mawili (Kusini na Kaskazini), je, Serikali haioni umuhimu sasa kutoa gari mbili za wagonjwa upande wa Kaskazini na Kusini ili kuweza kuhudumia wananchi wa Wilaya ya Tunduru ambao eneo lao ni zaidi ya *square kilometer* 18,000? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mpakate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza anaulizia Serikali kutoa nguvu ili kumalizia hicho kituo cha afya. Pesa ambayo imepelekwa, shilingi milioni 400 na shilingi milioni 500 inaashiria dhamira njema ya Serikali ya kuhakikisha kwamba vituo vya afya vinajengwa hususan katika Halmashauri ya Tunduru. Halmashauri nayo ina vyanzo vyake,

kwa bajeti ambayo inaisha mwaka 2017/2018 wameweza kukusanya wastani wa shilingi bilioni 2.78 na katika bajeti inayokuja, wanatarajia kukusanya shilingi bilioni 3.1, ni wazi kabisa hakika wakiweka kipaumbele cha kumalizia hicho kituo cha afya na kwa sababu wamesaidiwa na Serikali, wanaweza kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili kuhusu kupeleka *ambulance,* ni kweli tangu mwaka 2007 ile gari itakuwa imeshakuwa chakavu kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi. Ni vizuri tukashirikiana na Halmashauri kwa kutumia vyanzo vyao wakati Serikali Kuu tunahangaikia, tukipata, tutakuwa tayari kuwafikiria lakini siyo vizuri nao wakabweteka kwa sababu wana chanzo kizuri na wanakusanya vizuri. Ni vizuri kiasi hicho ambacho kinapatikana wakatenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya kununua *ambulance,* sidhani kama itaathiri sana Halmashauri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina Vituo vya Afya vinne vya Kichiwa, Lupembe, Sovi na Matembwe. Katika vituo hivi vyote hakuna gari hata moja la wagonjwa, ni lini Serikali itatuletea gari la wagonjwa kwa ajili ya vituo hivi ukizingatia kwamba Kituo cha Lupembe tunafanya operesheni lakini hatuna gari? Inapotokea tatizo la watoto njiti, inakuwa ni shida sana kuwakimbiza Kibena, zaidi ya kilometa 80. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la ndugu yangu Mheshimiwa Hongoli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia njema ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma za afya zinasogezwa na hasa maeneo ambayo ni mbali kuwe na gari kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa. Pia ni ukweli usiopingika kwamba uhitaji ni mkubwa na ndiyo maana tumekuwa tukitoa magari kwa kadri yanavyopatikana na uwezo wa kibajeti unavyoruhusu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kadri fursa itakavyopatikana, tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba kule Lupembe ambako ni mbali nako gari inapatikana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Halmashauri nyingi ikiwemo ya Tabora Manispaa uwezo sasa wa kifedha hasa zile zinazotokana na *own source* umepungua kutokana na baadhi ya mapato ya Halmashauri kwenda kwenye Serikali Kuu na hii imesababisha huduma nyingine kama za afya na hasa vituo vya afya Halmashauri kushindwa kupeleka fedha kule kutokana na upungufu huo. Serikali ina mpango gani wa kuziba pengo hilo ili zile Halmashauri ambazo hazina uwezo ziweze kupata fedha ambazo zinaweza kusaidia vituo vya afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi. Mheshimiwa Gekul jiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakasaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kutembelea Manispaa ya Tabora na katika nafasi ile tulitembelea na kuona vyanzo vya mapato vya Manispaa ya Tabora. Nilikuwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge na tukawashauri, vile vyanzo vilivyopo kwanza ni vizuri wakavisimamia wakahakikisha

kwamba hakuna hata senti tano ambayo inapotea. Tulitembelea eneo la stendi, jinsi ambavyo wanakusanya hatukuridhika na jitihada ambazo zinatumika katika kukusanya, lakini pia kuna vyoo pale na maeneo mengi ambayo hakika wakisimamia vizuri, bado ni maeneo oevu ambayo pesa zinaweza zikakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na TAMISEMI, nguvu yetu tukiweka pamoja hakika huduma katika vituo vya afya na hospitali zitaweza kuboreshwa. Naye mwenyewe ni shuhuda, ameona jinsi ambavyo bajeti ya afya imeongezeka kutoka shilingi bilioni 31 mpaka shilingi bilioni 269. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ni azma na nia ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha vituo vya afya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alibahatika kufanya ziara katika Jimbo letu la Babati Mjini, nasi tukamuonesha jinsi gani tumeathirika baada ya vyanzo vyetu vya Halmashauri kuchukuliwa na Serikali Kuu. Hivi karibuni mliwaita Wakurugenzi, Wenyeviti wa Halmashauri na Maafisa Mipango mkasema kwamba mtatupatia fedha na gawio letu lilikuwa shilingi milioni 900 kwa ajili ya kukamilisha vituo hivi na miradi mingine. Naomba nifahamu, fedha hizo shilingi milioni 900 zinafika lini Babati maana Vituo vya Singe, Mutuka na Sigino tumeshapaua, tunasubiri hela za *finishing?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi, fedha zinafika lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuliwaita Wenyeviti na Wakurugenzi ili waainishe vipaumbele katika maeneo ambayo yataenda kuanza kutumika pindi pesa itakapokuwa imepelekwa kule kwao na wakaainisha. Ofisi ya Rais, TAMISEMI zoezi lile tulishalikamilisha na tulishakabidhi Hazina. Ni matarajio yetu kwamba Hazina wakishakuwa na pesa ya kutosha kutoa, tutaweza kupeleka ili zikafanye kazi ambazo zilikusudiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyohiyo na swali la Mheshimiwa Mangungu, Mbunge wa Mbagala.

Na. 480

**Posho ya Kufundishia na Nyumba za Walimu - Mbagala**

**MHE. ISSA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Serikali ilikuwa na utaratibu wa kutoa Posho ya Kufundishia *(Teaching Allowance)* lakini kwa sasa imefutwa:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali iliifuta posho hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuirejesha posho hiyo?

(c) Katika Jimbo la Mbagala, shule nyingi hazina nyumba za walimu; mfano, Shule za Msingi Mbagala, Maji Matitu na Rangi Tatu. Je, ni lini Serikali itatatua kero hii kwa mkakati maalum kama ilivyoweka mkakati wa upatikanaji wa madawati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Jimbo la Mbagala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haikufuta Posho ya Kufundishia bali iliijumuisha katika mshahara wa mwalimu kwa lengo la kuongeza kiwango cha fedha (pensheni na kiinua mgongo) baada ya kustaafu. Awali posho hiyo ilikuwa inatolewa kwa watumishi nje ya mshahara, hivyo, haikuwa sehemu ya kikokotoo cha mafao ya watumishi baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua upungufu wa nyumba za walimu uliopo katika maeneo yote mijini na vijijini. Hata hivyo, kutokana na urahisi wa walimu na watumishi wengine wa Serikali kupata nyumba za kupanga maeneo ya mjini kama ilivyo katika Manispaa za Jiji la Dar es Salaam, kipaumbele cha juu cha ujenzi wa nyumba za walimu kimewekwa zaidi katika maeneo ya vijijini kule ambako kuna mazingira magumu ya kupata nyumba za kupanga ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwenye maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali inasema kwamba wameingiza *Teaching Allowance* katika mishaharana Serikali ilikuwa inafanya uhakiki kwa ajili ya kulipa madeni ya walimu na malimbikizo yao wakati wa kustaafu na wale ambao wako kazini. Je, Serikali imefikia wapi katika kuhakiki madeni hayo na kuyathibitisha ili walimu

sasa waanze kulipwa maana wamekuwa wakisumbuka na muda mrefu wamekosa kupata haki zao hasa wale waliostaafu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, anasema kwamba walimu wa mijini wanaweza wakapanga nyumba. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwaongezea *allowance* hizi ili waweze kukabiliana na changamoto ya nyumba katika maeneo ya mijini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeshakamilisha uhakiki wa madeni na watumishi wengi tu wakiwemo walimu wameshaanza kulipwa. Wale ambao hawajalipwa naomba waendelee kusubiri, muda wao wa kulipwa ukifika watalipwa. Hakuna mtu yeyote ambaye hatalipwa deni ambalo ni halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili ameuliza kwamba Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea *allowance* walimu? Napenda nimhakikishie kwamba Serikali ni mwajiri wa watumishi wote, siyo walimu peke yake. Kwa hiyo, kama ambavyo tumeweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba tunaweka kipaumbele cha kuwa na nyumba katika maeneo ambayo ni vigumu kupata nyumba kama maeneo ya vijijini ambako hakuna hata nyumba za kupanga kwa watumishi wote; watumishi wa afya, walimu na watumishi wengine, hivyo hivyo hatuwezi kubagua kwamba sababu ni walimu kwa sababu ni walimu, tuwaongezee *allowance* walimu peke yao watumishi

wengine tuwaache gizani, hapana. Nadhani huo utakuwa ni ubaguzi na Serikali haiwezi kufanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Utakubaliana nami kwamba hakuna kada inayonyanyasika hapa nchini kama walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali ilipunguza baadhi ya walimu wa sekondari kwenda shule za msingi kutokana na upungufu wa walimu na ikadai kwamba ina fedha za kuwalipa. Leo tunavyozungumza, baadhi ya Wakurugenzi wamewaambia wale walimu warudi kwenye shule za sekondari. Kwa hiyo, ina maana Serikali ilikuwa haijajipanga. Je, ni lini Serikali itawalipa walimu hao fedha kama ambavyo walidai kwamba watawalipa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini? Jiandae Mheshimiwa Kakoso.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uamuzi ule wa kuhamisha walimu wa sanaa waliozidi katika shule za sekondari kuwapeleka kwenye shule za msingi ulikuwa ni sahihi. Kilichosisitizwa ni kwamba mtumishi yeyote anastahili apate haki zake kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni zetu za Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tangazo la Mheshimiwa Rais limetoka mwezi Februari kwamba mtumishi asihamishwe mpaka alipwe, wale ambao walikuwa wameshahamishwa watalipwa madeni yao halali, wala hakuna tatizo. Wale ambao walikuwa bado, wasubiri,

watahamishwa baada ya fedha kupatikana. Wale ambao wamerudishwa ni kwa muda tu. Kwa hiyo, naomba hili liwe *clear* wala halina matatizo yoyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika imejitahidi sana kuhamasisha wananchi kujenga vyumba vya madarasa na nyumba za walimu lakini bado kunahitajika nguvu ya Serikali kumalizia majengo yale ikiwemo Shule ya Msingi Busongola, Bulamata, Pandandogo na nyinginezo. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo ili ziweze kumalizia majengo hayo ambayo wananchi wamejitolea? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moshi Selemani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, kwa nchi nzima maeneo mengi kabisa wananchi wamejitahidi, wamejenga majengo na mengi ya majengo hayo yamefika kwenye lenta tayari kumaliziwa. Sasa hapo ni jukumu letu sisi Serikali, Halmashauri na wadau wengine kuunga mkono nguvu za wananchi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo tunalizingatia. Naomba sana tuwasiliane mwezi huu wa Julai na Agosti ili kusudi tuweze kuyatatua matatizo kama hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano la Mheshimiwa Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini.

Na. 481

**Kuunganishwa na Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa**

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU** aliuliza:-

Watanzania tuliaminishwa kwamba iwapo Tanzania ikiunganishwa na Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa, tutaimarisha mawasiliano na kupunguza gharama za mawasiliano:-

Je, taarifa hizo zilikuwa sahihi kwa kiwango gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Constatine John Kanyasu, Mbunge mahiri wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa kuwa kujengwa kwa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kumeimarisha mawasiliano na kuleta faida ya kushuka kwa gharama za mawasiliano nchini, pamoja na faida nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkongo umewezesha kushuka kwa gharama za kusafirisha masafa kwa umbali unaozidi kilomita 1,000 kwa kiwango cha 2Mbps kutoka Dola za Kimarekani 20,300 mwaka 2009 hadi Dola za Kimarekani 160 kwa mwaka 2015. Hilo ni sawa na punguzo la zaidi ya asilimia 99. Hii imewezesha gharama za huduma za kupiga simu kwa mtumiaji wa mwisho kushuka kutoka Sh.147 kwa dakika mwaka 2009 hadi wastani wa Sh.56 kwa dakika mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya simu na *internet* kutoka watumiaji 17,642,408 mwaka 2009 hadi kufikia watumiaji 40,080,954 mwaka 2017 kwa watumaiji wa simu; na kutoka watumiaji 520,000 mwaka 2009 hadi kufikia watumiaji 22,995,109 mwaka 2017 kwa watumiaji wa *internet*. Vilevile gharama za maunganisho baina ya mtandao mmoja na mwingine *(interconnection fee)* zimeshuka kutoka Sh.115 kwa dakika mwaka 2009 hadi Sh.15.6 kwa dakika mwaka 2018, ambapo imesababisha watoa huduma kuwa na huduma za vifurushi vinavyoruhusu mtumiaji kununua kifurushi kinachomwezesha kupiga simu katika mitandao yote na kutumia *internet* kwa bei nafuu kuliko ilivyokuwa hapo awali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kabla ya Mkongo wa Taifa ilikuwa ukinunua *GB10* ni Sh.10,000 lakini baada ya Mkongo wa Taifa gharama imeongezeka sasa ukinunua *GB10* ni Sh.35,000. Nilitaka kupata maoni ya Mheshimiwa Naibu Waziri anaposema gharama imeshuka kwenye *data* ana maana gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, wakati wa Mkongo wa Taifa unapigiwa debe, tuliambiwa utakwenda katika kila halmashauri na taasisi za umma ili kusaidia taasisi hizo kwanza kuwa *informed* na *information system* lakini kusaidia katika shughuli mbalimbali. Ni kwa kiwango gani agizo hili limetekelezwa katika taasisi za umma na halmashauri zote nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Constatine John Kanyansu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utafuatilia jibu langu la msingi, nimeeleza kwa ujumla jinsi ambavyo Mkongo umesaidia kupunguza gharama za matumizi na kuhakikisha kwamba Watanzania wengi wanapata huduma za mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza la Mheshimiwa Kanyasu linahusu kwa nini kabla ya Mkongo kulikuwa na huduma ambazo ni nafuu, kwa jinsi anavyoona yeye. Tukumbuke kwamba kabla ya Mkongo watumiaji walikuwa wachache sana sasa hivi napozungumza, huduma zimeendelea kushuka. Hiyo gharama aliyoisema ni ya kujiunga na vifurushi, kama hujiungi na vifurushi, ukiweza kupata Sh.10,000 peke yake unaweza ukapata *GB* nyingi za kutosha kutegemeana na aina ya mtandao ambao unautumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uunganishwaji wa taasisi mbalimbali, napenda nimweleweshe Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka sasa hivi tumeunganisha taasisi za Serikali na *Agency* zake jumla 72, *Local Government Authorities* nazo tumeunganisha 77, taasisi mbalimbali kama vyuo na watafiti, *RITA* na huduma za afya tumeunganisha jumla 207.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Catherine, ajiandae Mheshimiwa Bobali.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Ngorongoro Mkoa wa Arusha imetengwa kimawasiliano kwa muda mrefu sana, hata imefikia *stage* Mkurugenzi wa

Halmashauri anashindwa kuwasiliana kwa njia ya *email* katika shughuli zake za kikazi. Je, ni lini Serikali itaunganisha Wilaya ya Ngorongoro na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Catherine Magige kwa jinsi ambavyo anafuatilia sana huduma mbalimbali zinazotakiwa kupatikana katika mkoa wake na hasa eneo alilolitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna baadhi ya wilaya hapa nchini bado hazijaunganishwa lakini ni chache. Kati ya Wilaya 187 bado hatujaunganisha Wilaya 16 na tumeshawaelekeza *TTCL* waende wakaunganishe Mkongo ili huduma hizo ziweze kupatikana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kumekuwa na wimbi sasa limeibuka la wizi wa kutumia mitandao ya simu, wakiwa wanatuma *message* kwamba umeshinda Tatu Mzuka, umeshinda Tigo, tuma pesa kwenye namba hii; kumekuwa na desturi hiyo sasa hivi. Nilitaka kupata majibu kutoka kwa Waziri, *TCRA* imechukua juhudi gani kuhakikisha kwamba wizi wa mitandao kwa kutumia simu unakomeshwa na wahusika wanakamatwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Mipata ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bobali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na matukio ya Watanzania mbalimbali kutumiwa *message* ambazo zinaonyesha na kuashiria kwamba kuna utapeli unaoendelea katika huduma za mawasiliano. Kwa kutumia Sheria ya Mitandao ya 2015, *TCRA* kwa kushirikiana na Polisi wameendelea kufanya kazi kwa karibu kuhakikisha kwamba wote wanaosambaza ujumbe huo, wanakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa mawasiliano unazidi kupanda kwa huduma za jamii na kiuchumi. Wananchi wa Kata ya Ninde na Kata ya Kala katika Ziwa Tanganyika ndiyo pekee hawana mtandao wa simu. Nimechukua hatua kama Mbunge kuandika barua kuleta Wizarani na kumfuata Mheshimiwa Waziri kumueleza juu ya tatizo hili. Je, wananchi watapata lini huduma hii muhimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mipata, kama ifuatavyo:-

Mheshimwia Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna baadhi ya maeneo machache ya nchi yetu huduma za mawasiliano ya simu ni duni. Kwanza nimpongeze kwa jinsi anavyofuatilia; ameshakuja mara nyingi sana ofisini kufuatilia huduma za mawasiliano kwa eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, tenda imetangazwa na hivi karibuni tutawapa watoa huduma ambao wataenda kuweka minara sehemu mbalimbali ambazo mpaka sasa hivi hazina huduma za mawasilinao. Baada ya kufanya hivyo, basi huduma hiyo itaanza kupatikana kama kawaida kwa wananchi wake. *(Makofi)* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mnashauriwa na kushawishiwa mtumie *line* za *TTCL,* zina huduma bora nchini kote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Rweikiza.

Na. 482

**Kujenga Barabara ya Kanazi – Izimbya kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Barabara ya kuanzia Kanazi, Kata ya Kemondo kupitia Ibwera kwenda Katoro, Rubale na Izimbya ipo chini ya *TANROADS*, na ni muhimu kwa wakazi wa Bukoba na kwa uchumi wa Taifa:-

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara tajwa inaitwa Kyetema – Kanazi – Kyaka 2 yenye urefu wa kilometa 42.37 na inapita katika vijiji vya Ibwera na Katoro. Barabara nyingine ni Rutenge – Rubale – Kishoju yenye urefu wa kilometa 74 ambayo inapita katika Vijiji vya Izimbya na Rubale. Barabara zote hizo ni barabara za Mkoa na zinahudumiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)*. Barabara hizi ni kiunganishi muhimu cha barabara kuu za lami ambazo ni barabara ya Mutukula – Bukoba – Kagoma – Lusahunga na barabara ya Kyaka – Bugene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa baraba hizi, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo ya aina mbalimbali ili ziweze kupitika wakati wote wa mwaka. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, barabara ya Kyetema – Kanazi – Kyaka 2 imetengewa shilingi milioni 598.13 na barabara ya Rutenge – Rubale – Kishoju imetengewa shilingi milioni 333.20. Aidha, Serikali imejenga kwa kiwango cha lami maeneo korofi yenye urefu wa kilometa 4.8 sehemu ya Kyetema hadi hadi Kanazi kwenye barabara ya Kyetema – Kanazi – Kyaka 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kipaumbele cha Serikali ni ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara za kuunganisha makao makuu ya mikoa, pamoja na barabara za kuunganisha Tanzania na nchi jirani. Hivyo, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za mikoa zikiwemo barabara za Kyetema – Kanazi – Kyaka 2 na Rutenge – Rubale – Kishoju utaendelea kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba ina kata 29. Kati ya hizo, kata 20 zinahudumiwa na

barabara niliyoitaja. Kata hizo ni Katerero, Kemondo, Ibwera, Nakibimbiri, Kasharu, Kisogo, Kaibanja, Katoro, Kyamuraire, Ruhunga, Mugajalwe, Izimbya, Kibirizi, Kaitoke, Kikomero, Rukoma, Rubare, Buterakuzi, Mikoni na Bujugo. Aidha, Bukoba kuna mvua nyingi sana barabara ya udongo inaharibika, mara nyingi inakuwa haipitiki na huko ndiyo kuna mazao mengi kama kahawa na ndiyo uchumi mzima uko kule. Kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kujenga lami barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rweikiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua maeneo haya ni muhimu sana katika uzalishaji na pia tunatambua kwamba ziko mvua nyingi na kumekuwa na uharibifu wa mara kwa mara. Nampongeza tu Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu mara nyingi tumezungumza juu ya kuhakikisha kwamba barabara hizi tunazitengeneza na kwa kweli kama alivyosema, hizi ni kata nyingi sana, kata 20 kati ya kata 29.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge ikiwa ni pamoja na wananchi wa maeneo ya Kata hizi ikiwemo Kata za Katerero, Kemondo, Ibwera na kata nyingine kwamba baada ya kukamilisha kuunganisha mkoa na mikoa mingine nguvu kubwa tutailekeza katika maeneo haya ya barabara ambazo zinapita kwenye wilaya zetu ikiwemo maeneo haya aliyoyataja ili sasa tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Bukoba Vijijini kwamba maeneo haya tutayatazama na tutayaweka katika mpango ili siku za usoni tuweze kuitengeneza barabara kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Qambalo wajiandae.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri kuhusu swali lililopita, naomba kuiuliza Serikali, barabara ya Kyaka 2 kutoka Katoro - Ishembulilo - Kashamba - Kyaka; eneo lile ni bovu sana kila mwezi Aprili barabara haipitiki. Pamoja na kwamba amesema inahudumiwa na *TANROADS,* naomba *commitment* ya Serikali ya kuweka madaraja kwenye maeneo yale ili mwezi wa Aprili kuwe kunapitika kama sehemu nyingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi na Mheshimiwa Kawambwa ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Bulembo kwamba nimemsikia, nami nimwelekeze tu Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Kagera aende kuangalia eneo hili na kushauri tufanye nini juu ya kutengeneza daraja eneo hili korofi. Kama ilivyo kawaida, maeneo yote korofi nchi nzima tunaendelea kuyashughulikia wakati tukiendelea na harakati za kuboresha barabara kuhakikisha wananchi wetu wanapita muda wote katika maeneo yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto atafuatia Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Rais mwezi Mei alifika Iringa katika Wilaya ya Kilolo na akatoa ahadi kwamba barabara ile ya kutoka Ipogolo - Kilolo ambayo inaitwa sasa barabara ya Mfugale ianze kujengwa mara moja. Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa ili ahadi ile ya Rais aliyotoa kwa wananchi iweze kutimia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwamoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana kwa sababu tumezungumza sana juu ya barabara hii hata kabla ya ahadi ya Mheshimiwa Rais. Kwa vile Mheshimiwa Rais ametoa ahadi kuitengeneza barabara hii, tulikubaliana kwamba baada ya Bunge hili nitatembelea huko ili tuweze kuweka msisitizo kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi natambua kwamba barabara hii ilishasanifiwa. Kwa hiyo, harakati za ujenzi wa barabara hii, napenda wananchi wa Kilolo wajue ujenzi ulishaanza kwa sababu hatua za awali tumeshaanza, sasa ni zoezi la kupata fedha ili barabara ijengwe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwamoto asiwe na wasiwasi barabara hii itajengwa na kwa msisitizo wa Mheshimiwa Rais tutakwenda kuijenga barabara hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Qambalo halafu Mheshimiwa Kawambwa.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ujenzi wa barabara ya *Oldian Junction* – Mang'ola – Matala - Kolandoto umeshakamilika miaka miwili iliyopita na barabara hiyo ni muhimu sana kwa sababu

inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu. Je, ni lini sasa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Qambalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ukiotokea upande wa Lalago ukivuka Sibiti kwa kushoto kule iko barabara hii ambayo itakuwa inakwenda Karatu ambayo michoro na usanifu wake umeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ina *interest* kubwa sana kwa sababu kuna uzalishaji mkubwa, historia muhimu na pia kuna utalii mkubwa katika maeneo haya. Kwa hiyo, kwa sababu hatua hii imeshakamilika, tuko kwenye hatua ya kutafuta fedha, wakati wowote tukipata fedha ujenzi utaendelea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kawambwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Makofia - Mlandizi ni muhimu sana ambayo inaunganisha wananchi wa Halmashauri ya Bagamoyo na Kibaha Vijijini. Barabara hiyo sasa hivi ina matatizo sana ya kupitika hasa baada ya mvua hizi nyingi zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ni ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005, 2010 na 2015

kujengwa kwa kiwango cha lami. Ni lini fidia italipwa kwa ajili ya barabara hiyo na lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kawambwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Kawambwa ni shahidi kwamba tumezungumza muda mwingi sana juu ya barabara hii. Barabara itakuwa na urefu wa kilometa zaidi ya 30 kuja Mlandizi. Kuhusu fidia tulishafanya tathmini tayari, tutaendelea kuwasiliana na wenzetu Wizara ya Fedha hizi fedha zipatikane ili wananchi hawa walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi watalipwa kwa sababu tulikuwa na fidia nyingi nchi nzima katika maeneo mbalimbali, lakini tumefika hatua nzuri, maeneo mengi tumeshalipa fidia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Kawambwa asiwe na wasiwasi. Nafikiri baadaye tuzungumze na tuongee na wataalam tuone hatua hii imefika wapi ili tuweze kulipa mara moja hii fidia ya wananchi wake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo na swali la Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 483

**Ujenzi wa Barabara ya Nangurukuru – Liwale**

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE** aliuliza:-

Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 6.4 kwa mwaka 2012 mpaka mwaka 2015 kwa ajili ya ukarabati wa kawaida wa barabara ya Nangurukuru – Liwale yenye urefu wa

kilometa 230 na barabara hii inawaunganisha watu wa Liwale na Wilaya za Lindi na Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam:-

Je, Serikali iko tayari kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lathifah Chande, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kuhakikisha kuwa kwanza makao makuu ya mikoa yote inaunganishwa kwa barabara za lami ambapo kwa sasa karibu mikoa yote nchini imeunganishwa kwa barabara za lami. Pili, kuunganisha nchi yetu na nchi za jirani kwa barabara za lami ambapo karibu 64% ya barabara kuu zimejengwa kwa kiwango cha lami. Tatu, ni kuhakikisha kuwa, barabara zote za mikoa ambazo nyingi zinaunganisha makao makuu ya Wilaya zinapitika majira yote ya mwaka. Kwa sasa barabara nyingi za wilaya zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na zinapitika majira yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Lathifah Chande, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nangurukuru – Liwale ni barabara ya mkoa inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Lindi. Hivyo, Wizara yangu kupitia *TANROADS* inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali yatakayoiwezesha barabara hii kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya shilingi bilioni 1.086 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya muda maalum na katika mwaka wa fedha

2018/2019, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.76 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati na matengenezo ya muda maalum kwa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2015 imepanga kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Kwa sasa inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge. Mazungumzo yamekuwa mengi hata *Hansard* sasa wanashindwa kupata majibu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lathifah.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali la kwanza, kwa sababu ni Sera ya Serikali kuunganisha mikoa kwa barabara ambazo ndizo tunazitegemea kwa ajili ya maendeleo yetu. Ni lini tutegemee Serikali itaunganisha barabara inayotokea Liwale Mkoa wa Lindi kuweza kufika Morogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa muda mrefu sana Serikali imekuwa ikijificha kwa kusema kwamba kumekuwa na upembuzi yakinifu ukiwa unafanyika na mara nyingi upembuzi huu umekuwa ukichukua muda mrefu na wakati mwingine inaweza kufika hata miaka 10 tunakuwa kwenye upembuzi yakinifu. Ni lini tutegemee Serikali itaweza kuweka *limitation* au taratibu ambapo kutakuwa na muda maalum wa upembuzi yakinifu kufanyika ili ujenzi wa barabara uwe unaanza kufanyika mapema? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, muda wetu unakwenda.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lathifah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ni Sera ya Serikali kuunganisha mikoa. Kama nilivyojibu wiki iliyopita wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Mlinga, nilisema kwamba tutakwenda kutazama kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Lindi kwa maana ya Liwale na Mahenge, lakini hii ni siku za usoni, kwa sababu ziko *logistics* nyingi lazima zifanyike kwa sababu barabara hiyo itapita katika Hifadhi ya *Selous* lakini pia *structures* zake zinahitaji fedha nyingi. Kwa hiyo, tutaendelea kuitazama na Serikali inajua umuhimu wa kipande hiki cha barabara kuunganisha kuja Mahenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba Serikali inajificha kwa kusema inasanifu na kutengeneza michoro; hili siyo kweli. Niseme kwamba mpaka sasa hivi barabara za lami zinazounganisha mikoa karibu mikoa yote tunakamilisha. Barabara zaidi ya kilometa 13,000 tumeshatengeneza kwa lami kwa maana ya kuunganisha mikoa na nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika bajeti hii ya mwaka 2018/2019, tumependekeza kufanya usanifu wa barabara kilometa 3,856. Hizi ni kilometa nyingi sana na hii ni kuonesha jinsi namna gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi iko *committed* kuhakikisha kwamba kila tunapokamilisha barabara fulani ni mwanzo wa kuendelea kusanifu barabara nyingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lathifah ataendelea kusikia tukisanifu na kutengeneza michoro ya barabara kila wakati kwa sababu kila wakati tunavyokamilisha ujenzi wa barabara, kwetu sisi kama Serikali ni fursa ya kutengeneza barabara nyingine. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aisharose halafu Mheshimiwa Mwambe

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, barabara inayotokea Singida Mjini – Ilongero – Mtinko – Mudida – Kidarafa – Ikungi - Haydom yenye urefu wa kilometa 93.4 ujenzi wake kwa kiwango cha lami umekuwa ukisuasua. Kukamilika kwa barabara hii kutaharakisha sana shughuli za maendeleo kwa Singida Vijijini. Barabara hii ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne...

**MWENYEKITI:** Swali, swali.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia iko katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015. Je, ni lini sasa barabara hii itakamilika kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuharakisha shughuli za maendeleo kwa wananchi wa Singida Vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, anataka kujua ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii imekuwa ikitengenezwa kidogo kidogo lakini nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba matengenezo yale aliyoyaona yalitokana na usimamizi mzuri wa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Singida. Kila alivyobakiza fedha ameendelea kutengeneza kilometa moja, kilometa mbili na takriban sasa tuna kilometa 10 zimetengenezwa kwa mtindo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu, mwaka huu wa fedha 2018/2019, tumetenga shilingi milioni 200 kuanza usanifu wa kilometa hizi 93 kwenda Haydom. Nami wiki zilizopita nimepita kwenye barabara hii kuweka msisitizo kwamba usanifu uanze mara moja mara baada ya kupata fedha ili sasa barabara hii iungane na barabara itakayokuwa inatoka Haydom kuja Sibiti, barabara kubwa hii ambayo itajengwa kwa kiwango cha lami ili wananchi wa Singida na maeneo mengine ya jirani waweze kwenda kirahisi kupata huduma katika Hospitali ya Haydom.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL M. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu kutoka Serikalini kwamba barabara ya Masasi inayopitia Vijiji vya Nangaya – Chikunja – Lukuledi – Naipanga – Mkotokuyana mpaka Nanganga inaelekea kujengwa kwa lami hivi karibuni. Hata hivyo, uthamini wa mali na rasilimali za watu katika maeneo hayo yote niliyoyataja umefanyika zaidi ya miaka mitano iliyopita. Je, Serikali itakwenda kurudia kufanya uthamini au itawalipa watu wale fidia zao kutokana na uthamini uliofanyika miaka mitano iliyopita? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mwambe pamoja na wananchi kwamba uthamini uliofanyika kama hakuna matatizo makubwa ya kurudia, ndiyo utakaotumika kulipa wananchi hawa. Niwafahamishe tu wananchi kwa ujumla kwamba utaratibu uliopo kuna namna ya kuangalia thamani ya fedha kwa sasa, lakini *base* itakayotumika ni ule uthamini uliofanyika kipindi

ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, uko utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba fedha zile zitalipwa kulingana na hali ya sasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati na swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe.

Na. 484

**Mpango wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji Moto**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Katika Bunge lililopita la 2010 – 2015 Serikali iliongelea kuhusu mpango wa kuwekeza umeme unaotumia chemchemi ya maji ya moto yanayopatikana katika Kata ta Maji Moto:-

(a) Je, mpango huo umefikia wapi?

(b) Je, ni lini sasa Jimbo la Kavuu litapata umeme kwa maendeleo ya wananchi wa eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi ni moja ya mikoa inayopitiwa na Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, hivyo kuwepo na uwezekano wa kuwa na hifadhi kubwa ya joto ardhi. Serikali inaendelea kufanya tathmini ya rasilimali ya nishati ya joto ardhi ili kujiridhisha na uwepo wa rasilimali ya kutosha kabla ya kuchoronga visima vya

majaribio. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali kupitia *Tanzania Geothermal Development Company* imepanga kufanya utafiti wa kina katika maeneo zaidi ya 50 yenye viashiria vya joto ardhi likiwemo eneo la Maji Moto.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Jimbo la Kavuu vya Kibaoni, Usevya, Ilalangulu na Manga, vinapata umeme kutoka Sumbawanga, Mkoani Rukwa kupitia Mji wa Namanyere, Wilayani Nkasi. Aidha, vijiji vingine vya Jimbo la Kavuu ikiwa ni pamoja na Maji Moto, Mbende, Chamalangi, Mkwajuni, Ikuba, Mamba na Kasansa vitapatiwa umeme kupitia mzunguko wa kwanza wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu *(REA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupatikana kwa suluhisho la kudumu la umeme katika Jimbo la Kavuu, Serikali imeanza hatua za awali za utekelezaji wa mradi wa kusafirisha umeme wa gridi, kV 400 kutoka Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma hadi Nyakanazi. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza Machi, 2019 na kukamilika mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Maji Moto wameanza kuwekeza kuitikia kauli mbiu ya viwanda; na kwa kuwa hawana umeme wa uhakika; na kwa kuwa, *REA* Awamu ya Tatu, *round* ya kwanza haijulikani itaanza kutekelezwa lini katika Jimbo la Kavuu, je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuharakisha hizi tafiti zao za *geothermal* kwa ajili ya kuwapatia wananchi wa Maji Moto umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa vijiji vya Kibaoni, Usevya, Ilalangulu na Manga vimefikiwa na

umeme unaotoka Sumbawanga, lakini kumekuwa na tatizo kubwa la kukatika kwa umeme katika maeneo hayo na kufanya wananchi katika Kata ya Kibaoni kupata hasara sana kutokana na kukatikakatika kwa umeme. Je, Serikali inawaeleza nini wananchi waliopata umeme huu ambao ni wa Kata ya Kibaoni kupata umeme wa uhakika ambao hauwatii hasara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kushukuru maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kikwembe, lakini kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika Mkoa mzima wa Katavi na hasa Jimbo la Mheshimiwa Dkt. Kikwembe lina shida na kero za umeme. Katika maswali yake ya msingi mawili, la kwanza ni *geothermal.* Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, kati ya maeneo ambayo kwa kweli yanafanyiwa tafiti za kutosha katika upande wa *geothermal* ni pamoja na eneo la Maji Moto katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo 50 ambayo tunatarajia kuyafanyia upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujua mashapo ya *geothermal* ni pamoja na Jimbo lake. Hivi sasa *TGDC* wanaendelea na kazi hiyo na mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Kikwembe nampongeza sana kwa hoja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na umeme wa uhakika katika maeneo ya Mheshimiwa Mbunge, Katavi pamoja na Sumbawanga, Serikali imeanza utaratibu wa kujenga njia kuu ya kusafirisha umeme wa kilovoti 400. Katika maeneo ambayo tutayapatia kipaumbele sana ni pamoja na Jimbo la Kavuu ambapo maeneo ya Maji Moto ni maeneo

ya kibiashara, kwa hiyo, njia kuu za kusafirisha umeme zitakamilika. na tumetenga shilingi bilioni 664 kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Kikwembe nampongeza sana, lakini Serikali inalifanyia kazi. Ni matarajio yetu kuanzia Januari miundombinu inaanza kujengwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika Jimbo la Mbulu Mjini kuna maporomoko ya Haino katika Tarafa ya Nambisi, Kata ya Nambisi. Maporomoko hayo ambayo wataalam kutoka Serikalini na taasisi mbalimbali zisizo za Serikali wameendelea kuyatembelea; na kwa kuwa, tuna mahitaji makubwa ya uzalishaji wa umeme nchini, je, ni lini Mheshimiwa Waziri na Wizara yake watatembelea maporomoko ya Haino ili yaweze kutoa mchango wake katika sekta ya umeme kwa nchi nzima na hususan Jimbo la Mbulu Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issaay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunatambua uwepo wa maporomoko haya ambayo kwa mujibu wa tafiti mbalimbali yana uwezo hata wa kuzalisha Megawati 5,000. Kupitia Serikali na *TGDC* tuna mpango wa kuhakikisha kwamba tunazalisha Megawati 200 kupitia maporomoko mbalimbali ambayo yataleta nishati ya joto ardhi ifikapo 2025, naomba nimkubalie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama Serikali kupitia Wizara ya Nishati tutafanya ziara katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwenye jibu lake kwamba kwa mwaka huu kuna maeneo kama 50 ambayo yatafanyiwa tafiti

likiwemo eneo la maporomoko hayo katika Jimbo la Mbulu Mjini. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Malocha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ujenzi wa miradi ya umeme awamu ya pili na awamu ya tatu bado utekelezaji wake hauendi kasi kama ilivyopangwa hasa katika Mkoa wa Rukwa, Jimbo la Kwela na tatizo kubwa ikiwa ni upatikanaji wa nguzo. Mkoa wa Rukwa unahitaji nguzo 13,000. Pamoja na jitihada zote, ni nguzo 350 tu zilizopatikana. Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hilo ili miradi ya umeme iweze kutekelezwa haraka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ni lini?

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na kweli nilitembelea eneo lake. Nimhakikishie tu kwamba kero ya nguzo kwa sasa kimsingi haipo. Mwanzoni mwa mwaka 2017 tulisitisha kuingiza nguzo kutoka nje ambapo ndiyo lilikuwa tatizo la Wizara kwa muda mrefu. Waagizaji wa nguzo walikuwa wanachukua miezi sita hadi nane kufikisha hapa nchini, hivi sasa nguzo zinapatikana. Mahitaji yetu ya nguzo kwa mwaka ni 200,800 wakati nguzo zinazopatikana kwa wazalishaji wa ndani ni nguzo 2,000,872. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge miradi hii itatekelezeka kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimetembelea Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na nampongeza sana anavyohangaikia maendeleo ya wananchi wake. Ni kweli mkandarasi anasuasua na jana tumemwelekeza, hivi sasa anaendelea katika Kijiji cha Maendeleo ili kusudi aanze kuwapatia wananchi umeme. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Mbunge lakini suala la nguzo hivi sasa siyo kero kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara halafu Mheshimiwa Atupele wa Mbeya City ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kitunda, Mvute, Mbondole, Nzasa na Iyongwa kote huko kuna sekondari. Maeneo yote haya ambayo nimeyataja hayana umeme. Naomba nijue ni lini maeneo haya ya umma yenye zahanati, shule na wananchi watapelekewa umeme wa uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waitara. Mimi kwanza ni mpiga kura wake katika Jimbo lake, naelewa sana maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli kabisa maeneo ya Mbondole na maeneo mengi sana ya Chanika hayana umeme, lakini maeneo yote 27 yameingia kwenye Mpango mahususi wa *Peri-Urban* ambao utekelezaji wake umeshaanza. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge utekelezaji huu unaanza mwezi Julai na utakamilika mwezi Machi mwakani. Kwa hiyo, ni matarajio yetu ndani ya miezi mitano vijiji vyote vitakuwa vimeshapata umeme maeneo ya Mbondole.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Atupele.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme unaotokana na joto ardhi ama *geothermal* ni endelevu na *sustainable* ama *renewable* na Serikali ingeweza kutumia vyanzo vyote tungepata zaidi ya Megawati 5,000. Je, ni lini Serikali itaweza kukamilisha mradi wake ambao ilikuwa inaendelea kuufanya wa kuchoronga visima katika Ziwa Ngosi lililopo Wilayani

Rungwe pamoja na Mto Mbaka uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri. Kusema ukweli kati ya maeneo ambayo tunayafanyia upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujua mashapo ya *geothermal,* yako zaidi ya 50. Tunachofanya sasa hivi, tunapitia marejeo ya takwimu sahihi katika Ziwa Ngosi ambao liko Mbozi, maeneo ya Katavi pamoja na Rukwa. Tathmini za awali zinaonesha kwamba mashapo yaliyopo ya *geothermal* yanaweza kutupa jumla ya Megawati 5,000 kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tunakwenda hatua kwa hatua, tunataka kuanza Megawati 20 hadi Megawati 100. Kwa hiyo, ni matarajio yetu kwamba ndani ya miaka hii miwili tutakuwa tumeshapata mashapo sahihi ili tuanze sasa na Megawati 100 kwa ajili ya *geothermal.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Mradi wa *REA III* kuna Kitengo kimeanzishwa kinaitwa *Peri-urban* katika Halmashauri ambazo bado zina maeneo ya vijiji na vitongoji. Je, ni lini kitengo hiki kitaanza kufanya kazi katika Halmashauri zetu kwenye Kata za Kilare, Mzizima, Pongwe, Marungu na Maweni ili tuweze kupata huduma hii ya umeme wa *REA III?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri, pumzika leo, yuko mwenyewe hapa.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza katika ufafanuzi wangu uliotangulia, ni kweli tunatekeleza miradi miwili kwa mijini. Uko mradi wa *urbanisation* unaotekelezwa na *TANESCO* lakini uko mradi

wa *Peri-urban* ambao unatekelezwa kimtindo wa *REA,* ingawa katika mitaa ya mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mheshimiwa Mbunge kule Tanga Mjini yako maeneo 17 ambayo tumeshaainisha ikiwemo na Izizima pamoja na Majani Mapana. Utekelezaji umeanza kufanyika, ndani ya miezi sita ni matarajio yetu utakamilika na maeneo yake yataanza kupata umeme kwa utaratibu wa *Peri-urban.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL K. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize Mheshimkiwa Waziri, Mikoa ya Katavi na Kigoma, *REA III* haijaanza kwa sababu ya migogoro iliyoko Mahakamani, lakini taarifa tulizonazo ni kwamba *ruling* imeshatoka. Ni lini sasa mkandarasi ataanza kazi katika Mikoa ya Kigoma na Katavi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Nzanzugwanko. Ni kweli kabisa Mikoa miwili ya Katavi na Kigoma ilikuwa na migogoro katika Mahakama zetu. Napenda kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba mgogoro huo kimsingi kwa upande wa Ujiji umetatuliwa, mgogoro uliobaki ni ile kesi ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe taarifa tu kwa upande wa Mkoa wa Kigoma, namshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ijumaa ametupa mwelekeo na sisi kuanzia Jumatano ijao, mkandarasi tunamkabidhi rasmi mkoa nzima wa Kigoma. Mkandarasi kwa upande wa Katavi tunakamilisha maandalizi ya manunuzi ili mwisho wa mwezi huu naye akabidhiwe. Ufikapo mwezi Julai, utekelezaji

wa *REA* III kwa mikoa miwili ya Katavi na Kigoma utakuwa umeshaanza na tayari kukabidhiwa kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tarafa ya Ilongero iliyopo Wilaya ya Singida Vijijini ambayo iko kwenye bonde la ufa haijawahi kupata umeme tangu *REA I* na II na ya sasa imeanza kutekelezwa. Kuna Kituo cha Afya ambacho hawawezi kutoa huduma kwa sababu hakuna umeme. Je, ni lini sasa Serikali itawapatia umeme wananchi wale au Waziri aongozane tu nami twende kwenye Tarafa ile akashuhudie ili aweze kuwahimiza wakandarasi waweze kukamilisha umeme katika bonde lile? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa natambua kwamba Kata ya Ilongero iko kwenye mpango wa upelekaji umeme katika awamu inayoendelea. Hivi sasa mkandarasi ameshakaribia maeneo yale, ametoka Marendi kwa Mheshimiwa Mwigulu na wiki ijayo atakwenda Ilongero ambapo kuna Kituo cha Afya. Kwa hiyo, nimpe uhakika Mheshimiwa Mlata kwamba atafika kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongezana na Mheshimiwa Mlata, mimi sina wasiwasi, kama kawaida yangu nitaambatana na Mheshimiwa Mlata tukatatue kero za wananchi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo na swali la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga.

Na. 485

**Usambazaji wa Umeme Vijijini - Jimbo la Manonga**

**MHE. SEIF K.S. GULAMALI** aliuliza:-

Je, ni lini utekelezaji wa usambazaji wa umeme katika Kata za Igoweko, Uswaya, Tambarale, Mwisi, Sungwizi, Mwamala, Ntobo, Ngulu, Mwashiku na Kitangiri utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa usambazaji wa umeme katika Kata za Igoweko, Uswaya, Tambarale, Mwisi, Sungwizi, Mwamala, Ntobo, Ngulu, Mwashiku na Kitangiri utafanyika kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza wa kusambaza umeme vijijini iliyoanza mwezi Julai, 2017 na kukamilika Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kusambaza umeme katika kata hizi inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 zenye urefu wa kilomita 76.48; njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 60.62; ufungaji wa transfoma 36 za KVA 50 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 733. Gharama ya kazi hii ni shilingi bilioni 1.22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Nagu.

**MHE. SEIF K.S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Wizara hii ya Nishati ikiongozwa na Mheshimiwa Medard Kalemani pamoja na Mheshimiwa Subira Mgalu kwa kazi kubwa wanasozifanya kuhakikisha kwamba umeme unapatikana katika maeneo yenye shida ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu msingi ambalo nilitaka kujua kwa sababu tumeshaanza utelezaji wa uzambazaji wa umeme katika baadhi ya maeneo yaliyotajwa lakini tumeanza kwa kusuasua. Je, ni lini sasa kama Wizara; Mheshimiwa Waziri pamoja Mheshimiwa Naibu Waziri wataweza kuja kuona maendeleo ya mradi huu katika maeneo hayo yaliyotajwa kwa sababu uzambazaji wa umeme huo mwisho wake ni Juni, 2019? Ujio wao utasababisha msukumo kuwa mkubwa na kazi hii itafanyika kwa haraka zaidi. Je, ni lini wataweza kufika katika maeneo hayo tajwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nampongeza sana Mheshimiwa Gulamali kwa jinsi ambavyo anatupa ushirikiano katika kupeleka umeme kwenyeJimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa katika Jimbo la Gulamali mkandarasi yuko katika Kijiji cha Matinje ambacho pia ni cha wachimbaji wadogo wa madini. Nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge, wakandarasi watakapotoka Matinje wanakwenda Nsimbo na ili wafike Nsimbo ni lazima wapite Mwamala, Tambarale, Uswaya na Igoweko. Kwa hiyo, vijiji vyake ambavyo amevitaja kimsingi vitapata umeme kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni lini tutakwenda tena, napenda kutumia nafasi hii kumwambia Mheshimiwa Gulamali kwamba mara baada ya Bunge tutatembelea maeneo yake kwa sababu tunataka tutembelee maeneo yote ya Mkoa wa Tabora. Mkoa wa Tabora unahitaji umeme wa nishati wa kutosha kwa sababu ni mkubwa. Kwa hiyo, tutakwenda Roya kwa Mheshimiwa Ntimizi, tutakwenda Mswaki pamoja na maeneo mengine ya Waheshimiwa Wabunge wa Tabora. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wilaya ya Hanang ilipata vijiji vichache sana awamu ya kwanza ya *REA* na awamu ya pili. Hii awamu ya tatu Mheshimiwa Waziri ameniahidi atanipa vijiji vingi lakini vile tulivyokubaliana ameacha Gocho, Dumbeta, Gisambalang' na Getasam. Mheshimiwa Waziri amesema atakwenda na mimi sasa anaahidi kila mmoja, sijui kama atapata nafasi ya kwenda na mama yake. Ahsante. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, ajiandae Mheshimiwa Julius Kalanga.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni kweli nilimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitakwenda Hanang, lakini kabla sijaenda Hanang tulimpa vijiji 47 vya kuanzia na tukamwongezea vijiji vingine 12, kwa hiyo, lazima tuvitembelee. Kati ya vijiji ambavyo tumeviongeza ni pamoja na Gocha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa Hanang mbali tu na kuongozana na Mheshimiwa Mbunge lakini nitawatuma wakandarasi

waanze kufanya kazi hizo ili wakati tunakwenda, tunakwenda kuwasha na wala siyo kukagua peke yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Julius ajiandae Mheshimiwa Mwilima.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli *REA* III ni vijiji 10 tu kati ya 42 ndivyo vimewekwa kwenye mpango. Je, ni lini Serikali itaongeza vijiji vingine katika *REA III* katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Monduli?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeze Mheshimiwa Mbunge. Tumekaa na Mheshimiwa Mbunge wiki iliyopita. Ni kweli kabisa tulipopitia katika Jimbo la Monduli tulikuta ni vijiji 10 tu ambavyo tumevipangia umeme. Baada ya kufanya mapitio kwa nchi nzima, tumeongeza vijiji 1,442 na vijiji 12 vya Mheshimiwa Mbunge wa Monduli vimo. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa wazo lake zuri lakini tumefanya mapitio na tumeongeza vijiji zaidi ya 1,542 kwa nchi mzima. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge maeneo yote ambayo tulikuwa tumeyaruka hivi sasa kwa kiasi kikubwa tumeyaingiza ili nao wapelekewe umeme kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwilima ajiandae Mheshimiwa Sanga.

**MHE. HASNA S.K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni timu ikiongozwa na Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Kigoma walienda Tarafa ya Nguruka kukagua vijiji vyote vitakavyopatiwa umeme *REA III* lakini hadi leo hii tunavyoongea, mkandarasi alikuwa afike tarehe 2 Juni, 2018 hajakanyaga kwenye vijiji hivyo ambavyo vinatakiwa vipate

umeme kwenye Tarafa yangu ya Nguruka. Je, ni lini sasa mkandarasi atafika na kuanza kazi kuingiza umeme kwenye vijiji vyangu vya Tarafa ya Nguruka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu, ni lini?

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati namjibu Mheshimiwa Nsanzugwanko nimesema, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge anavyofuatilia maeneo hayo. Jumatano ijayo mkandarasi kwa Mkoa wa Kigoma tunamkabidhi *site* nasi tutafuatilia utekelezaji wake. Nampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Uvinza, eneo la Nguruka litakuwemo kwenye mpango huu pamoja na eneo la Ilagala na maeneo mengine. Kwa hiyo, Jumatano ijayo Mheshimiwa Mbunge wa Uvinza mkandarasi pia atafika na maeneo yake yataanza kupelekewa umeme kwa wakati mmoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sanga,

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kata ya Lyamkena, Kijiji cha Kiumba Makatani Kilabuni, Mheshimiwa Waziri anajua, walichomeka nguzo na baadaye wakaziondoa. Ni lini mtawarudisha nguzo zile ili wananchi waendelee kupata umeme? Nataka kauli ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nilifika Jimbo la Mheshimiwa Sanga na kwa kweli nilitembelea maeneo yale, eneo la Makatani, leo asubuhi kabla sijaja hapa wamepeleka nguzo nyingine 20. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakandarasi wako *site* wanaendelea na kwa vile amenikumbusha pia kesho nitamwagiza Meneja akafuatilie utekelezaji wa maeneo hayo ambayo ameyataja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maftaha na Mheshimiwa Bwanausi.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Manispaa ya Mtwara Mikindani ina mitaa mingi ambazo nguzo za umeme hazijafika na nimekuwa nikiitaja hapa Bungeni kwa muda mrefu sana, kwa mfano, Kijiji cha Mbwala Chini, Mtaa wa Naulongo, Mkunja Nguo, Kata ya Magomeni, Kata ya Ufukoni na Kata ya Mitengo maeneo mengi hayana nguzo za umeme. Nilikuwa naomba kujua kwa sababu nimeongea kwa muda mrefu ndani ya Bunge hili, kwa nini Serikali haitaki kuwapatia wananchi hawa umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Maftaha, lakini kusema kwamba Serikali haitaki, siyo kweli, ukweli ni kwamba Serikali inataka kuwapelekea umeme wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge, wiki iliyopita niliongea naye, Kijiji cha Mkunja Nguo tayari mkandarasi tumeshamtuma na ameshafanya *survey.* Maeneo mengine ya Mbwala Chini bado wanafanya *survey.* Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge maeneo yote ya Mtwara Mjini ambayo ameyataja yatapelekewa umeme na mara baada ya Bunge hili tutakwenda kukagua. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge vijiji 12 na mitaa nane ya Mtwara Mjini tutaipelekea umeme kupitia mradi huo unaoendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bwanausi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa mradi wa uzambazaji wa umeme *REA III* katika Jimbo la Lulindi ni wa kusuasua sana na mkandarasi hadi jana alikuwa hajafunguliwa *LC*. Je, Mheshimiwa Waziri anataka kuwaambia nini wananchi wa Jimbo la Lulindi ambao wanasubiri kwa hamu umeme huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Bwanausi anavyofuatilia maendeleo ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumeshafanya uzinduzi kwa Mheshimiwa Bwanausi na kijiji cha Kalipinde tayari kilishawashwa umeme na baada ya kutoka Kalipinde inakwenda kata inayofuata. Ni kweli kabisa mkandarasi hatua ya kwanza alianza kwa kusuasua kwa sababu kulikuwa na masuala ya kiutawala na kiusimamizi yaliyokuwa yanaendelea. Hivi sasa naipongeza Wizara ya Fedha imeshafungua *LC, advance payments* zimelipwa, ni matumaini yetu sasa mkandarasi atakwenda kwa *speed*. Nimhakikishie Mheshimiwa Bwanausi kwamba mara baada ya Bunge tutamfuatilia mkandarasi huyu ili awashe umeme vijiji vingi kwenye jimbo lako.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niulize swali la nyongeza. Kampuni ya *East Africa Fossils Limited* inakamilisha kazi ambayo iliachwa na Spencon ya kupeleka umeme awamu ya pili katika Tarafa ya Nkoko, Jimbo langu la Manyoni Mashariki. Kutokana na kasi kubwa ya kampuni hii kumekuwa na uhaba mkubwa sana wa nguzo za umeme. Mpaka navyozungumza hapa wameshachimbia mashimo karibu kilomita 10 nguzo hamna, kila wanapoulizwa wanasema Mufindi imezidiwa.

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini nguzo zitapelekwa katika kampuni hii ili tuweze kukamilisha suala la umeme katika Tarafa ya Nkoko?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampa pole kwa msiba alioupata hivi karibuni lakini tunafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa sana na Mheshimiwa

Mtuka na ana kata nne ambazo hatujazigusa. Mkandarasi ameagiza nguzo 2,278 na amenipa taarifa kwamba kuanzia wiki ijayo nguzo zitaanza kwenda *site.* Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mtuka kwamba maeneo yote ya kata zake 12 na hizi nne tulizoongeza yatapelekewa umeme kwa sababu sasa nguzo zinapatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa majibu sahihi. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni na Sanaa na swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini.

Na. 486

**Ligi Kubeba Majina ya Kampuni Zinazowekeza kwenye Michezo**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Je, ni vigezo vipi ambavyo Serikali imeviweka juu ya kampuni zinazowekeza kwenye michezo nchini kuruhusiwa Ligi husika kubeba majina ya kampuni hizo kama vile *Vodacom Premier League* badala ya *Tanzania Premier League*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa gharama za mfumo wa uendeshaji wa Mpira wa Miguu Duniani, Shirikishao la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)*

limelazimika kutafuta wadhamini au wafadhili wa kusaidia kuendesha shughuli za mpira wa miguu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya makubaliano yanayofikiwa kati ya Shirikisho na Wadhamini ni mdhamini kujitangaza kupitia mchezo wenyewe. Kwa mfano, ligi kuu ya Uingereza wakati ikifadhiliwa na Benki ya Backlays, ligi ilijulikana kwa jina la *Backlays English Premier League*. Hapa Afrika Mashariki kuna mashindano ya *Kagame Cup* ambayo mfadhili wake ni Rais wa Rwanda, Mheshimiwa Paul Kagame na yanajulikana kama *CECAFA Kagame Cup.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo suala la ligi kuu ya Tanzania kutumia jina la Mdhamini wa ligi hiyo, Kampuni ya *Vodacom,* linatokana na makubaliano ya kimkataba baina ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania na mdhamini wa ligi hiyo ambayo ni kampuni ya *Vodacom*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkataba huo, miongoni mwa masuala waliyokubaliana ni pamoja na mdhamini kuwa na haki ya kutumia jina lake (*Naming Right)* katika uendeshaji wa ligi hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kabisa kwenye ligi ya Uingereza ilijulikana kama *Backlays English Premier League* na siyo *Backlays Premier League*, pia hata *Kagame Cup* haikujulikana kama *Kagame Cup* inajulikana kama *CECAFA Kagame Cup*. Serikali haioni haja sasa kwamba umefika wakati wa kuitangaza Tanzania kwenye michezo na *league* yetu ikaitwa *Tanzania Vodacom Premier League*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Kampuni ya Azam wameanzisha mashindano makubwa sana yanaitwa *Azam Sports Federation Cup,* nichukue fursa hii kuwapongeza sana, je, Serikali haioni haja sasa ya

kushawishi na makampuni mengine yaweze kuanzisha mashindano ili ku-*promote* soko la Tanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi. Ajiandae Mheshimiwa Toufiq.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwalimu Mussa Sima kwa kifupi sana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pendekezo la kuweka jina la Tanzania kabla ya jina la mdhamini lina mashiko, tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kampuni nyingine kuiga mfano wa Azam, nami naunga mkono suala hilo. Natoa wito kwa makampuni mengine yajaribu kuiga mfano wa Azam ili tuweze kukusa soka katika nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Toufiq na Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa soka la wanawake limekuwa likifanya vizuri sana hapa nchini na kimataifa, lakini soka hili halina wadhamini wa kulidhamini. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhamasisha wadau mbalimbali ili waweze kulidhamini soka hili la wanawake nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, soka la wanawake pamoja na kwamba limechelewa sana kupewa uzito stahili katika nchi yetu, tayari lina wadhamini. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Toufiq kwamba kila mwaka tunazidi kuongeza juhudi za kuwapata wadhamini. Moja ya nyenzo kuu ya kuwapata wadhamini wengi zaidi ni kuhakikisha kwamba tunaomba au tunaingia mikataba na kampuni mbalimbali za utangazaji ili soka hiyo iweze kuonyeshwa *live* katika luninga zetu na hata kutangazwa katika redio mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kweli udhamini katika soka la wanawake hauridhishi na *league* ya mpira wa miguu ya wanawake inaendeshwa katika mazingira magumu sana. Ni kwa nini isiwe ni lazima kila udhamini unaopatikana kwa *league* ya wanaume uende sambamba na udhamini pacha wa *league* ya wanawake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtolea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba udhamini kwa timu za wanawake siyo mkubwa kama ulivyokuwa kwenye timu za wanaume, lakini lazima tuangalie historia kwamba *league* kuu nchi hii miaka 50 iliyopita ilianza kwa wanaume tu na tulianza na timu chache tu kama sita, lakini sasa hivi tuna timu 16 na mwaka ujao tutakuwa na timu 20. Kwa hiyo, imeongezeka ukubwa na udhamini wake lazima tuupiganie nao uwe mkubwa vilevile. Sasa hivi ndiyo tumeanza na ligi ya wanawake, tumepata udhamini mdogo, lakini tunaendelea na juhudi kuongeza ukubwa wa udhamini wa timu za wanawake kulingana na ukubwa wa *league* yenyewe.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, maswali yetu yamekwisha. Sasa ni kipindi cha wageni. Wageni wa Mheshimiwa Spika leo waliopo *Speaker's Gallery* ni Balozi Amen Kunji, Mwakilishi Mkazi wa Mtandao wa Mashirika ya Maendeleo ya *Aga Khan Tanzania,* karibu Balozi; Dkt. Harison Chuwa, *Director on College Aga Khan Health Services in Tanzania;* Dkt. John Lugala, *Director of Institute of Education Development East African Aga Khan University*; Dkt. Columber, *Academic Head School of Nursing and Midwife Aga Khan University;* Habid Maliki, *CEO Aga Khan* University; Ally Aladha, *Aga Khan Development Network;* na Nehebuchaps*, Aga Khan Develepent Network. (Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii waliopo Jukwaa la Spika ni wageni 58 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao wamegawanyika katika makundi yafuatayo: Marafiki zake watano kutoka Mkoani Mbeya wakiongozwa na Ndugu Daudi Mwakisale, Mwenyekiti wa marafiki wa Mheshimiwa Naibu Spika; na viongozi na Wachezaji 28 wa Timu ya Mpira wa Miguu, Ndato *FC* wakiongozwa na Ndugu Christon Tweve. Hawa ni washindi wa kwanza katika mashindano ya mpira wa miguu kwenye *Tulia Trust Cup* 2017 yaliyofanyika Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Wengine ni wachezaji 12 wa Timu ya Mpira wa Pete *(Netball)* wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutoka Tukuyu, Rungwe wakiongozwa na Kocha wao Ndugu Agustino Sabula. Hawa ni washindi wa kwanza katika machindano ya Mpira wa Pete kwenye *Tulia Trust Cup* 2017 yaliyofanyika Mkoani Mbeya; wafanyakazi 13 wa kujitolea wa Taasisi *Tulia Trust* wakiongozwa na Ndugu Jacqueline Boaz, Meneja wa *Tulia Trust. (Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 71 wa Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu ambao ni wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Igunga, Mkoa wa Tabora wakiongozwa na walimu wao. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Sebastian Kapufi ambao ni familia yake kutoka Mpanda Mkoani Katavi, Ndugu

Simon Sebastian Simon na Ndugu Bridget Sebastian Simon. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Edward Mwalongo ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *UDOM* wanaotokea Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Pangani Mkoani Tanga. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Juma Kombo Hamad ambao ni rafiki zake kutoka Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 39 wa Mheshimiwa Martha Mlata ambao ni *Tanzania Music Foundation* kutoka Mikoa mbalimbali. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni 25 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni Kikundi cha Wajasiriamali kutoka Mkoani Iringa wakiongozwa na Mama Mchungaji Kiwanga. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni familia yake wakiongozwa na mtoto wake, Ndugu Haroun Rashid Shangazi. Karibuni. *(Makofi)*

Pia tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Boniventura Kiswaga ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Magu, Mkoani Mwanza. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Naibu Waziri wa Uchukuzi ambao ni marafiki zake kutoka Ushetu, Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Wageni 51 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa pamoja na Mheshimiwa Innocent Bilakwate ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, wanatoka Karagwe. Karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 62 kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino Tanzania, Tawi la Arusha. Karibuni. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 66 kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine cha Mjini Morogoro wakiongozwa na Rais wao, Ndugu Laurent Peter. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jasson Rweikiza, anaomba kuwatangazia Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kuwa leo kutakuwa na kikao saa 7.00 mchana baada ya Bunge kuahirishwa.

Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania *TWPG* unatoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote walioshiriki katika shughuli mbambali zilizofanikisha hafla ya uchangishaji fedha kwa ajili ya maendeleo ya mtoto wa kike nchini. *(Makofi)*

Aidha, shukrani za kipekee za *TWPG* ziwafikie pia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania; mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu; Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Bunge la Tanzania; Vyombo vya Habari pamoja na wadau mbalimbali kwa namna walivyojitoa katika kufanikisha shughuli hiyo ambayo iliwezesha upatikanaji wa zaidi ya shilingi bilioni 1.4. *(Makofi)*

*TWPG* inawapongeza Wabunge wote walioonyesha vipaji vyao katika singeli, kwaya, sarakasi, sebene, *fashion show*, mashairi na taarabu. Taarifa kamili ya shughuli hiyo itaandaliwa na itatolewa kwenu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba mnakaribishwa kwenye hafla ya chakula cha usiku iliyoandaliwa na Mwakilishi Mkazi, Mtukufu Aga Khan, leo Jumatatu tarehe 25 Juni, 2018. Hafla

hiyo itafanyika kwenye eneo la maegesho ya Bunge mara baada ya kuhairishwa Kikao cha Bunge. Mgeni Rasmi atakuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Aidha, mnakaribishwa kuhudhuria maonesho ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Taasisi ya Aga Khan hapa nchini kuanzia saa 4.00 asubuhi.

Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports*, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Uongozi wa Bunge *Sports Club* unawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote hususan, Wabunge wachezaji walioshiriki kuburudisha kwenye Mkesha wa Usiku wa *TWPG* uliofanyika siku ya Ijumaa. Tunatambua kwamba uchovu wa wachezaji uliotokana na Mkesha wa Usiku wa *TWPG*, ndiyo ulisababisha *Ndugai Boys* kupoteza mchezo kati yao na Mbeya *Combine* dhidi ya Kapoa kwa goli 5 kwa 4. Magoli haya yalipatikana kwa njia ya *penalty* baada ya kutoka sare. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Aah, Mheshimiwa Nkamia, subiri kwanza.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Chacha.

**MWENYEKITI:** Subiri kwanza.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkamia subiri, kaa chini.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Haya.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Chacha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ryoba, Mheshimiwa Gekul, kule nyuma nani ni Mheshimiwa Maftaha?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Boni.

**MWENYEKITI:** Sasa umekaa sehemu siyo yako nimeshindwa kukujua. Tunaanza na Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niombe mwongozo wako. Nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 28(7) na kwa sababu ya kuokoa muda na kwa ruhusa yako nisingependa kuisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi wakati hatujaanza shughuli za Bunge hili tuliomba dua ndani ya Bunge ikiwa ni ishara kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaheshimu imani za dini zetu. Taasisi ya *Darul Irashadi Islamic Centre* iliyoko Dar es Salaam ni moja kati ya taasisi zilizosajiliwa kisheria na inafanya shughuli zake kwa mahusiano na Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA). Moja kati ya kazi zake ni kueneza elimu ya Uislamu na kufanya shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kulikuwa na Mashekhe kutoka nje ya nchi ambao walikuja Tanzania kufanya shughuli hizo nilizozitaja hapo awali na kwa kuzingatia urafiki kati ya taasisi za dini za nje pamoja na taasisi hii ya *Darul* ambayo ilianza mwaka 1957 kabla ya nchi yetu haijapata uhuru. Mashekhe hawa walipewa *visa* ya kuingia

Tanzania lakini *visa* yao haikuonesha kwamba kila wanapokwenda katika mkoa, lazima waombe *visa* ya kila mkoa, kwa sababu Tanzania hatuna utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi *RIO* wa Mtwara aliwazuia wasiende Mtwara na walipomwona Kamishna wa Uhamiaji Tanzania, aliwaambia atawapa taarifa, lakini kilichofuata ni kwamba Mashekhe hawa wamepewa siku saba waondoke Tanzania. Jambo hili limekuwa likitokea mara kwa mara hapa Tanzania kwa sasa kwamba kumekuwa na aina fulani hivi ya sintofahamu kati ya Serikali na baadhi ya taasisi za dini na kurushiana maneno ya hapa na pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali iko hapa naomba tupate kauli ya Serikali, hawa Mashekhe walioambiwa waondoke ndani ya siku saba na utararibu huu wa kuambiwa kwamba unapoomba *visa* ukiwa Shekhe kutoka nchi nyingine utaje na mikoa unayotaka kwenda umeanza lini. Leo nikiomba *visa* ya kwenda Marekani, siwezi kuambiwa nitaje kama naenda *Maryland*, *Massachutt* au *California* bali napewa *visa* ya kwenda Marekani *as a country*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kauli ya Serikali ndani ya Bunge hili, nini msimamo wa Serikali? Naiomba Serikali ifute huo uamuzi wake wa kuwafukuza Mashekhe ndani ya siku saba. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na mwongozo wangu unaenda TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Mara, sijui mikoa mingine, kuna wazabuni wanaosambaza vyakula shuleni, wana miaka zaidi ya mitatu hawajalipwa jambo linalopelekea kugoma kusambaza vyakula kwa sababu ya kutokulipwa madeni yao. Kwa hiyo, nilitaka nijue maana

tunakumbuka wote hapa Rais alisema anatoa shilingi bilioni 200 kwenda kulipa wazabuni, ni nini kimetokea mpaka sasa wazabuni hawajalipwa? Hii inapelekea wasilipeleke vyakula kwenye shule na wanafunzi wetu watapata shida. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako, tupate kauli cha Serikali kuna tatizo gani kati yao na wazabuni wanaosambaza vyakula kwenye shule zetu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi jambo langu ni dogo tu, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) juu ya swali ambalo asubuhi nililiuliza na Mheshimiwa Naibu Waziri alilijibu vizuri sana kuhusu fedha ambazo Serikali Kuu waliahidi kutuletea kwenye Halmashauri zetu na Mheshimiwa Naibu Waziri alisema yeye hana tatizo, wao kama TAMISEMI, isipokuwa Wizara ya Fedha mpaka leo hawajawajibu chochote na mwaka wa fedha unakwenda kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halijafanyika Babati tu, limefanyika kwa Halmashauri zote nchini, Wakurugenzi, Wenyeviti wa Halmashauri pamoja na Maafisa Mipango walikaa Dodoma siku mbili, lakini pia sisi Kamati za Fedha za Halmashauri tuliitwa kwa dharura, kuweka miradi ambayo italeta *impact* ya haraka lakini miradi itakayokamilika; nasi tulifanya hivyo na Serikali haituletei fedha za maendeleo. Naomba mwongozo wako, Waziri wa Fedha tuko naye, zimebaki siku sita mwaka kwisha, kwa nini asituambie fedha hizi zinafika lini kwenye Halmashauri zetu? Kama hawana, uungwana ni vitendo, watuambie.

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeshaeleweka. Mheshimiwa Boni.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) juu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu suala la kuchoma nyavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni-*declare interest* kwamba mimi ni nimesomea mazingira na nimekuwa nikifuatilia sana hizi shughuli za kuchoma nyavu. Viwanda vingi vinavyotengeneza nyavu hapa nchini vinatoa *material* kutoka nje na nyavu zinavyochomwa na kutangazwa kwamba milioni 300 au 400 za nyavu zimechomwa, kitaalamu nyavu hizo zinaweza kurudishwa kiwandani na kutengeneza nyavu zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Wizara isifuate utaalam huo badala ya kuwachomea watu nyavu hizi kwa kuzichukua zile na nyavu na kuzirudisha tu kiwandani na kumlazimisha yule ambaye wanamtoza faini alipie matengenezo mapya ya nyavu hizo na kurudi kwenda kufanya kazi ya kuvua? Kwa hiyo, naomba kupata mwongozo wako, ni kwa nini utaalam wa kurudisha nyavu hizi kiwandani kutengeneza nyavu mpya hauhusiki badala yake tunaharibu *material* ambayo tunatoa nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimepata miongozo minne. Mheshimiwa Boni, suala la nyavu ni la siku zote na halijatokea leo humu ndani mapema, lakini Serikali ipo, imesikia na ni vizuri ukakaa nao mkajaribu ku-*caucus* na kujua majibu ya hizi nyavu.

Mheshimiwa Gekul, wewe ulikuwa umeuliza swali la nyongeza, halikuwa swali la msingi. Hata hivyo, hoja hii Serikali imeipokea, baadaye m-*caucus* muambizane lini Serikali italeta pesa?

Mheshimiwa Ryoba, suala lako vilevile halijatokea mapema Bungeni, lakini hata hivyo Serikali imesikia na pia mta-*caucus* na mtapata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mkamia, suala hili ni zito, acha Kiti kwanza ilifanyie kazi, halafu nitakupa majibu. Katibu.

**NDG. NEEMA H. MSANGI - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**na**

**Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Nape Nnauye, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika mapendekezo haya ya bajeti ya Serikali. Nianze kwa kuipongeza Wizara ya Fedha kwa hatua kadhaa za kikodi walizozichukua. Katika mapendekezo ziko hatua nzuri za kikodi wamechukua ambazo naamini kama zitatekelezwa vizuri, basi zitakuwa na matokeo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba maeneo ambayo yameshauriwa yafanyike mabadiliko, bila shaka Serikali itayazingatia ili tupate matokeo mazuri. Naamini tumejifunza kwa bajeti mbili zilizopita, mipango na mapendekezo tuliyoyaweka na matokeo yake. Kwa hiyo, naamini hizi hatua za kikodi ni matokeo ya uzoefu huo wa nyuma. Bila shaka, kama mapendekezo na baadhi ya mabadiliko yatafanyika vizuri, basi tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, naomba nianze kwa kuzungumzia suala la korosho. Korosho kwa Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani na sasa mikoa mingine 17 imeongezeka inaanza kulima korosho; kwetu sisi ni maisha. Ukizungumza korosho, unazungumzia maisha. Kama ambavyo wakulima wa pamba wakizungumza pamba wanazungumza maisha yao. Sisi hatuna pamba, mifugo, dhahabu, almasi, maisha yetu ni korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa suala hili, napenda linapojadiliwa tuweke ushabiki pembeni, tunazungumza maisha ya watu. Bahati mbaya yapo mambo yanapotoshwa sana kwenye mjadala huu. Itakumbukwa tulilijadili hili jambo kwenye Bajeti ya Kilimo na mimi nilikamata shilingi hapa na Mwenyekiti bahati nzuri siku hiyo uliongoza kikao tukatoka nje, tukazungumza tukashindwana tukarudi hapa ndani lakini yako mambo yanapotoshwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, uanzishwaji wa mifuko hii ukiwemo huu wa pembejeo na suala zima la *export levy* siyo tu ni suala la sheria ya kawaida ni suala la Kikatiba, lina msingi kwenye Katiba ya nchi. Katiba yetu Ibara ya 136(2) inazungumza uanzishwaji wa mifuko hii kwa madhumuni maalum, kwa hiyo, ni suala la Kikatiba tusije tukapotosha likaonekana tu ni jambo tu la kawaida hivi, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, lengo la *export levy* lilikuwa na mambo mawili watu wanapotosha sana hapa na bahati mbaya wengi wanaopotosha siyo wanaolima korosho, hawapigiwi kura na wakulima wa korosho, sisi walima korosho lazima tuwe wakweli kwenye jambo hili na ukweli wetu ni kuiambia Serikali ukweli hapa. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo makubwa mawili ya *export levy*, moja ni kuendeleza zao lenyewe la korosho ili hatima yake tubangue korosho hapa nchini, ndiyo kilele

chake. Sasa lilipoanza, unaanza kwa kuongeza uzalishaji na uzalishaji unaongezwaje ni kwa kutengeneza mazingira mazuri watu wapate pembejeo, utafiti ufanyike na kazi zingine za mfumo mzima ambapo zilianza na hela ilikuwa kidogo sana, tulianza kwa kupata shilingi milioni 800. Tumeendelea mazao yakaongezeka na *export levy* inaongezeka, tumekwenda tumefikisha shilingi bilioni 100 *plus* ndiyo kelele imeanza. Tulipokuwa shilingi milioni 800 hakukuwa na kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria iliyotungwa inasema asilimia 65 itakwenda kwenye korosho, asilimia 35 itakwenda kwenye Mfuko Mkuu. Kuna dhana inajengeka kama vile mapato yote ya korosho yanatakiwa yakasaidie Kusini peke yake, hapana! Kuna hela ilikuwa inakweda Mfuko Mkuu na inakwenda kufanya kazi zingine na hatuulizi, ikiwemo kodi zinazotozwa kwa wale wakulima wa korosho na watu wengine wanaojihusisha katika mfumo mzima wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotusikitisha katika jambo hili, nilipoleta hoja hapa ilikuwa ni hoja ya kusimamia utekelezaji wa sheria. Sheria haisimamiwi, tunakumbusha isimamiwe hela ziletwe, badala ya kutuletea hela zetu Mheshimiwa Dkt. Mpango unaleta sheria ya kuzifuta kabisa asilimia 100 zije kwenu. Kwa kweli, huku ni kutudharau kwa hali ya juu ambayo haina *degree* yake. Hii si sawa! *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, hebu zungumzeni namna ya kuleta hela mliyoichukua, hii habari ya sheria mnayotaka kubadilisha toeni kwanza, *after all* Mheshimiwa Dkt. Mpango mbona unazungumza korosho na katani peke yake, mazao mengine yako wapi? Huoni kwamba kuna nia mbaya/ovu ya kupora fedha za watu? Yaani tunapora hela, halafu tunaleta sheria ya kurasimisha uporaji. Hii haiwezekani jamani! Haya ni maisha yetu, tusifike mahali tukafikishana huku, huku kubaya. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata madhila mabaya sana kwenye gesi, mbaazi imeanguka, mazao mengine yameanguka, leo mnataka kutupeleka tena kwenye korosho. *After all* Mheshimiwa Dkt. Mpango hela kidogo uliyokuwa unaipa hutaipata tena kwa utaratibu huu kwa sababu korosho inakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasema kuna matumizi mabaya ya fedha kwenye mfuko huu, hivi dawa yake ni kuufuta, dawa yake ni kuchukua hela? Mbona Hazina kuna hati chafu hatusemi! Mbona taasisi zingine zina hati chafu hatuzifungi, *no!* Tusiende huku. Haya ni maisha yetu, *you want to kill us* na hii siyo sawa. Hatuwezi kukubali katika hili, kabisa, kabisa. Leo mnatuambia kuna matumizi mabaya, kuna hata mtu mmoja mmeshtaki? Tunahalalisha kwa hoja nyepesi sana Mheshimiwa Dkt. Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba tuzungumze namna ya kuleta hela yetu. Kwa sababu hata mkitunga leo sheria, hairudi nyuma hela yetu tutaendelea kuidai. Wanaosema siyo hela yetu hiki kiatu hamkivai ninyi kinatubana siye, imetungwa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili, Mheshimiwa Dkt. Mpango hebu kuweni na huruma kidogo. Mheshimiwa Dkt. Mpango nikuambie tu mapendekezo haya yanakwenda kuiua CCM Kusini, yatakwenda kutuweka mahali pagumu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchangiaji

asipende kila wakati anapochangia jambo lake kuwafanya wananchi hawa wa Kusini hawana uwezo wa kupima jambo na badala yake kusema kwamba Kusini wataenguliwa kwa ajili ya korosho.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Hiyo siyo taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Siyo taarifa maana yake nini?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, utulivu. Mheshimiwa Nassari, Mheshimiwa Haonga, utulivu tafadhali. Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwaombe wananchi wa mikoa inayolima korosho siyo Kusini tu, mikoa 17 inayolima korosho wamsamehe mama na shangazi yangu. Kwa sababu bahati mbaya hajui analolisema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo takwimu, mama yangu inawezekana hajui, za majimbo tuliyopoteza Kusini kwa sababu na ya tatizo la ku-*mishandle* gesi katika nchi hii. Tunazo takwimu za maisha ya watu za mali, wako Wabunge humu ndani wamechomewa nyumba zao kwa sababu ya ku-*mishandle* mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema hapa nia yetu ni njema kutahadharisha kwamba hatua tunazoenda nazo mbaya, mimi nakaa kule, nimetoka kule juzi, hali mbaya. Kama tunataka tu kuziba masikio, tuzibeni masikio na tunaweza kutumia ubabe tukapisha, haitakuwa jambo baya, tutakuwa tumeamua kwa sababu katika maisha haya ni kuamua. Kuna kuamua uzima ama mauti na yote iko mbele yetu, tunaweza kuamua. Kupanga ni kuchagua, tuchagueni

tunakwenda wapi, kazi yetu itakuwa ni kutahadharisha, tukiamua kwenda huko tunakotaka kwenda twendeni na karibuni Kusini, tutayaona haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba wamsamehe mama yangu. Bahati mbaya hajui kwa sababu ni mama huyu ndiye alisimama akasema twende tukale mbaazi, nami nimewaomba wamsamehe. Leo nazungumzia korosho anasimama kutoa taarifa, naomba tena wamsamehe. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani Mheshimiwa Dkt. Mpango atuambie hizi fedha moja ya eneo ilikuwa inakwenda ni kwenye uzalishaji wa mbegu za korosho, miche ile ambayo ndiyo hiyo imesababisha tumesambaza mikoa 17 sasa na ikiwemo Morogoro, Tanga, Singida, Dodoma na maeneo mengine. Kazi ile ilikuwa inafanywa na kusimamiwa na vizuri na Kituo cha Naliendele na leo siyo tu Naliendele, Vituo vya Utafiti wa Kilimo nchi nzima hali yake taabani. Taabani kwa nini, ni kwa sababu ya haya maamuzi ya kuchukua fedha zote kuzipeleka sehemu moja. Sasa swali langu mimi ni ndogo, kama hatukuweza kupeleka hela sheria ikiwepo ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, malizia.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukiifuta sheria hii tutafanyaje? Mapendekezo yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango badilisheni uamuzi, leteni hela yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nape, muda wako umekwisha. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia, ajiandae Mheshimiwa Jasson Rweikiza. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu na namwomba anijalie niweze kumaliza kuzungumza haya ambayo nimepanga kuyachangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nianze kwa masikitiko makubwa sana juu ya mambo ambayo yanasambazwa kwa makusudi dhidi ya Wabunge wanaotetea kupelekewa pembejeo kwenye maeneo yao. Tuna taarifa jana watu wamekaa vikao, wameandaliwa waje huku kutudhalilisha Wabunge tunaowatetea wananchi wetu wapate pembejeo za korosho. *(Makofi/Vigelegele)*

**WABUNGE FULANI:** Sema, sema, sema.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote humu ndani tuna haki sawa za kutetea wananchi wetu. Anayetoka kwenye pamba ataitetea pamba, anayetoka kwenye madini atatetea madini yake na anayetoka kwenye korosho ana haki ya kuitetea korosho yake.*(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda niwahakikishie wananchi wanaolima korosho Wabunge wao tuko imara, tutapambana kuhakikisha haki hii inapatikana. Hata isipopatikana wajibu wetu tutautimiza kama wawakilishi wa wananchi kuja kuwatetea wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa sisi wabinafsi, korosho inalimwa kwa kiwango kikubwa mikoa miwili au mitatu. Wadau wa korosho tumekaa kwenye vikao vyetu tukasema korosho ilimwe mikoa 17, tukapanga mipango ya kupeleka miche na utaalam kwa pesa hizo za kutoka katika mikoa miwili, leo tunaambiwa ni wabinafsi, nani mbinafsi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanakuja kusimama wanasema wao ndiyo wanaijua korosho kushinda mtu mwingine humu ndani. Nenda Mzumbe, *thesis* yangu

*Undergraduate, Masters* nenda Sokoine nimefanyia korosho. *Undergraduate* nimeangalia upande wa *production* niliangalia *role* ya *Cashewnut Industry Program (CIP)* kwa kiasi gani imefufua zao la korosho. Kwa upande wa *Masters* niliangalia *marketing* ya *cashewnut*. Leo mtu humu anakuja mimi najua korosho, tunasema kila mtu atetee lake. Nawaomba wananchi wanaolima korosho mjiandae kuwasikiliza walioandaliwa hapa kuja kutudhalilisha. Nachokisema tudhalilisheni, tuchambeni, fanyeni chochote, lakini bado tutaitetea korosho. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikaa upande wa Serikali wakati wa gesi, niliitetea Serikali kupeleka gesi kokote Tanzania kwa sababu nilijua Serikali inatenda haki. Nilichomewa moto nyumba yangu, mabomba ya kupeleka maji kijijini kwetu yaling'olewa, mikorosho ya baba yangu ilikatwa, minazi ya baba yangu ilikatwa na katika *process* hiyo nilimpoteza baba yangu.

**WABUNGE FULANI:** Duuuu.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado nilimshukuru Mwenyezi Mungu nilisema *Alhamdulillah, Alhamdulillah, Alhamdulillah*. Kwa sababu niliona Serikali inachokifanya iko sahihi lakini kwa hili siko tayari kuchomewa moto nyumba na siko tayari kwenda kuharibiwa mali zangu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatuambia kwamba kuna ubadhirifu katika Mfuko wa Korosho tuambiane sekta gani au Wizara gani ambayo *CAG* hajatoa hoja. Kulikuwa na *ESCROW* hapa tumevunja Wizara ya Nishati na Madini na *EPA* tumevunja Wizara zilizohusika. Kazi ya Serikali ni kuwashughulikia waliofanya ubadhirifu kama upo. Kwa sababu mpaka napozungumza hapa hakuna mtu hata mmoja amepelekwa Mahakamani wala kuhojiwa kuhusu huo ubadhirifu, badala yake Serikali inaamua mwaka huu hakuna pembejeo, wakulima wetu wanahangaika, walanguzi wanauza kwa bei yoyote wanayoitaka na uzalishaji mwaka huu utapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosema kama kuna mtu amefanya ubadhirifu hata kama ni Hawa Ghasia nimefanya ubadhirifu kwenye Mfuko wa Korosho nipelekeni Mahakamani. Hao wananchi tunaowaambia Wabunge wa Kusini wabinafsi, wanataka kuigawa nchi, wana akili na wanajiongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, sheria hii ilipita katika Bunge hili, ikafanyiwa marekebisho kwenye Bunge hili na huu mfuko ulianza na wadau wenyewe. Mwenyekiti wa kwanza kwenye Mfuko huu alikuwa Shekhe Ismail ikiwa *CDF,* umekwenda ukibadilika. Sisi Mkoa wa Mtwara wenyewe tulikuwa na Mfuko wetu wenyewe wa MRATIFU, tulikuwa tunanunua pembejeo wenyewe, tunaagiza meli nzima kutoka nje mpaka Mtwara, ukauliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana amekuja Mheshimiwa Tizeba akasema anagawa *sulphur* bure tukamkatalia, tukabishana, tukapambana, tukasema Serikali hamna uwezo ninyi wa kutupa *sulphur* bure. Akatoa na akaelekeza wale waliochangia kwenye ile mifuko yetu ya kila wilaya warudishiwe pesa zao. Msimu huu wananchi hawakuchangishwa halafu baadaye hakuna pembejeo zilizonunuliwa, lengo hasa Mheshimiwa Tizeba ilikuwa ni nini? Kwa sababu miaka yote pamoja na pesa hizi bado kila wilaya ilikuwa na mfuko wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kazi yetu ni kusema *Alhamdulillah, Alhamdulillah, Alhamdulillah*. Mwenyezi Mungu anajua vilivyoko ndani ya vifua vyetu. Kama kuna nia mbaya anajua, kama kuna nia njema anajua. Tunakuomba Mwenyezi Mungu wale wenye nia njema waendelee kuwa na nia njema zao lakini wenye nia mbaya Mwenyezi Mungu wadhihirishie hapa hapa duniani. *(Makofi/Vigelegele)*

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kutoa masikitiko yangu kwa wale watu kuandaliwa, kujiandaa kuja kutudhalilisha. Aliyetuumba

Mwenyezi Mungu ndiye atatuumbua. Kama sisi ni wezi tupelekeni Mahakamani, muudhihirishie umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alituambia hapa wameagiza pembejeo zitauzwa Sh.32,000 sasa hivi nenda kaangalie kuna pembejeo za Sh.32,000 ukiacha *TANECU* pamoja na ile ya wananchi wenyewe waliyofanya utaratibu wao? *Sulphur* sasa hivi inauzwa zaidi ya Sh.50,000 na haionekani, hata kama una hela hiyo *sulphur* huioni kwa sababu wafanyabiashara walijua Serikali itanunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nia ni njema, tulitegemea mwaka huu ambapo Serikali mmeua ule mfuko wananchi wapate pembejeo kwa uhakika ili hata ikiletwa hii sheria wananchi tungekuwa na amani na na uhakika. Sheria haijabadilishwa pembejeo zimechelewa, hazijafika. Mimi na Wabunge wenzangu wa Mtwara, Mbunge wa Nanyumbu, Mbunge wa Masasi, Mbunge wa Nanyamba, Wabunge wa Mtwara, tumeenda kwa Waziri wa Fedha ofisini kwake mara chungu mzima, anabadilisha sababu. Mara ya kwanza amesema hakuna kanuni, kanuni imetengenezwa. Mara ya pili akasema mpaka baada ya *midyear review* imepita, hakuna. Hadithi kila siku kubadilisha visingizio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho sasa hivi ilikuwa inaenda mikoa 17 na lengo ilikuwa ni kuifanya Tanzania iwe mzalishaji namba moja wa korosho duniani. Ndiyo maana tukasema iende nje ya mikoa iliyokuwa inalima korosho. Wenzetu Naliendele wakafanya utafiti mwaka jana miche imefika mpaka Tabora, Dodoma, Uvinza, Morogoro, imefika Mikoa 17 halafu mnasema sisi wabinafsi. Imefikaje hiyo mikoa 17 kama siyo kwa sisi kupanga mipango mizuri. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba nia ya Serikali ni kuua mazao yote ya biashara. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kaa chini. Mheshimiwa Ghasia endelea. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kusema na Watanzania wote wajue kwamba sisi tuna haki ya kuwatetea wakulima wetu na kuitetea korosho. Napenda niwahakikishie wananchi wa Kusini, korosho haitakufa labda mikoa mingine ambayo wanaanza kujifundisha sasa hivi. Kikao chetu cha wadau tutaweka mikakati yetu mwakani tutakatana wenyewe pesa zetu na tutaagiza pembejeo. Kwa hiyo, hakuna mtu anaweza kuua zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nimshukuru tena Mwenyezi Mungu ameniwezesha kuzungumza yale ambayo nilikuwa nimeyapanga kuyazungumza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68 (7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo iko hapa mbele yetu ni hotuba ya Waziri wa Fedha. Tunapoendelea kuichangia tunaendelea kuchambua yale yaliyojiri katika hotuba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako katika jambo hili ambalo naliona tukiliacha siyo jambo sahihi sana na hasa pale Serikali inapotuhumiwa kwamba ina nia ovu ya kuwanyanyasa ama kuwadhulumu Watanzania wanaotoka katika Mikoa ya Kusini na hasa katika jambo hili la korosho. Naamini na nakumbuka vizuri, baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani, zao la kwanza ambalo liliongezeka uzalishaji kwa kusimamiwa na Serikali tena kusimamiwa na Waziri Mkuu kwa karibu lilikuwa ni zao la korosho na lilifanya vizuri sana.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mafanikio yaliyooneshwa na hasa zao hili la korosho kusimamiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, yako maendeleo mengine makubwa ambayo yamekwisha kufanyika kwenye Mikoa hiyo ya Kusini na wote tumeishuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu....

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa *order, order please!*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** *Order!* Mheshimiwa Mwambe kaa chini.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Anajadili.

**MWENYEKITI:** Mwambe kaa chini, Mheshimiwa Mwambe kaa chini.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe kaa chini.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mwambe kaa chini. Mheshimiwa Waziri malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu kwako ni kwa nini mjadala huu unaoendelea ndani ya Bunge usijikite katika kuishauri Serikali namna nzuri ya kuokoa zao la korosho...

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Badala ya kuituhumu Serikali kwamba ina nia mbovu na nia ovu kwa maendeleo ya wananchi wa Mikoa ya Kusini. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, mjadala huu usiwe kitu cha kuligawa Bunge hili.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Sasa mnataka niahirishe mjadala? Sikilizeni basi mimi niseme. Natakiwa niseme mimi.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kwa mujibu wa Kanuni nikisimama mnatakiwa mkae kimya. Pili, *you have to catch the Speaker's eye* ili nikwambie useme. Mtakaposema *out of ten* matokeo yake na nitafanya maamuzi yangu humu ndani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wabunge wana uhuru wa kujadili maoni yao kwa utaratibu wa Kibunge uliowekwa, ndiyo kazi ya Mbunge. Serikali ina majibu mazuri ya kujibu hoja za Wabunge. Kwa hiyo, tusubiri hoja zitakapotolewa, Serikali itakuja kujibu majibu sahihi. Nachokiamini majibu ya Serikali yatakuwepo na muafaka utapatikana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii ya Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wengine wanaohusika na bajeti hii huko Serikalini. Pia niipongeze Serikali kwa kazi nzuri inayofanyika katika maeneo mbalimbali, miradi mikubwa na midogo inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Katibu wa Wabunge wa CCM. Mimi ndiye nayepanga wachangiaji wa CCM

upande huu. Nalisema hili kwa sababu Mheshimiwa Hawa Ghasia amesema kuna watu wamepangwa na Serikali, hii siyo sahihi. Orodha ya wachangiaji nimepanga mimi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Naomba mnisikilize, tulia, tulia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza hebu kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, kila mtu ana uhuru kama nilivyosema wa kuchangia mawazo yake kwa mujibu...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** *No, No, No*. Nitaanza kuandika majina ya watu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kila mtu ana nafasi yake ya kuchangia ndani ya Bunge. Mimi ndiye ninayesimamia vikao.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Jesca, Mheshimiwa Frank, Mheshimiwa Hawa tulieni, mtapata taabu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Rweikiza, endelea.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya wachangiaji wa CCM nimepanga mimi. Mimi ndiyo napanga wachangiaji. Mheshimiwa Hawa Ghasia

nimempanga kuchangia leo asubuhi na kwenye orodha ya Katibu wa Bunge hayumo, basi ningemnyima kuchangia. Kama kuna orodha iliyopangwa na Serikali nisingempa nafasi achangie. Hiyo ilikuwa ni utangulizi.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza, zungumza na Kiti.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la korosho, naomba niseme tu kwamba nafikiri uelewa unatofautiana.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, hii ni *warning* yako ya mwisho. Msemaji anazungumza na Kiti, kama mtu una hoja unatoa taarifa na nikikuruhusu utasema, kama sikuruhusu unaendelea kukaa chini. Nasema tena mtapata taabu. *(Makofi/Kicheko)*

Tuendelee, Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba uelewa unatofautiana. Fedha zinazozungumziwa kwenye korosho kama alivyosema Mheshimiwa Nape ni *export levy* na inatozwa kwenye korosho inayopelekwa nje ikiwa ghafi. Lengo la kuweka *levy* hii au tozo hii ni kuzuia kupeleka korosho nje ikiwa haijabanguliwa. Siyo fedha ya mkulima, ni fedha ambayo analipishwa mpelekaji nje *(exporter)* ili asipeleke korosho ghafi. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO :** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza, kuna taarifa, Mheshimiwa Zitto.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niliomba taarifa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba analipotosha Bunge. Jambo analolizungumza limeshatolewa maelekezo na Kiti wakati Mwenyekiti ni Mheshimiwa Chenge. Anarudia jambo ambalo limeshazungumzwa na maelekezo yameshatolewa. Fedha hizi ni mapendekezo ya wakulima wadau wa korosho wanakutana kila mwaka na wanapanga utaratibu wake.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Zitto. Mheshimiwa Rweikiza endelea, hakuna taarifa tena sasa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Habari ndiyo hiyo, kaeni chini.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taarifa hiyo kama nilivyosema awali uelewa unatofautiana, haelewi nachokisema. Hizi ni fedha ambazo zinalipishwa *exporters* juu ya bei. Kwa mfano, kama bei ya kilo moja ya korosho ni Sh.3,000 *exporter* anayepeleka korosho ghafi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, uko ndani ya Bunge hauko mitaani.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *exporter* ambaye anapenda kupeleka korosho ghafi ambayo haijabanguliwa anaongezewa Sh.3,000 juu ya bei, Sh.3,000 anapewa mkulima, *exporter* anatozwa *over and above the*

*price*, ndiyo maana ya *export levy*. Tozo hii haipo kwenye korosho peke yake, ipo pia kwenye kahawa ili isipelekwe nje kahawa ambayo haijakobolewa. Ipo pia kwenye pamba ili isiende nje pamba ghafi.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bwege, nimeshasema hamna taarifa, kaa chini. Mheshimiwa Bwege, kaa chini *please!* Mheshimiwa Katani, kaa chini.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Haya, kama ni utaratibu *okay*.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 64(1)(a), inasema kwamba mtu hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria tunayoitumia ni hii, tunachokizungumza hapa ni sheria hii na huo mgao umezungumzwa upo kwenye sheria hii. Mheshimiwa Rweikiza anapoleta hoja nyepesi za kutaka kushawishi watu asome sheria hii kwanza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rweikiza endelea.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea, nasema hata kwenye pamba kuna *export levy*. *Exporter* anayepeleka pamba ghafi anatozwa.

**MBUNGE FULANI:** Iko wapi?

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Hata kwenye tumbaku, anayepeleka majani ya tumbaku nje kabla haijawa sigara anatozwa.

**MBUNGE FULANI:** Kwa sheria ipi?

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Vilevile kwenye katani, alizeti na kadhalika *export levy* inatozwa. Lengo ni kwamba asipeleke nje mbegu apeleke mafuta ili mafuta hayo yawe *processed* hapa tuongeze thamani ya zao hilo lakini pia tuwe na ajira nyingi kwa Watanzania kwenye viwanda vya mafuta. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kwa sheria ipi?

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mkulima hawezi kudai pesa hizi, ni kodi ambayo iko juu ya bei, *over and above,* juu ya bei anayoipata mkulima. Kwa hiyo, kudai siyo sawa. Ukisema hivyo maana yake hata wa kahawa, pamba, tumbaku, katani, alizeti, chai, madini nao wadai fedha hiyo itakuwa ni vurugu.

**MBUNGE FULANI:** Kaandaliwa huyo.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinatumiwa na Serikali kujenga barabara, kuboresha afya, ulinzi, kuleta elimu nzuri na kadhalika.

**MBUNGE FULANI:** Kaandaliwa huyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiswaga ajiandae Mheshimiwa James Millya.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nianze kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote wanaoshughulika kuhakikisha nchi inapata mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tulipo kwa namna ambavyo nchi inaendesha mfumo wa ukusanyaji wa kodi tunapiga hatua. Kinachohitajika ni kuhakikisha elimu ya kutosha kwa mlipa kodi inatolewa, maana wananchi wako tayari kulipa kodi kwa sababu wanajua hela yao inalindwa na inafanya kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zote zinazoshughulikia viwanda ni vizuri zikajielekeza kutoa elimu ya kutosha juu ya uwekezaji wa viwanda. Ili tuendelee kwenye sekta hii ya viwanda, taasisi hizi zinapaswa zitengeneze mfumo wa pamoja wa namna bora na sahihi ya kumwezesha mwekezaji aweze kuwekeza. Mfumo uliopo sasa siyo rafiki sana kwa mwekezaji. Kwa sababu mwekezaji anapotaka kuwekeza kiwanda kwa sasa kabla hata hajaanza uwekezaji gharama tu ni zaidi ya shilingi milioni 70. Unategemea uwekezaji wa kiwanda utafanikiwa kwa namna gani? Kwa hiyo, mifumo ijielekeze kusaidia urafiki wa kuwekeza viwanda hivi ili tupate mapato na ajira nyingi kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka *EFD mashine* kwenye *petrol station* ni zuri sana. Niombe Serikali iboreshe mfumo kwa sababu liko tatizo mfumo unapokwama hizi *petrol station* wanashindwa kuuza mafuta. Wakati mwingine mfumo unaweza kukataa saa mbili usiku, je, ataripoti wapi? Kwa hiyo, uwepo mfumo kama makampuni ya simu yalivyo ukipata tatizo unapiga kwa mtu ambaye anahusika ili akupe taarifa ambazo zinapaswa zikuwezeshe wewe kuendelea na huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri *TRA* iweke mfumo thabiti ili wakati wowote huyu anapopata tatizo apate mawasiliano na aweze kuendelea na biashara hiyo. Kwa sababu wakati mwingine wanafika mahali wanaanza kuuza lakini wanapokuja kukagua watu wa *TRA* wanapigwa faini ya shilingi 2 au 4, haisaidii sana kwa wawekezaji wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuendeleze viwanda ni vizuri kuondoa *bureaucracy* ambazo zinaendelea huko chini.

Kwa mfano, zamani pamba ilikuwa inapakiwa saa ishirini na nne na kusafirishwa kwenda viwandani saa 24. Leo Kanuni zimewekwa saa 12.00 jioni hakuna kupakia wala kusafirisha pamba, maana yake kiwanda kule kinasimama. Je, tunasaidia viwanda viendelee? Waziri mwenye dhamana na Kanuni hizi ni vizuri akaangalia jinsi ya kusaidia ili viwanda hivi vifanye kazi saa 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho. Niko hapo hapo kwenye pamba, ubebaji wetu wa pamba lazima ubebe pamba inayotoka juu ya bodi ya gari lakini iko miongozo inazuia ubebaji huo. Tunawafanya wabebaji sasa wachukue pamba kidogo na wamtoze gharama kubwa yule ambaye amebeba pamba, gharama hizi zinakwenda kwa mkulima kushusha bei ya pamba. Ni vizuri tukaangalia miongozo ambayo haina tija tukaifanyia marekebisho na tuiondoa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la *Treasury Single Account*. Nchi zote duniani zilizoendelea zinatumia mfumo huu. Mfumo huu ni salama ambao una-*control* fedha zote za Serikali na kuwa na namna fulani ambapo Serikali inaweza ku-*control* hela zake. Pia mfumo huu unaiwezesha Serikali kujua fedha zake zote zilipo na namna ambavyo inaweza kuzitumia. Mfumo huu ni mfumo ambao hata *East Africa* tumeridhia kwenye *protocol*. Kwa hiyo, ili nchi iendelee ni vizuri tukakubalina na mfumo huu, ni mfumo pekee ambao utaleta usalama wa fedha za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo Serikali imefanya vizuri sana kwenye mapendekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha lakini lipo jambo ambalo naomba ikiwezekana litazamwe upya. Mwaka jana mlipoleta mapendekezo ya kuondoa *Motor Vehicle Licence Fee* tuliona kama kazi ngumu sana lakini leo Serikali inakusanya fedha nyingi kuliko tulivyokuwa tunakusanya. Hebu liangaliwe na hili la *insurance* za magari linaweza kuwekwa wapi ili kusaidia. Badala ya kila mwaka mtu analipa, aweze kulipa kidogo kidogo, naomba liangaliwe kwa upana wake.

Naamini tunaweza kukusanya fedha nyingi na tukaondoa tatizo kubwa ambalo wananchi wanalipata wakati wote. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Millya ajiandae Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimshukuru Mungu kwa kusimama siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Wabunge wa Kusini walivyoongea, hii hoja ya korosho ni nzito na Mheshimiwa Nape ameiongelea vizuri sana, amesema ni maisha ya watu wa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naongelea tanzanite kama maisha ya watu wa Kaskazini. Bahati nzuri au mbaya nilikuwa Mjumbe wa Kamati Maalum ya Bunge iliyoundwa na Mheshimiwa Spika kuchunguza masuala ya tanzanite. Septemba 2017, tulipokuwa pale Ikulu, Mheshimiwa Rais alisema mapendekezo yote ya Kamati Teule yatatekelezwa kwa asilimia mia moja. Mpaka sasa pendekezo peke yake la Kamati Maalum ya Tanzanite ambalo limetekelezwa ni pendekezo la kujenga ukuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Simanjiro hatuna shida na ujenzi wa ukuta kwa sababu nia njema ya kudhibiti rasilimali yetu ipande bei na kuweza kui-*control* kwenye soko la dunia ilikuwa ndiyo maana ya ukuta. Pendekezo namba moja la Kamati Teule ya Bunge la kuvunjwa kwa mkataba wa kampuni ya kitapeli ya *Sky Associates* na Kampuni ya Serikali mpaka leo halijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kuridhika na kazi iliyofanywa na Kamati, ametuteulia Mawaziri watatu kwenye Kamati hiyo ikiongozwa na Mheshimiwa Doto Biteko ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ni Naibu Waziri leo, Mheshimiwa Subira Mgalu ambaye ni Naibu Waziri leo na akateuliwa mwingine ambaye ni dada yetu Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa ni Naibu Waziri. Kamati ilifanya kazi nzuri ya kizalendo, Wajumbe hawa waliamua wasichukue rushwa lakini cha ajabu sana Mheshimiwa Prof. Kabudi na Profesa Mruma wakaenda wakaketi chini na naionya Serikali ya CCM msipoachana na tabia ya huyu Mheshimiwa Profesa Kabudi mwenye sura mbili ya kuweza kuwashauri mara mbili, mmemsikia kwenye Bunge la Katiba alipokuwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba maoni ya Prof. Kabudi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa elekeza maoni yako kwa hoja iliyopo mbele yako.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo naijenga.

**MWENYEKITI:** Usitaje majina ya watu nakuomba tafadhali.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Kabudi ana sura mbili. Moja alisema ukweli kwenye suala la Katiba Iliyopendekezwa lakini baadaye anakana kauli yake. Naomba usimjibie atakuja kujibu mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa elekeza hoja yako kwa hoja iliyopo mbele yako.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Hoja yangu ni kwamba...

**MWENYEKITI:** Tuna hoja ya Wizara ya Fedha.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa hoja ni Wizara ya Fedha, hoja yangu ni kwamba kwenye suala la tanzanite mpaka leo imeshindikana kujengwa vizuri na

kutekeleza Maazimio ya Kamati Maalum kwa sababu washauri wanaomshauri Mheshimiwa Rais wanapotosha kwa maslahi binafsi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mpango unakumbuka tulivyoenda kwa Waziri Mkuu kikao kilichofanyika Dar es Salaam, uliwaona wale wawekezaji wawili Feisal na Hussein Gonga na mwenyewe ukakiri kwamba hawa siyo wawekezaji. Nami naionya Serikali bado wale ambao mnataka kuwarudishia mkataba ule hawana uwezo, mnawatetea kwa sababu ya maslahi binafsi. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, naomba kwa sauti hii kubwa ya watu wa Simanjiro, Simanjiro na tanzanite imeharibika kwa sababu ya wawekezaji hawa mnaowatetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya CCM ya Awamu ya Tano mmemuona Mheshimiwa Kikwete kwenye suala la *Richmond,* baadhi ya mapendekezo mengi ya Bunge yalitekelezwa na kwenye suala la *ESCROW* yametekelezwa. Leo hii wezi wenu ambao Kamati zote zimewabainisha, mfano kwenye Kamati ya Tanzanite mnawaacha mnakimbilia wale ambao Mheshimiwa Kikwete amewabaini, ndiyo maana Rugemalira na Harbinder Singh wapo ndani lakini wezi wenu wa Awamu ya Tano mnawaacha, mna-*negotiate* nao na ndiyo maana Acacia mnawapa mkataba tena, Serikali gani? Mlijenga heshima kubwa ya kutetea rasilimali za nchi lakini sasa mnaanza kukaa na wezi kuanza ku-*negotiate* nao, mtaelewekaje na wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa wa Sheria Mheshimiwa Kabudi, Januari, 2018 alitunga Kanuni za Madini, kifungu cha 7(f) kinasema hivi, mtu yeyote kwenye madini ya *gemstone* hawezi kupewa zaidi ya *square meter* moja lakini mpaka leo anataka kusaini mkataba na wawekezaji wenye *square meter 7.6.* Katunga mwenyewe lakini bado anavunja sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kwenye kesi ya Uingereza ya mwaka 1924 ya R v Sussex Justices, walisema

hivi kwa Kiingereza, *"not only must justice be done; it must also be seen to be done."* Tafsiri ya kawaida tu ni kwamba haki haitakiwi kusikika kuwa imefanyika lakini ionekane imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Profesa anatuambia fedha za makinikia na adhabu ambayo tuliianisha kama Wabunge haitakiwi ionekane popote kwenye bajeti ya Serikali na wananchi hawatakiwi kuambiwa lakini kwenye bajeti hii hatujaona mahali popote kama pesa ambayo inaingia kwenye bajeti ya Serikali. Tunasema hivi, kama ni fedha za umma inawezekanaje zikafichwa kama siyo kuna chochote hapo ndani? Fedha za umma lazima zijulikane lakini tunaambiwa hatupaswi hata kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kodi peke yake, naomba niwakumbushe huu mgodi ulinunuliwa kwa dola za Kimarekani milioni 2, Kamati Teule ya Bunge ya Tanzanite kwenye *angle* moja tu ya kodi za Serikali, watu hawa wanadaiwa shilingi bilioni 34. Wao wamenunua kwa shilingi bilioni 10 na wanadaiwa kwa *angle* moja peke yake shilingi bilioni 34. Mgodi huu ulitolewa kwa rushwa, haupaswi kuwa mikononi mwa watu ambao hawana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashawishi Wabunge kuendelea kufikiria kwamba rasilimali hizi hazipo na hazitadumu, tukizigawa kama njugu Watanzania watateseka. Leo Simanjiro, Mererani, Naisinyei na popote wanapotegemea tanzanite watu wamekuwa maskini sana baada ya jamaa hawa kupatiwa huu mgodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali mfikirie mara ya pili. Nimemuona Mheshimiwa Waziri Mkuu nilikuletea kilio hiki na Mheshimiwa Mpango akawepo chini, wale wanaosema ni Watanzania wamewekeza fedha zao, hakuna hata shilingi moja benki yoyote ya Tanzania iliyothibitisha wameweka fedha zao pale ndani. Ni kilio kikubwa cha watu wa Simanjiro, hatupingani na ukuta lakini maisha ya watu yameharibika kwa kuwakabidhi watu ambao hawana uwezo wa kuendesha mgodi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wana lingine, wanawafukuza kazi wafanyakazi 600. Nilileta wakati fulani malalamiko nikasema wanawafukuza watu 201, wamewafukuza wale. Leo hii wanawafukuza 600 tena, hawasaidiki, Watanzania wanateseka na watu hawa wana kiburi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama kweli mnaona ni sahihi basi Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Ngonyani ambao mmewaondoa kazini kwa sababu ya tanzanite, kama ninyi mnaona wapo sahihi basi muwaachie na wao warudi kwenye Uwaziri. Karugendo yupo, Serikali inawaonea watu wa kawaida kabisa lakini wawekezaji Awamu ya Tano haina uwezo wa ku-*deal* nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Acacia kwa taarifa zilizopo kwa sababu ya *negotiations* mbaya wanaenda kuishtaki Serikali ya Tanzania kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi kwa sababu mmeshindwa ku-*handle* suala la madini na mmeshindwa kuitetea rasilimali yetu. Kwenye hili la tanzanite mmeingizwa chaka, mnaumiza watu, watu wa Simanjiro wanaendelea kuwa maskini kwa sababu mmekabidhi mgodi wetu kwa mtu ambaye hana uwezo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka niligusie ni suala la *insurance.* Mheshimiwa Dkt. Mpango unakuja na mipango mingi sana, kuna watu wanaitwa *brokers* wa *insurance* unataka *NIC* ikusanye...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la *insurance* lazima mliangalie, *NIC* mkipeleka ile *Cobweb Theory* kwa wananchi kwamba watu wote wapeleke biashara kwa Serikali...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia ajiandae Mheshimiwa Nuru Bafadhili.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema tu kwamba jamii yoyote yenye migogoro haiwezi ikastawi na inapoelekea sasa Serikali hii inaamua kuligawa Taifa hili vipande vipande na tukiligawa Taifa tunaangamia, tunakwisha kabisa. Sheria iko hapa imesainiwa tarehe 23 Juni, 2010, kifungu cha 4, wape wana korosho haki yao na Serikali iheshimu sheria hii. Serikali isipoheshimu sheria hii hata *35%* wanayopata hawatapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ambayo haiheshimu sheria ni Serikali ya migogoro na inaliangamiza Taifa hili. Sasa unaligawa Taifa kwa sababu watu wanadai haki zao unasema eti watu wa Kusini ni wabinafsi, hapana, Taifa hili ni moja. Wimbo wa Taifa unasema tutumie hekima, umoja na amani, Taifa hili ni moja. Watu wa korosho wapewe shilingi bilioni 200 zao sasa hivi bila kigugumizi chochote. Ni haki ya Watanzania na hawa ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania leo hii tupo wapi? Nilikuwa naangalia takwimu hapa, tukiangalia *in terms of globally* kuhusu amani ya Taifa hili kwenye *Global Peace Index* Tanzania tunashika nafasi ya 51 kati ya nchi 163 wakati kwenye *happiness index* tunashika nafasi ya 153 kati ya nchi 156. Utaona ni namna gani watu wana utulivu tu wa ndani, mnasema amani, amani, hili suala la korosho litaleta machafuko katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nianze kuchangia bajeti hii. Hoja ya Mheshiwa Waziri ukurasa wa 5 anazungumzia makinikia, sisi tuwe na akili nzuri tu, tuwe na utulivu tu wa ndani, mwaka jana vigelegele vilipigwa humu ndani tukiambiwa mnapata kodi ya makinikia ya dola bilioni 190, mbona sizioni kwenye hotuba hii? Dola bilioni 190 ambazo ni zaidi ya trilioni 436 ambazo ingebidi iendeshe bajeti

ya Serikali hii kwa miaka 13 mpaka 2021 bila kukopa popote, kutoza kodi yoyote na bila msaada wa aina yoyote. *Serikali ya mazingaombwe, Serikali ya namna gani hii? Vitu vya ajabu tu. (Makofi)* ***[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]***

Mheshimiwa Mwenyekiti, *let me be sincere...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia tumia lugha za kibunge.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Nasema hivi kwa sababu mwaka jana hapa...

**MWENYEKITI:** Hilo nimelifuta kwenye *Hansard. (Kicheko)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu mwaka jana tulizomewa hapa, Serikali ikaja kwa mbwembwe hapa, Mawaziri wakasema hapa tunapata fedha hizo, Wazungu wameleta fedha kwa ndege, ziko wapi kwenye bajeti hii? Imeandikwa ukurasa wa 5 na Rais anapongezwa katika mambo 10 muhimu ambayo ameweza kuyafanyia maamuzi, tuulize dola trilioni 436 ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba hii tunazungumzia fursa ukurasa wa 16 na 17, suala la nguvu kazi na umoja wa Kitaifa, tunazungumzia pia ukurasa wa 40 huduma za jamii, afya, elimu, maji na mengineyo na ukurasa wa 79. Hotuba hii ukiiangalia kwa mapana sawa lakini kwa nini tunaamua kila siku kulifanya Taifa hili kama ni kichekesho? Nasema hivyo kwa sababu kupanga ni kuchangua, ukitaka kuliangamiza Taifa lolote ni watu wake kutokupata namna nzuri ya kujitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye elimu ukurasa wa 40, elimu ya leo hii ili watu wake wajitambue ni mazingaombwe. Niulize bilioni 107 zilizotumika kutengeneza vitabu hivi hapa 2,000 mwaka juzi, Serikali hii nani ametumbuliwa na nani ametangazwa fisadi kwenye vitabu

hivi vya bilioni 107? Vitabu hivi vinaondolewa kwenye soko sasa hivi. Serikali hii mnazungumza kila siku ni kama pata potea fulani hivi, inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa dhati kabisa, tusipokuwa na utulivu tukapanga vizuri, tukahakikisha Taifa hili linakuwa moja, rasilimali kubwa kuliko zote duniani leo hii ni rasilimali watu walioelimika vizuri, walio na utulivu mzuri na tukawa na umoja wa kitaifa Taifa letu hili ni letu sote na tutaenda mbele. Tunashuhudia magazeti, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe yakifanya uchochezi wa hali ya juu katika kuligawa Taifa lakini kusema ukweli hakuna hatua yoyote imechukuliwa, leo hii wewe ukiwa ni Mchaga basi ni laana kwa Taifa hili. Wachaga, Wachaga, Wachaga. Mpaka na kauli inatolewa na Serikali kule Iringa kwamba watu wa Kaskazini wasubiri kwanza, je, watu wa Kaskazini hatulipi kodi ndani ya Taifa hili? *No taxation without representation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wawakilishi wa Wachaga na watu wa Kaskazini. Yaani mimi nikiwa na damu ya Kichaga ndiyo dhambi kwamba mimi sifai ndani ya Taifa hili la Tanzania? Taifa tumeanza kugawana kwenye Uchaga, huyu ni Msukuma na huyu Mfipa? Leo hii mnakuja na mambo ya Kusini na mmeingia mpaka kwenye Makanisa mnawasema Wakatoliki Maaskofu ni Wachaga, ni mambo gani haya? Ni vitu vya kutisha, tunaangamiza Taifa hili na nasema... *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia, subiri kuna taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**WABUNGE FULANI:** Si ulikataa taarifa?

**MWENYEKITI:** Mimi ndiyo Kiti.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Naruhusu ma-*Chief Whip* peke yao.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe utaratibu wa Kanuni ya 64(1)(a). Mheshimiwa James Mbatia anataka kulithibitishia Bunge hili na Watanzania kwamba kuna ubaguzi mkubwa...

**WABUNGE FULANI:** Sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba ukiwa Mchaga wewe huna haki ndani ya Taifa hili na mambo mengine mengi yanayohusiana na mgawanyiko mkubwa wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao uhakika tena uhakika mkubwa, ndani ya Taasisi za Serikali na kwenye maeneo mengi tu ya uwajibikaji Watanzania wamepewa mamlaka ya kumsaidia Rais katika utendaji kazi wa Serikali bila kujali makabila yao, dini zao wala maeneo wanayotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea...

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini, subiri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea kuendekeza matamshi ya kuligawa Taifa hili kwa ukabila na udini tutafika mahali ambapo siyo sawa. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Mbatia, namheshimu sana lakini kauli hii ama aiondoe ama aithibitishe ndani ya Bunge hili kama Taifa hili linaendeshwa kwa ukabila na wale wote ambao ni Wachaga wanabaguliwa ndani ya Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya hayakuanza leo. Gazeti la Tanzanite, Gazeti la Jamvi la Habari, limekuwa likiandika huu ubaguzi, limekuwa likibagua watu, Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe yuko hapa hakuna hatua zilizochukuliwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini, umeeleweka. Mheshimiwa Mbatia, endelea.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. kaa chini. Mheshimiwa Mbatia, endelea.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana dada yangu, Mheshimiwa Jenista. Nilichokuwa nakisema hapa ni namna ya kuliweka Taifa liwe moja na nikauliza magazeti haya yamechukuliwa hatua gani? Mimi nazungumzia kulileta Taifa kuwa moja, wao wanaendeleza kuligawa Taifa la Tanzania, *that is my stand.* *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia, elekeza hoja yako kwenye bajeti.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nazungumzia bajeti, bila umoja wa Kitaifa, ndiyo nilikuwa nasema rasilimali kubwa kuliko zote ni rasilimali watu. Watu wakiwa wamoja, tukizungumzia nguvukazi inayozungumziwa ukurasa wa 40, 79 na 17, nguvukazi ya Taifa ukaileta pamoja, tutawekeza vizuri kwenye kilimo na afya za Watanzania zikiwa nzuri watazalisha vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Taifa ambalo limegawanyika na ni tunu za Taifa. Wimbo wetu wa Taifa unaanza na tunu zilizopo, suala la hekima, umoja na amani. Taifa ambalo watu wake siyo wamoja hatuwezi tukawa na amani ya Kitaifa, Taifa ambalo watu wake hawaelewani ni kazi kubwa imefanywa na Baba wa Taifa hili na hakukosea kuzungumza tunu hizi tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Marekani, Barack Obama alivyokuja Tanzania alizizungumza tunu hizi tatu kwa heshima ya Watanzania, hekima, umoja na amani. Tunatakiwa tuwe na utulivu wa ndani ili tuone Taifa hili ni moja. Mbona vyombo vingine vya habari vinafungiwa, vinaondolewa, vinavyofanya uchochezi mdogo mdogo?

**MBUNGE FULANI:** Hayo ya kwao.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Lakini haya makubwa ya kuwabagua watu kwa misingi ya ukabila wao na dini zao kimya. Dini hizi ambazo zinabaguliwa wako zaidi ya milioni 30 ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujumbe wa Kwaresma, ninao hapa, ujumbe wa Pasaka wa KKKT ninao hapa, Waraka wa Salamu za Iddi wa Jumuiya ya Taasisi za Kiislam ninao hapa, hawa ni Watanzania... *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Waislam usisingizie ni uwongo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia, elekeza mchango wako kwenye bajeti, masuala ya dini Waheshimiwa Wabunge naomba kwenye Bunge acheni.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea.

**MWENYEKITI:** Nani anapinga kauli yangu? Mmekaa kimya. Mheshimiwa Mbatia, endelea.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaenda kwenye dini, nachosema hawa ni Watanzania, kwanza wao ni raia na ni Watanzania wenzetu, pili ndiyo mamlaka yao ya kidini. Tufanyaje ili tutoke hapa kwa sababu tunaona Mataifa mengine yakisambaratika hivihivi, turudi kwa Watanzania wenyewe, kauli ya umma inayotokana na umma, umma unataka ujiongoze namna gani, turudi kwenye misingi ya maoni ya Katiba mpya. Watanzania walitoa kauli zao kwenye Katiba mpya wajiongoze namna gani, waishi namna gani, haya mambo ya kuingiliana kwa mihimili hii yatakuwaje, tukirudi kwenye Katiba mpya ndiyo hapo tutakuwa na bajeti endelevu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mbatia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nataka kutoa tahadhari kila Mbunge aheshimu mchango wa Mbunge mwenzake.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Nyamaza. *(Kicheko)*

Tena ninyi mnaosema ndiyo, Mheshimiwa Mbatia kachangia mmefurahi vizuri sana ni haki yake, haki yenu, wengine wakichangia kinyume cha Mheshimiwa Mbatia msianze fujo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Hapana, nasema kila mtu achangie kivyake.

Tunaendelea na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Nuru.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu...

**MWENYEKITI:** Dakika zako ni saba.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge hili Tukufu nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita katika suala la viwanda. Sasa hivi Serikali inasema kwamba tunaelekea kwenye Tanzania ya viwanda. Mimi nikizungumzia kuhusu Jiji langu la Tanga, Jiji lile lilikuwa na kiwanda cha mbolea, kiwanda cha chuma na viwanda vingine vingi vya watu binafsi. Jambo la kusikitisha kiwanda cha mbolea kiling'olewa mpaka mashine na hatujui mashine zile

zimepelekwa wapi. Kwa maana hiyo, uchumi huu wa viwanda hautawafikia wakazi wa Jiji la Tanga kwa sababu viwanda vingi vimekufa. Kulikuwa na Kiwanda cha Amboni, Viwanda vya Sabuni za gardenia na mbuni na kiwanda cha nguo**,** viwanda hivi vyote kwa kweli viko dhoofu na vingine vimekufa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wanakosa ajira na matokeo yake inasababisha vijana wetu wajiingize kwenye mambo mabaya ya uvutaji wa unga, wizi, ubakaji na mengine mengi sana. Serikali ingeweza kuwekeza kwenye viwanda vilevile vilivyokuwepo vikafufuliwa vingeweza kutoa ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha, kuna mwekezaji amekuja katika Kata moja ya Kirare katika Jiji la Tanga, akazungumza na wananchi wa kata husika akaelekezwa wapi ajenge kiwanda chake. Kiwanda hicho kilikuwa kijengwe katika Mtaa wa Tundaua katika Kata ya Kirare. Cha kusikitisha zaidi Diwani wa Kata ile anapinga kujengwa kwa kiwanda kile katika ile Kata ya Kirare. Kama tunavyosema, maendeleo hayana vyama, tunatakiwa tuendelee, kiwanda kikija katika mtaa husika kitawasaidia wote, hakijali huyu ni mwanachama wa chama fulani au dini fulani, watu wote watapata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji amepakubali pale kwa sababu pana miundombinu inayohitajika, umeme unapita, barabara ipo, anataka kupeleka sehemu ambayo inaitwa Mtambuuni ambako barabara yenyewe pia ni matatizo. Yote haya ni mambo ya kisiasa, Diwani huyu kweli atatupeleka kwenye Tanzania ya viwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayati Mwalimu Nyerere katika hotuba zake za miaka ya 60 na 70 alituambia kwamba, nanukuu, *"uchumi mnao, mnaukalia"*. Ni kweli tuna uchumi sisi. Tukiangalia katika masuala ya bahari, tuna bahari kuanzia Jasini mpakani mwa Tanzania na Kenya hadi mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, Serikali ingewekeza kwenye viwanda tungeweza kujengewa viwanda vya kuchakata minofu ya

samaki na wananchi wakaweza kupata ajira na Serikali ikaweza kupata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Sri Lanka nchi yao wanaiendesha kwa uvuvi tu. Kuna maziwa vilevile na kuna kila kitu lakini sasa sijui sisi tunafanya nini. Lazima Serikali iwekeze katika vitu ambavyo vina manufaa kwa sababu bahari, maziwa au mito ni viwanda ambavyo havihitaji malighafi. Mwenyezi Mungu ameshavileta vile kwa ajili ya kutusaidia sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Malaysia nchi yao inapata uchumi kutokana na michikichi. Leo Malaysia imefikia mpaka kutengeneza vichwa vya treni, ni kilimo kilichowafikisha hapo. Sisi Tanzania tuna ardhi ya kutosha, nadhani hatujafikia kulima hata nusu ya ardhi, tulitakiwa tuwekeze vizuri vilevile kwenye kilimo ili tuweze kupata tija kwa Tanzania yetu hii na kuepukana na umaskini. Umaskini tulionao siyo kuwa ni tatizo la Mwenyezi Mungu, ni kukosa mipango mizuri katika kuzalisha mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu *TRA,* kule Jijini kwetu Tanga kuna bidhaa zinaingia kutoka Kenya badala ya *TRA* kuwa na utaratibu mzuri wa kuhakikisha bidhaa hizi zimepita mpakani kihalali na zimelipiwa, watu wanapita kwa njia za panya, *TRA* wanakuja kusimama barabarani sehemu ambazo wanajificha magari yakitokea yanasimamishwa watu wanapekuliwa mizigo yao kwa hiyo atakayekutwa na mzigo ambao haukulipiwa anatoa mulungula. Pesa ile haiendi popote inaishia mikononi mwa watu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo utamkuta mtu wa *TRA* amejenga nyumba, ukiangalia mshahara wake na nyumba aliyoijenga ni tofauti. Kweli kwa hali hii Tanzania tutafika? Kwa hiyo, tuiangalie sana hii *TRA.* Watanzania wote tunalipa kodi, hata mtu ambaye hana uwezo wa kulipa kodi analipa kodi kwa sababu ukinunua kibiriti dukani umeshalipia kodi, kila unachokinunua unalipia kodi, lakini sasa wenzetu hawa...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, dakika zako saba zimekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani na Bunge mheshimu mchango wa kila mtu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Vipi?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Magereli.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Fedha pamoja na *delegation* yake yote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja ya Akaunti Jumuifu ya *TSA.* Sababu za kusema hivyo ninazo. Akaunti hii Jumuifu ya *TSA* itasaidia sana kwanza kuweka uhifadhi wa pesa pamoja, itaondoa gharama nyingi na kubwa za kibenki ambazo zilikuwa zinafanyika, itarahisisha kufanya usuluhishi wa kibenki na itarahisisha usimamizi mzuri wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Cecil Mwambe, nakuheshimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani, subiri.

Waheshimiwa Wabunge, amechangia Mheshimiwa Mbatia vizuri tu hapa, kulikuwa hakuna *disturbance* yoyote, kila mtu anapata haki ya kuchangia na kusikilizwa na kuelimishana.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sokombi. Mwacheni Mheshimiwa Jacqueline atoe mawazo yake, usiyeelimika utaelimika na mawazo yake na kama hajaelimika Waziri wa Fedha atakuja kuelimisha Bunge hili. *(Makofi)*

Naomba watu wote mheshimu mawazo ya kila mtu. Masuala ya kimbelembele, kuoneshana vidole napiga marufuku, nasema ukweli. Kwa nini hakuna kuheshimu mchango wa mwenzio? Kama yeye anapinga wewe njoo muelimishe baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ngonyani endelea.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana naomba unilindie muda wangu, umeshatumia dakika kama tatu hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo siku za nyuma tulikuwa tukijadiliana hapa kuhusu *housing levy.* Ilitokea michango mbalimbali hapa, Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanapinga kwamba kwenye hii *housing levy* tusiitoe kwenye Halmashauri zetu na kupeleka kwenye mfuko mmoja na kwamba *TRA* wao ndiyo wakusanye yale mapato, lakini mwisho wa siku tunaona faida ya *housing levy.* Pesa zile zinakusanywa zinapelekwa Hazina na zinarudi kwenye Halmashauri mbalimbali katika nchi yetu, zinarudi kwa mtindo mbalimbali kwa maana ya kwenda kufanya kazi kwenye miradi mbalimbali. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia vituo vya afya vikijengwa...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara, kaa chini.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zinapelekwa kwenye vituo vya afya.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bwege, tafadhali kaa chini.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zinapelekwa kwenye vituo vya afya na utekelezaji wa Ilani unaendelea.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona hela za korosho hazijarudi zipo huko Hazina?

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wasioitakia mema nchi hii hawatapenda utekelezaji huu ambao unafanywa na Awamu hii ya Tano ya Dkt. John Pombe Magufuli. Watu wameshashikwa pabaya, kufa kwa nyani kila mti unateleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *order, order* ndani ya Bunge.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatekeleza majukumu yake kwa vitendo. Amesimamia vizuri sana mazao mbalimbali katika nchi yetu kuhakikisha kwamba mazao haya yanaleta tija kwa wananchi likiwemo pia zao la korosho. Yeye pia ni Mbunge ambaye anatokea Nyanda za Juu Kusini ambapo ndipo korosho inapolimwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, endelea hivyohivyo, Mungu akuongoze katika maisha yako na akupe nguvu ya kutekeleza majukumu yako ipasavyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, endelea hivyohivyo, wala usirudi nyuma. (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia namna ambavyo umesimamia pale Tabora kwenye Bodi ya Tumbaku. Watu walikuwa wanafanya ubadhilifu kwenye ile Bodi, wale wote ambao walikuwa wanafuja mali ya umma wamekamatwa na wamepelekwa ndani na mpaka sasa hivi sheria inachukua mkondo wake, kwa hiyo, tunataka hivyo. Mheshimiwa Rais na wewe simama imara, utumbuaji uendelee, sasa tunahamia kwenye Bodi za Mazao mbalimbali ili wale wote waliokuwa wanafuja mali ya umma waweze kushughulikiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi naunga mkono hoja ya kwamba fedha hizi za mfuko ambazo ni asilimia 65 na asilimia 35, zote zipelekwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na sababu ninazo na nitazitoa.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, kuhusu utaratibu subiri, Mheshimiwa Bwege, umepata staili mpya ya kuchangia?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine kuna mbwa wameingia humu ndani.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Msemaji...

**MWENYEKITI:** Kanuni ipi iliyovunjwa?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 64(1)(a), kutoa taarifa za uongo. Mheshimiwa Mbunge anayesema sasa hivi anasema Mfuko wa Hazina ndiyo utatunza hela zetu vizuri kabisa. Kama husemi uongo basi tuleteeni hela zetu za korosho ndiyo tutajua kweli ninyi Hazina mnatunza fedha zetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Kicheko)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *kwa kifupi huwa sipokei taarifa za kibwegebwege.* ***[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge].***

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimuambie mtoa taarifa...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamesimama)*

**MWENYEKITI:** Kaeni chini, kaeni chini, Mheshimiwa Jacqueline, kaa chini.

**MBUNGE FULANI:** Afute kauli yake.

**MBUNGE FULANI:** Amezoea huyo lugha mbovu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MBUNGE FULANI:** Aombe radhi.

**MWENYEKITI:** Nyamazeni.

**MBUNGE FULANI:** Amezoea.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline, futa hilo neno ulilolisema siyo la Kibunge. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini yeye mwenyewe si anajiita Bwege?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeliondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka nimwambie.....

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Kaeni chini ameshafuta neno lake hilo.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeliondoa, lakini nataka nimwambie mtoa taarifa kwamba Ngaliba yeyote huwa haogopi mkojo.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anapaswa afute na aombe radhi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi namsikiliza msemaji, kama anafuta au hafuti siwezi kusikia kama ninyi mnapiga kelele. Sasa natoa onyo la mwisho kwa pande zote, Mheshimiwa Jacqueline nataka ufute hilo neno sasa hivi.

**MBUNGE FULANI:** Amefuta.

**MWENYEKITI:** Sijasikia.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuta, lakini namwambia tu mtoa taarifa kwamba Ngaliba mzuri huwa haogopi mkojo.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, samahani naomba ukae chini.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *export levy*. Suala la *exports levy* limekuwa likipotoshwa sana. Mimi naomba niseme hivi, Mheshimiwa Waziri Mkuu huyu anatoka kule Nyanda za Juu Kusini, kama jambo hili lingekuwa baya asingekubali kuweka utaratu mbovu ambao utawakandamiza wakulima.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa Zitto.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *export levy* ni pesa ambayo wanatozwa wafanyabiashara wakubwa ambao wamenunua ile korosho, haitozwi kwa mkulima.

**MHE. ABDALLAH N. MAFTAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Bodi za Korosho, Bodi za Tumbaku na Bodi zote za mazao kumekuwa na ubadhirifu mkubwa sana. Kwa hiyo, hatuwezi kukubali, ni vizuri pesa hii ikapelekwa kwenye Mfuko Mkuu ili kila mwananchi mwisho wa siku afaidike kama ambavyo tumekuwa tukifaidi fedha za *housing levy*.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufujaji huo ni kama ifuatavyo, naomba nitoe dondoo kidogo.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wa upande huu, nimesema kila mtu aheshimu mchango wa mwenzake. Kama huupendi mchango wake kaa kimya. Kama hupendi kusikiliza mchango wake toka nje nenda kapumzike *canteen*. Mnalifanya hili Bunge kama ni Bunge la kitoto na mnavyofanya hivyo mnadharau Kiti, ngojeni. Mimi nina kazi ya kufanya hapa na mimi nina jukumu la kusimamia Kanuni, Kanuni hizi ni kali sana.

Waheshimiwa Wabunge, natoa onyo la mwisho, wote mnaozomea, wote mnaopuliza nawaona na nitawachukulia hatua. Majibu ya Serikali yatatolewa na naamini majibu ya Serikali yatakuwa ni sahihi. Kama wewe hupendi kaa kimya, huwezi kukaa kimya toka nje au

nitakutoa nje. Hili sasa ni onyo la mwisho, yeyote anayefanya fujo kwa kila upande namuona na namjua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jacqueline, malizia dakika yako moja. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah, dakika zangu zilikuwa tano.

**MWENYEKITI:** Maliza ama kaa chini.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba fedha hizi za Mifuko yote ya Bodi zinapokwenda kwenye mazao hayo mbalimbali tuhakikishe kwamba zinakwenda mfuko mmoja wa Serikali, ili pesa zile ziende kutumika nchi nzima kupeleka maendeleo katika maeneo mbalimbali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Khadija Nassir.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba hii ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa, kabla sijasahau naomba kuunga mkono hoja, pia naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Naibu Waziri na *staff* wao wote kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo, naomba moja kwa moja nijikite kwenye mchango wangu na nitaanza kuongelea suala la umeme. Ieleweke kwamba Zanzibar tunaponunua umeme tunanunua umeme kama malighafi. Umeme ule tunapoununua lazima kwanza upozwe, usafirishwe lakini pia uwe *distributed* kwa wananchi ili uweze kuanza kutumika. Kinachosikitisha sana bado mpaka

sasa Serikali imeshindwa kuleta marekebisho ya sheria ili kuweza kupata msamaha wa kodi katika umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumekuwa tukilipigia kelele sana tangu mwaka 2015 mpaka leo Serikali inatuambia kwamba wako kwenye maongezi. Tumekuwa tunaona hapa mambo yanakuja kwa uharaka na yanapata ufumbuzi. Sasa Serikali ituambie ni kwa nini mpaka sasa suala hili limeshindwa kupata ufumbuzi?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kaa chini. Endelea Mheshimiwa Khadija.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilohilo kuanzia mwaka 2011, Zanzibar ilikuwa kwenye *category* ya *bulk supply* kwenye suala la umeme. Suala hilo lilikuwa linabadilika upande wa bei siku hadi siku na mpaka sasa tunavyoongea tumeondolewa kwenye *category* hiyo, tunalipia bei ya umeme sawa na wateja wengine wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei tunayonunulia umeme ni sawasawa na Zanzibar leo ikiamua kwenda kununua umeme Uganda au nchi nyingine ya jirani. Tunasema tuko kwenye Muungano na ni kweli tuko kwenye Muungano, faida hiyo ya Muungano kwenye suala hili tunaiona wapi? Naomba Waziri atakapokuja ku-*wind up* atueleze mazungumzo hayo yataisha lini na lini tutapata ufumbuzi wa suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la uchumi wa Zanzibar. Tunapoongelea uchumi wa Zanzibar tunaongelea masuala mawili, suala la biashara na utalii. Siyo dhambi kusema ili uchumi wa Zanzibar uwe *stable* tunategemea *support* kutoka Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea vitega uchumi vya kukuza uchumi wetu Zanzibar bado tunaona kuna changamoto ambazo zinatufanya tusiweze kukaa sawa. Tumekuwa tukiongea sana hapa, bado Serikali

haijaonesha nia thabiti ya kuweza kutusaidia ili kuona sasa utalii unaleta tija Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mara tulikuwa tunapokea watalii na walikuwa wakija na kutuachia fedha za kigeni. Sasa kumeanza kuwa na matatizo, kuna baadhi ya watalii ambao ni wa daraja la juu wanapoingia Zanzibar sheria inatubana kuweza kuwapa *visa on arrival*. Suala hili niliona tu lilikuwa labda ni la kisheria na lingeweza kupatiwa ufafanuzi au ufumbuzi wa haraka lakini mpaka sasa limezidi kuwa kubwa na gumu, tunapoteza watalii na mapato. Waziri utakapokuja tunaomba utueleze ni lini hili suala litafikia mwisho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuja kuongelea suala la kibiashara, naomba nijikite kwenye bandari. Kumekuwa na makandokando mengi sana kwenye bandari yetu hasa kwenye masuala ya kikodi. Tumeongea hapa, tumepiga kelele, wafanyabiashara wetu wanapotaka kuingiza mizigo kumekuwa na makandokando katika masuala ya kodi na kila siku tunaambiwa Serikali inakaa kuongea. Maongezi hayo yana miujiza gani kwamba mpaka leo yanashindwa kufikia muafaka nasi tukaweza kujipanga na kuona tunapata faida na wafanyabiashara wetu wakaweza ku-*move* vizuri? Waziri utakapokuja tunaomba utujibu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee suala la mifuko ya maendeleo. Tukiri kwamba kuna baadhi ya mifuko imekuwa ikianzishwa hapa nchini kwa faida ya kisiasa. Haya matatizo yanatuumiza sana kwa sababu tumeona tumeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na mpaka sasa umeshindwa kufanya vizuri na tumeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii na mpaka sasa umeshindwa kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yetu ifanye tathmini, je, hii mifuko imeweza kufikia malengo yake kiasi gani? Mifuko hii mingine tunaianzisha bila ya kuwa na *strong*

*legal framework* matokeo yake huku mbele inakuja kutuchanganya. Ushauri wangu kwenye hili, Serikali ikae ione namna gani itaweza kuanzisha mfuko mmoja wa Kitaifa wa maendeleo ili sasa tuweze kuendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee suala la mashirika ya umma. Katika hili, naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC,* nimeshangazwa sana na hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango. Ukurasa wa 37, naomba kumnukuu, anasema, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya tathmini na uchambuzi wa mikataba ya utendajikazi 31 iliyoingiwa baina ya Msajili wa Hazina na Wenyeviti wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma katika mwaka 2017/2018. Katika hitimisho lake, amesema matokeo ya tathmini yanaonesha wastani wa taasisi kufanya vizuri kwa asilimia 70. Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa umetudanganya waziwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sehemu ambayo tume-*fail* sana kama Serikali kusimamia mashirika yetu ya umma vizuri. Naomba tu niseme, hakuna sehemu ambayo mpaka sasa hivi tuna-*inject* hela na kuna mashirika mpaka sasa hivi yanaendesha biashara kwa hasara na bado Serikali inaingiza hela zake humo. Hapo unatuambia kwamba Serikali imeweza kufanya tathmini na asilimia 70 ya mashirika yameweza kufanya vizruri. Labda utuambie tathimini hiyo mmeifanya vipi kwa sababu kwenye ripoti ya *CAG* hatujaona hilo suala na tumeenda kukagua katika mashirika hayo mengine kuna uozo mkubwa sana. Unathubutu vipi kutuandikia kwamba mmeweza kufanya tathmini na mmeweza kuona kwamba kazi nzuri inafanyika kwenye mashirika kwa asilimia 70. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo, naomba sasa niongelee kidogo masuala ya vijana. Mimi ni Mwakilishi wa Vijana Bungeni nilitegemea katika hotuba hii angalau kungekuwa na nuru, angalau kungekuwa na ile

ndoto tuliyokuwa tunaisubiria kuona kwamba vijana tumeguswa katika bajeti hii ili ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili angalau tutakaporudi tuweze kuwaambia kwamba Serikali yetu kwenye hili...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Halima Bulembo, ajiandae Mheshimiwa Hamida Abdallah.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya tatu ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama Mbunge wa Vijana, napenda kuipongeza Serikali yangu kwa kuliweka kwenye sheria suala la mikopo ya vijana na wanawake. Ni hatua nzuri na itawapelekea Wagurugenzi wale ambao walikuwa hawawezi kufanya jambo hili kwani wasipolifanya watakuwa wanakiuka sheria na watachukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lililofanyika ni juhudi za utekelezaji wa Ilani ya chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 18 inasema, kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa mujibu wa sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo wenye masharti nafuu. Ukurasa wa 116 unasema kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendele ya Vijana kwa mujibu wa sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za vijana na wanawake ni nyingi sana. Kama tukizitilia mkazo na kusimamia utekelezaji wake sawasawa tutawanufaisha

vijana. Makadirio ya mwaka huu 2018/2019 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri makusanyo yanapaswa kuwa shilingi bilioni 735 ambapo asilimia 10 yake ni shilingi bilioni 73.5. Mwaka 2017/2018 yalikuwa ni shilingi bilioni 68 na mwaka 2016/2017 yalikuwa ni shilingi bilioni 53. Kwa miaka hii mitatu jumla yake inakuwa shilingi bilioni 186.5 ambazo zilipaswa kuwa zimetoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge wenzangu vijana humu ndani tusimamie suala hili kidete ili tuhakikishe fedha hizi zinaweza kutoka. Pia niiombe Serikali ione namna nyingine ya kuanzisha benki ya vijana kwani changamoto ya vijana siyo riba tu lakini na mfumo uliopo katika upatikanaji wa mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia taulo za kike. Serikali imepunguza gharama katika taulo za kike kwa ajili ya akina mama na wasichana lakini Kamati ya Bunge ya Bajeti imetoa maoni kwamba msamaha huu wa *VAT* hauna maana yoyote na wala bei hazitashuka na watakaofaidika ni makampuni yanayotengeza taulo za kike ya nje ya nchi. Naomba Serikali ifanye marekebisho katika msamaha huu kwa kuangalia malighafi za uzalishaji zipate msamaha pia. Kama itampendeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango aondoe kodi za mapato katika makampuni yanayotengeneza taulo za kike nchini ili bei ziweze kushuka na malengo ya Serikali yetu yatimie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli inatekeleza miradi mikubwa kama uzalishaji wa umeme, reli, usafiri wa anga na miradi mikubwa ya maji. Imefikia hatua kwamba kila kiongozi lazima apewe nafasi ya kuongoza maono yake ili kuweza kutufikishia maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusimulia kisa kimoja, Waheshimiwa Wabunge naomba mnisikilize kwa makini, kinachomhusu mtawala wa Dubai na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Falme za Kiarabu Emirates *(United Arab*

*Emirates)* Shekhe Mohammed Bin Maktoum. Shekhe Mohammed katika kitabu chake kimoja amesimulia alipokuwa mdogo baba yake Shekhe Rashid aliamua kujenga Bandari Jebel Ali, mnanisikiliza?

**WABUNGE:** Ndiyo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari hii ilianza kujengwa mwaka 1979 na kumalizika mwaka 1985. Wakati bandari hii inajengwa Dubai ilikuwa hali mbaya kiuchumi na kulikuwa na bandari nyingine ambayo wala haikuwa imejaa, *Port* Rashid lakini Shekhe Rashid aliamua kuendelea kujenga Bandari ya Jebel Ali. Wanasiasa, Mawaziri, wafanyabiashara na wananchi wote walimpinga Shekhe Rashid kwa kujenga bandari ile kwa kutumia fedha za umma ambazo tayari zilikuwa ni chache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, washauri wakaamua kumtuma Shekhe Mohammed mtoto wa Shekhe Rashid akamwambie baba yake achane na mradi wa Jebel Ali kwani haufai na hauna maana yoyote. Shekhe Mohammed akamfuata baba yake *site* ilipokuwa ikijengwa bandari ile ya Jebel Ali akamweleza baba yake. Baba yake hakumjibu chochote alimtazama. Jioni wakati wako kwenye *majlis* nyumbani akamuita mwanae Shekhe Mohammed akamwambia hivi, mwanangu acha nijenge watakuja watu wa kuitumia. Nafanya hivi kwa ajili yako wewe na ndugu zako, mtakuja kuona umuhimu wa bandari hii nikiwa sipo hai na mtakapohitaji kuijenga hamtakuwa na uwezo huo, acha nijenge watakuja kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, navyozungumza sasa hivi Bandari ya Jebel Ali ni tegemeo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbwege, nimejaribu kuwa *very patient* na najua nikisema nimtoe mmoja mtataka mtoke wote, ni bora, itasaidia vilevile kuendelesha Bunge hili vizuri. Sasa Mheshimiwa Mbwege...

**MHE SELEMANI S. BUNGARA:** Ndiyo Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Nakuomba utoke nje.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba niachie.

**MWENYEKITI:** Nakuagiza utoke nje.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Hamna tabu.

**MWENYEKITI:** Haya basi nenda nje.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Haya natoka nje, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nenda nje. Ahsante.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Naenda nje na vijana msitoke.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara nenda nje.

*(Hapa Mhe. Selemani S. Bungara alitoka nje ya ukumbi wa Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima endelea.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ya Jebel Ali sasa hivi ni kitega uchumi kikubwa Dubai, bandari imezidiwa, Shekhe Mohammed anajuta kumpinga baba yake na hivi sasa wameamua kujenga bandari nyingine kuisaidia hii bandari ya Jebel Ali kwa sababu imezidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi inayotekelezwa na Rais Magufuli inafanywa kwa ajili ya vizazi vijavyo, hasa kwa sisi Wabunge vijana. Wanaompinga Mheshimiwa Rais wampinge kwa kiasi kwa maana hapo baadaye mafanikio yatakapoonekana wataona aibu kusimama na kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno ya Shekhe Rashid kwa mwanaye Shekhe Mohamed, mtawala wa sasa wa nchi ya Dubai yanapaswa kuwa ya hekima sisi kwetu sote. Mwaka 2016 wapinzani walisimama Bungeni kupinga... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kusema Serikali isilegelege, isimame imara kutekeleza miradi yote mikubwa hapa nchini na sisi vijana tutasimama imara kutetea kwa sababu miradi hiyo ni yetu sisi vijana...*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Willy Qambalo, ajiandae Mheshimiwa Alfredina Kahigi.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kitabu cha Kamati ya Bajeti na laiti Serikali hii ingekuwa sikivu kwa maana ya kuzingatia ushauri ambao Kamati imeutoa nadhani huu mjadala wa kutumia nguvu kubwa humu ndani usingekuwepo. Kwa sehemu kubwa Kamati hii ambayo inawakilisha Bunge hili imefanya kazi nzuri sana, naomba niwapongeze. Hakuna eneo ambalo Kamati ya Bajeti imeliacha, maeneo yote ambayo ni kero kubwa wameyazingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sehemu ya pili, mahusiano ya watu wa *TRA* na walipa kodi si mazuri sana. Nashukuru jambo hili Waziri mwenyewe ameliona lakini pia Mheshimiwa Rais wakati anazindua reli ya *standard gauge* hapo Ihumwa pia alilioongelea. Nishauri watu wa *TRA* waache ubabe, kutumia nguvu na silaha wakati wanapokusanya kodi. Watanzania hatuna mila na desturi ya ulipaji wa kodi, inatakiwa tuelimishwe, Watanzania inatakiwa wapelekwe taratibu ili hatimaye wawe walipaji wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia siamini sana kama nyumba yako ile iko salama. Wakati wewe una nia njema ya kukusanya kodi, kwamba kodi yote iwe inakuja kwenye mfuko wa Serikali, wako baadhi ya watendaji wa *TRA* fedha hizo wanaziweka mifukoni. Hebu naomba uweke mikakati ya kutosha ili fedha zote zinazopaswa kukusanywa ziwe zinakuja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye eneo lingine la hii mifuko ambayo imeanzishwa kisheria kwa ajili ya malengo maalum. Ni jambo la kusikitisha kidogo Serikali ambayo tungetegemea ingekuwa mfano wa kuhakikisha fedha zile zinazokusanywa zinakwenda kwenye mifuko hiyo ndiyo imekuwa sasa inadaiwa. Nadhani Serikali mnatakiwa kuwa mfano. Huu mjadala wa korosho haupaswi kuwepo. Fedha za korosho ziende kule ambako kumekusudiwa. Mimi natoka Kaskazini lakini ndugu zangu wa Kusini kwenye hili tuko pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia najiuliza, huko Kusini kwenye korosho ndiko anakotoka Waziri Mkuu, kiongozi wa pili kwa mamlaka ya nchi hii. Sasa sijui na yeye ameelemewa na jambo hili kiasi kwamba haliendi vizuri.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Umeanza eeh, haya *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe utaratibu Mjumbe ambaye anachangia sasa hivi. Kanuni ya 64(1)(b), Mbunge anayezungumza atazungumza jambo ambalo liko kwenye mjadala na si jambo ambalo haliko kwenye mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la korosho haliendani na uteuzi wa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu alipoteuliwa, ameteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na si Waziri Mkuu wa korosho. Kwa hiyo, namuomba Mbunge ajikite kwenye mjadala wa korosho kuhusu hoja za korosho na si kumuingiza Waziri Mkuu kama vile aliteuliwa kwa ajili...

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeeleweka. Mheshimiwa endelea na mchango wako, jielekeze kwenye hoja.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nadhani muongeaji hakuwa akinisikiliza, alikuwa ana-*chart* na simu yake ndiyo maana amesimama namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ni Mbunge na ametokea huko Kusini na hawa wakulima wa korosho tunaowasema na yeye pia asilimia kubwa ya watu wake ni hao hao wanaolima korosho. Kwa hiyo, mimi najiuliza hivi jambo hili ni nani yuko nyuma yake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nenda kwenye hoja yako ya bajeti, huna haja ya kumtaja Waziri Mkuu, huna haja ya kusema ndani ya Bunge mambo ambayo huna uhakika nayo. Mheshimiwa endelea na hoja yako ya bajeti, usitaje jina la Waziri Mkuu au mtu yeyote humu ndani.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa, mbona wengine wanataja.

**MWENYEKITI:** Unazungumza mambo ya hujuma huna uhakika nayo na wala hujui.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili linakaa kwa muda wa kutosha kupitisha sheria hizi. Bunge hili lilipitisha sheria hiyo ya *export levy,* sasa kwa nini fedha hizi zisiende? Kama fedha hazipo tuambiwe fedha hazipo subirini wakati fulani, kama fedha zipo ziende. Tafsiri inayopatikana hapa ni kwamba fedha hizi zinazuiliwa kiubabe wasipate. Nyota ya Kusini ilikuwa imeanza kung'ara kwa ajili ya hiki kilimo cha korosho sasa inakwenda kuzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama kweli Serikali ina nia njema ya kuhakikisha wakulima wanainuka na wanaboresha maisha yao ni kutekeleza tu haya mambo. Hata kama mnakuja na sheria ya kufuta kodi hiyo basi lipeni zile fedha za awali, kwa nini mnataka kuzipotezea? Mimi nadhani hii si sawasawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme kuhusu wakulima wa alizeti. Nchi hii tunaagiza asilimia 70 ya mafuta ya kula kutoka nje. Tunalima alizeti, ufuta, karanga na pamba, hivi tuna matatizo gani, nani katuloga? Tunaagiza nje asilimia 70 ya mafuta yetu ambayo hata ubora wake tuna wasiwasi nao. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa nini usije na mpango wa kuzalisha alizeti kwa wingi ili tukatengeneza soko la ndani hata tuuze huko nje? Hivi kweli nchi ambayo asilimia 70 ya watu wake ni wakulima bado tunaagiza jambo rahisi kama hilo nje? Nadhani kuna jambo haliendi sawasawa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tena kuhusu mbaazi yetu. Tuna maelfu ya tani za mbaazi. Tumesikia kauli ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda kila wakati amerejea, anasema tujifunze kula mbaazi. Mama yangu, hivi nani amekwambia hatuli mbaazi labda wewe ndiye hauli. Sisi mbaazi tunakula sana lakini tunazalisha na ziada sasa hiyo

ziada tunaifanyaje? Ndiyo maana mara nyingi tumesema, hebu Mawaziri ondokeni kwenye viti hivyo nendeni mkatafute masoko ya mazao ya kilimo ya wakulima. Vinginevyo mje na kauli mtuambie zao hili X, zao hili X, lakini sisi tutalima, tutafutieni masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusu hii mifuko ambayo imeanzishwa kisheria. Nimesoma kwenye kitabu cha Kamati, Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Maji mnazo *certificates* za wakandarasi ambao wameshamaliza kazi yao, shilingi bilioni 91 hamlipi. Kila siku tunalia, tunahangaika kuhusu upungufu wa maji nchi nzima nyie hamlipi hizi fedha, tatizo ni nini? Mkandarasi umemwajiri, amemaliza kazi yako, kuna shida gani kulipa wakati Serikali hii kila mara imejinasibu mnazo fedha za kutosha? Hata mtu uliyemuajiri kufanya kazi yako unashindwa kumlipa? Kwa hiyo, nadhani kuna vitu vingine tunajitakia tu hatupaswi hata kuvijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Ofisi ya Msajili wa Hazina. Imesemwa katika kitabu cha Waziri ukurasa wa 56. Msajili wa Hazina anasimamia karibu mashirika 260 kama yangesimamiwa vizuri nadhani yangeweza kurudisha Serikalini hela za kutosha. Msajili wa Hazina hana watumishi wa kutosha, hana fedha za kutosha, hapelekewi fedha kiasi kwamba yale mashirika yaliyoko chini yake kwa kweli karibu mengi yanaripoti hasara na fedha haziji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, juzi tumesikia *TTCL* wameleta shilingi bilioni 1.5, hivi kweli hiyo ni hela ya kuletwa na kampuni kama hiyo? Shilingi bilioni 1.5 kwa mwaka wakati karibu miaka 15 walikuwa hawaleti hela. Kama haya mashirika tunayatambua ni ya kwetu hebu tuyawezeshe yazalishe fedha ziingie kwenye mfuko wa Serikali, lakini yale ambayo yameshindikana, ni sugu, ni bora kuyaondoa kwenye orodha hiyo kuliko yanabaki halafu hayaingizi kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma mashirika ya kidini na hata taasisi fulani fulani zilisamehewa Kodi ya Ongezeko ya Thamani *(VAT)* baadaye kodi hiyo ikarudishwa.

Jambo hilo limesababisha miradi mingi isitekelezeke. Mashirika ya dini yalikuwa na mchango mkubwa katika miradi ya maji na elimu lakini baada ya kurudisha kodi hiyo, yaani mtu akusaidie fedha halafu na kodi alipe. Nadhani jambo hili kama kweli lilipitishwa na Bunge hili halikuwa sahihi sana. Hebu tuweke utaratibu kwa wale watu ambao wana nia njema ya kusaidia miradi yetu basi na hii kodi tuwasamehe maana wanatoa mchango mkubwa kwenye maendeleo ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne ilikuja na ubunifu mzuri wa kujenga maabara kwenye shule zote za sekondari nchini. Serikali ya Awamu ya Tano ilivyokuja haiongelei kabisa jambo hilo kwa nguvu kubwa. Tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda, tunahitaji mafundi bila kuwa na maabara zilizosheheni vizuri watoto wetu wataendelea kupata shida na ufaulu utashuka kwenye shule zetu za sekondari. Kwa hiyo, nafikiri ni muhimu sasa Serikali ihakikishe maabara zile ambazo sehemu nyingi zimebaki magofu zikamilishwe ili watoto wetu waweze kusoma kwa nadharia lakini pia waweze kufanya ile sehemu ya *practical.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la ukusanyaji wa kodi za Serikali. Mheshimiwa Waziri wa Fedha mlituelekeza ile kodi ya majengo ilipwe Sh.10,0000 au Sh.50,000 kwa ghorofa. Wananchi wetu wamelipa kodi, lakini juzi hapa, kwa mfano kule kwangu Karatu, *TRA* yaani watu wameshalipa kodi Halmashauri mwaka huu wa 2017/2018, *TRA* wamekwenda wanagawa tena fomu walipe kodi ya ziada, yaani kuna *double charging,* haya ni maelekezo ya nani? Yaani wameshalipa kodi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Wameshalipa kodi kwa Halmashauri halafu *TRA* tena wanataka walipwe kodi hiyo. Siyo jambo sahihi, naomba Waziri atupe ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Alfredina Kahigi, Mheshimiwa Nassari na Mheshimiwa Livingstone Lusinde wajiandae.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake kwa kazi nzito ambayo wanaifanya. Nasema kwamba kazeni buti kwa sababu kazi mnayoifanya ni nzito, ni ngumu lakini niombe mkubali ushauri ambao mtapewa. Nikiangalia nyuso zenu mnaonekana siyo watu wenye kuwa na kiburi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka katika Mkoa wa Kagera. Katika Mkoa wa Kagera tulijaliwa na Mwenyezi Mungu kupata Ziwa Viktoria lakini kwa hivi sasa tunaona maji yake tu, tunaliita Ziwa la Wazungu. Mhaya alizoea kula ndizi na kitoweo chake ni samaki maana sisi si wafugaji wa ng'ombe kwa wingi, lakini sasa hivi hatuna kitoweo cha samaki, tumezuiliwa tusivue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki ndizo zilizokuwa zituletea pato hasa vijana walikuwa wanavua, wanapata hela wanasaidia familia zao lakini sasa hivi wanarandaranda tu. Nyavu zimechomwa, wengine wamekopa mikopo wameshindwa namna ya kurudisha mikopo, wamekimbia familia zao, familia zinahangaika, wanawake wengine ni wajane, wana yatima, walikuwa wanategemea kwenda ziwani kupata ajira lakini sasa haiwezekani. Mkoa wa Kagera tumekuwa maskini wa kutupa, kitu ambacho kinatusikitisha sana. Sijui Serikali ina madhumuni gani, inataka watu wa Bukoba tufe tuishe kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ziwa Viktoria kuna samaki wa aina nyingi sana lakini Serikali inajali sangara na sato tu. Kuna samaki ambao wanavuliwa na nyavu ndogo,

sasa ni mbadala gani ambao Serikali inatuwekea kusudi tuweze kuvua wale samaki wadogo, kama vifuru, dagaa, gogogo na samaki wengine ambao ni wadogo wadogo ili tuuze tupate hela za kutusaidia na mboga za kulia ugali. Mtu anakula ugali kwa maparachichi, kweli maparachichi yanaweza yakamjenga mtu? Wanawake wanajifungua, wanakosa mboga ya kula, wanakula ugali kwa maparachichi, ni kitu ambacho kinasikitisha sana. Mimi nashauri Serikali ituhurumie watu wa Kagera, itupe mbadala wa namna tutakavyovua samaki katika Ziwa Viktoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho kinasikitisha, Mkoa wa Kagera haukuwahi kuwa na watoto wa utapiamlo kiasi ambacho tunacho sasa hivi. Sasa hivi tuko katika *list* ya watu ambao tuna watoto wa utapiamlo na si watoto peke yake, hata watu wazima sasa hivi wana utapiamlo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajiingiza katika kununua dawa ambazo isingekuwa inanunua. Kwa mfano, madawa ya vitamin, Serikali ndiyo imezalisha tatizo hilo, wangekuwa wananunua dawa nyingine lakini si ya vitamin kwa Mkoa wa Kagera. Naomba Waziri hili suala mliangalie sana, ni ombi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja katika mambo ya ujenzi. Mkoa wa Kagera tuna matatizo makubwa sana. Vifaa vya ujenzi vinauzwa ghali sana nadhani kuliko mikoa mingine. Bukoba tulikuwa na meli ilikuwa inasafirisha mizigo na watu, vitu tulikuwa tunavipata kwa bei nafuu. Tangu ilipozama Mv. Bukoba, meli ya Viktoria nayo ikaharibika mpaka sasa hatuna usafiri wa majini tunatumia malori kuleta vifaa vya ujenzi na kusababisha bei kuwa ghali. Mfuko wa saruji ni Sh.18,000 mpaka Sh.20,000 watu wameshindwa kujenga. Tulipata tetemeko, mpaka leo hii watu wanalala kwenye ma-*tent.* Tuoneeni huruma watu wa Kagera, nashauri Serikali ipunguze kodi kusudi wale wanaoleta vifaa vya ujenzi kwa malori wapunguze gharama

na wale wanaoviuza nao wapunguze ili watu waweze kujenga.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mengi ya kusema lakini nitaandika kwenye karatasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, utaandika kwenye karatasi. Tunaendelea na Mheshimiwa Nassari ajiandae Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kwenye Bajeti Kuu ya mwaka huu. Kabla ya kuzungumza, kwanza naona ni vyema Waheshimiwa Wabunge tukakumbushana majukumu yetu. Ukisoma Katiba yetu, Ibara ya 63(2) inasema:-

*"63.-(2) Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Ibara ya 64 ikizungumzia madaraka ya kutunga Sheria ya Bunge, inasema:-

*"64.-(1) Mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara yatakuwa mikononi mwa Bunge".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Bunge hili ambalo lilitunga sheria, ni Bunge hili ambalo liliweka huo utaratibu wa kwamba *65%* ya *export levy* ya korosho inapaswa kurudi kwa

ajili ya kuendeleza zao la korosho na ni Bunge hili hili ambalo lilitunga hiyo sheria likasema 35% peke yake ndiyo itakwenda kwenye Mfuko huo Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mwingi ambao nimekaa ndani ya Bunge hili kwa Bunge lililopita na Bunge hili la sasa ambalo ni awamu yangu ya pili, kama kuna kitu ambacho huwa kinaharibu kazi hii ya Bunge ni kitu kinaitwa *party caucuses*; vikao vya vyama vya Wabunge. Kwa sababu leo tunapiga kelele sana kuhusu habari ya korosho hapa, mimi ninayezungumza ni Mtanzania ninayetoka Kaskazini sio mtu wa Kusini silimi korosho hata kidogo, lakini Dkt. Martin Luther King Junior aliwahi kusema, *"Injustice anywhere is a threat to justice everywhere."* Mahali popote duniani ambapo unaona kuna kuminywa kwa haki, uminywaji huo ni sawasawa na umenywaji wa haki sehemu nyingine yoyote ile duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mnataka kuwatundika tena watu wa Kusini, mwaka 2014/2015 nilikuwepo ndani wakati wa sakata la gesi, nilikuwa Mbunge mimi hapa, watu walifungwa, walipigwa, waliteswa, wengine walipotea kabisa hawajulikani walipo, leo hii wanaongea habari ya hela yao shilingi bilioni 200 halafu kuna Wabunge wanasimama hapa wanasema hapana pesa isirudi kwa wananchi. Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi sijui nikwambieje ndugu yangu, lakini kuna kitu ambacho najiuliza na ni vema na wewe ukajiuliza, *be aware my friend, be aware* isije ikawa ...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Nassari, nimeshatoa *warning,* changia mchango wako. Huna haja ya ku-*compromise* watu wengine, huna haja kabisa, changia mchango wako wa korosho usitaje watu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunielekeza, nitajaribu kufuata maelekezo yako, lakini ni vema nikakumbusha kwamba *Southern Railway* iliyokuwepo ikitoka Mtwara ikienda Nanganga mpaka Nachingwea, mwaka 1963 wakati

Mheshimiwa Kawawa wakati ni Waziri Mkuu ambaye alitokea Kusini ile reli iling'olewa. Mwaka huu 2018 Waziri Mkuu mwingine kutoka Kusini Mheshimiwa Majaliwa hapa zao la korosho linakwenda kuuwawa. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa *Chif Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie jambo hili la utaratibu. Kwenye jambo hili la utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(b) hapa hatujadili uteuzi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba unahusiana na jambo la korosho ambalo liko mbele yetu. Mheshimiwa Waziri huyu anawajibu wa kusimamia korosho, mahindi, kahawa na kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la utaratibu na kama ni jambo la utaratibu na ulishatoa *judgment* yako Wabunge wanapaswa kusimama kwenye *judgment* ambayo umeshaitoa. Mheshimiwa Waziri Mkuu hatumiki na mtu yeyote katika kulihujumu zao la korosho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante, umeeleweka vizuri. Mheshimiwa Nassari, sidhani kama utarudia tena hayo maneno na kama huna mchango kaa chini tu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nilikuwa natoa mfano tu sijazungumza habari yoyote kuhusu uteuzi wa Waziri wala Waziri Mkuu hapa ndani. Nilichokuwa nasema ni ukweli tu mwaka 1963 reli ya Kusini iling'olewa, mwaka 2018 zao la korosho liko kwenye tishio la kuanguka. Nani alikuwa Waziri Mkuu mwaka 1963 utajua wewe Mheshimiwa, nani ni Waziri Mkuu mwaka huu

utajua wewe na anatokea wapi utajua wewe, mimi sisemi tena.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari hebu kaa kwanza. Mheshimiwa Nassari unajua ni kama vile unaki-*test* Kiti au unataka Kiti ki-*react*, mimi sishindwi ku-*react*. Nilishakwambia kwamba usitaje majina ya watu ndani ya Bunge, usitaje vyeo vya watu ndani ya Bunge.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Uliniambia una udhuru nimekuruhusu, naweza kukukataza vilevile usichangie. Haonga kaa kimya.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu tafadhali, niwakumbushe na hao wanaoangalia muda hapo kwa sababu wana tabia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali ndani ya Bunge ni Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wakati wowote, awe ni nani au nani, wakati wowote. Pia nimkumbushe Mheshimiwa *Chief Whip* hapo mbele, kwenye Jimbo lake la Peramiho kwenye Kata ya Mkenda wanalima korosho. Naomba nimkumbushe tena kwenye Jimbo lake la Peramiho sehemu inayoitwa Muhukuru wanalima korosho. Naomba nimkumbushe tena jimbo la jirani kwake, Jimbo la Madaba sehemu inaitwa Ngadida wanalima korosho. (Makofi)

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mwenyekiti ulishakataa taarifa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mhagama tafadhali kaa chini, endelea. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni ili wakae wakijua kwamba Watanzania wanasikiliza na waliowapigia kura wanawaona. Akae akijua siku akirudi kule Mkenda na kule Muhukulu atakwenda kuwaambia nini wakulima wa korosho. Mimi natoka Meru silimi korosho lakini nawapigania wakulima wa korosho kwa sababu naamini Tanzania ni moja na lazima tuilinde Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumetoka kujadili hapa ndani, ukiangalia hao wakulima wa korosho ambao leo hii pesa zao zinaondoka, shilingi bilioni 200 wamepewa bilioni 10 tu, hawa wakulima hawa ambao leo hii tunawapigania hapa na pesa zao zinaondoka na Waheshimiwa Wabunge wanatetea pesa ziondoke wakumbuke kwenye bajeti iliyopita ya 2016/2017 kilimo kilipewa bajeti ya maendeleo asilimia 2.2%, peke yake. Mwaka huu wa fedha 2017/2018 ambao tunaumalizia, wakulima hawa ambao tunawatetea leo hii tunataka hela zao zirudi zikakomboe mkulima wa zao la korosho bajeti ya maendeleo kwenye kilimo mwaka mzima wamepewa 11% peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya Wabunge tuliopo hapa ndani majimbo yetu tunayowakilisha yana wakulima, wavuvi, wafugaji na watu ambao wanahitaji maji. Mwaka 2016/2017 Wizara ya Mifugo na Uvuvi wamepewa 3%, mwaka 2017/2018, Wizara ya Mifugo na Uvuvi wamepewa 0% . Wakati Mheshimiwa Spika amekalia Kiti hapo alisema hata hii shilingi bilioni 10 ambayo imekwenda kwa wakulima wa korosho, Waziri wa Kilimo hapa Mheshimiwa Tizeba alikwenda kulia kwenye Kamati. Sasa hebu mtuambie...

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Tizeba, Waziri wa Kilimo.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulisema hakuna taarifa.

**MWENYEKITI:** Huyu ni Waziri wa Kilimo.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Haya.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana michango ya Wabunge kwanza tuitoe kwa kuheshimiana na hizo sauti za kulia huko naomba uziache tuheshimiane kabisa. Mimi nakaa humu ndani kwa kuheshimu watu sana na kwa hivyo nisingependa mtu aanze kunivunjia heshima hovyo hovyo namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili hiyo habari anayoisema Mheshimiwa Nassari ya bajeti ndogo ya Wizara ya Kilimo alipaswa asikilize vizuri wakati tunaweka bajeti yetu hapa. Tulizungumza kwa namna gani *percent* hizi zinakuwa *calculated* na si tu kama anavyoweka yeye. Tulikuwa na mradi ambao haukutelezwa katika mwaka ule wa fedha, umetekelezwa mwaka huu na hicho ndicho kilichangia kushusha *performance* ya bajeti yetu ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka uliopita. Sasa haya mazungumzo ya kilimo, kilimo, kilimo kinapiga hatua kubwa.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**WAZIRI WA KILIMO:** Labda kwa taarifa yako tu...

**MWENYEKITI**: Ahsante, utakuja kuwajibu baadaye vizuri tu, endelea Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana kaka yangu Mheshimiwa Tizeba na nitaendelea kumheshimu kama mzee lakini habari niliyoisema hapa sikuisema mimi alisema Spika wa Bunge akiwa amekaa kwenye Kiti hicho na *Hansard* ipo. Kama

anabisha nafikiri *Hansard* ivutwe halafu ionyeshe, akiomba nitathibitisha kama akihitaji hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachokisema mimi ni kitu kimoja tu. Leo hii tunaongelea habari ya Serikali ya viwanda, Serikali ya Awamu ya Tano imejikita kwenye kitu kinachoitwa viwanda na inapigia kelele viwanda, kila siku Mheshimiwa Mwijage anaimba viwanda hapa. Sheria ilipopitishwa na ikisema *65%* ya hii *export levy* irudi lengo lake lilikuwa ni kuendeleza hili zao la korosho. Kwa kuanzia katika kuliendeleza zao hili ilikuwa ni kuelekea kwenda kujenga kiwanda ili tuache ku-*export* korosho ambayo ni ghafi ili tuweze ku-*process* korosho hapa hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo vilevile zilikuwa zinakwenda kwenye ujenzi huo wa viwanda vya ku-*process* korosho hapa nchini lakini unaanzia kwenye nini? Hivi unajenga kiwanda wakati huna malighafi? Lengo lilikuwa ni kuanza kuzalisha malighafi ya kutosha ili uweze kuvutia uwezo wa kujenga viwanda kwenye nchi ambapo malighafi hiyo itakwenda kulisha viwanda vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wameshatanuka wamekwenda kwenye 17 *regions in the country,* miaka ya nyuma kidogo korosho ilikuwa inalimwa Kusini peke yake. Leo tunavyozungumza mbegu za korosho zimekwenda Morogoro, Kigoma na hapa Dodoma, mikoa 17 ya nchi hii. Sasa uzalishaji umekuwa mkubwa, pesa inatakiwa ije nyingi, uzalishaji uongezeke, tafiti zifanyike, mbegu zipatikane ili tujenge viwanda ndani ya nchi tu-*process* korosho yetu wenyewe badala yake Serikali inaiba hela ya wananchi, *this is theft*, huu ni wizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna lugha nyingine kwa sababu tumetunga sheria iko hapa na sheria ilipitishwa kwenye Bunge hili. Tumesema wenyewe *65%* ya pesa hii ya *export levy* inarudi kwa wakulima, inakwenda kwenye tafiti na inakwenda kuongeza hadhi ya zao la korosho kwenye nchi. Leo hii hela mmepeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali mnasema ikishaingia kule ndani haina *identity,* nani

kakudanyanya, kuna hela inaingia benki kwenye akaunti yako ambayo haina *identity*? Huu ni wizi hakuna lugha nyingine, hakuna lugha nyingine huo ni wizi wa hela za watu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari, futa hilo neno mwizi.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna neno mwizi nimelitamka nalifuta kabisa liondoke kwenye *Hansard.*

**MWENYEKITI:** Endelea na mchango wako.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilichosema, tafadhali naomba unisikilize vizuri, nakuheshimu sana mzee wangu.

**MWENYEKITI:** Nami nakuheshimu vilevile, heshimu Kanuni siyo mimi. Mimi wala usiniheshimu Kanuni tu hapa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Tatizo amesema wizi siyo mwizi.

**MWENYEKITI**: Endelea na mchango wako umebakiza dakika moja tu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Sitakuwa tayari kufuta kauli ambayo sijaisema. Nimesema kilichofanyika ni wizi na ahsante sitaendelea kuchangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali. Vilevile nimshukuru Mungu kwa kutupatia nafasi hii Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili tuweze

kuisaidia Serikali kwa michango yetu mbalimbali iweze kuboresha utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno mengi yamesemwa na ni vizuri yakasemwa kwa sababu humu ndimo jumba la kusemea maneno hayo. Nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna wengine wanasema viongozi hawana huruma, wakatoa mpaka mfano wa Mzee Mandela namna ambavyo mlinzi wake aliyemtesa jela ndiye aliyekuwa anamlinda lakini hawakufika mbali tu kujua kwamba kila binadamu anaukomo wa uvumilivu. Mandela pamoja na sifa zake zote hizo lakini Winnie Mandela hakumsamehe. Kwa hiyo, inaonesha kwamba binadamu ana kiwango fulani cha uvumilivu. Viongozi wengine wamo humu, wa CCM wapo ambao uvumilivu ukifika mwisho wanafukuza, wa CHADEMA wako ambao uvumilivu ukifika mwisho wanafukuza, kwa hiyo, viongozi kama binadamu nao wana ukomo wa uvumilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti Kuu ya Serikali, lengo letu ni kuishauri Serikali makusanyo yanayoingia kwenye Mfuko Mkuu wa Taifa, ambao zamani tulikuwa tunasema una matundu walau Awamu ya Tano umezibwa, yaweze kufanya kazi ya kuleta maendeleo kwa nchi nzima, ndilo lengo kubwa. Tunaishauri Serikali makusanyo wanayokusanya na kuyaingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali yafanye kazi ya kuliendesha Taifa zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imesemwa sana kuhusu *TRA* namna ya kukusanya mapato. Vilevile lugha za watendaji wetu wakati wa kukusanya mapato hayo lazima ziwe rafiki ili ziwafanye walipa kodi wawe marafiki na wanaokusanya kodi na tuweze kupata mchango mkubwa wa kuendesha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani tuna kada mbalimbali, kuna wanasheria humu waliobobea, hivi tunashindwa nini kulitolea ufafanuzi neno hili na sakata hili la korosho na likaisha? Maana inakuwa kama vile tuna

Wabunge ambao hawajasomea sheria kabisa. Tunao Wabunge hapa wanasheria waliobobea kutunusanua katika jambo hili...

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** *(Aliongea bila kipazasauti)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Naomba unyamaze mzee, wewe umechangia mimi sikusema, utanitoa nje nitakupa vitu halafu...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Nassari.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Nimemuona, ni rafiki yangu ndiyo maana nimemheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tunasueni kwenye jambo hilo. Kama ni sheria ya Bunge inayosema *export levy* itatozwa kwa wafanyabiashara wanaosafirisha korosho nje na ikiwa na nia ya kuendeleza zao la korosho ndani ya nchi na makusanyo yapo na mgawanyo upo, tatizo liko wapi kutunasua hapo ili tuweze kutoka kwenye eneo hilo? Mimi sioni kama kuna haja ya sisi kutukanana, Bunge kupanda morali wakati hili jambo liko wazi na mmeliwekea sheria. Tuna haja gani ya kuwa na wanasheria, ndiyo maana wakati mwingine huwa nasema, jamani kama kitu ni ukweli tusimamie ukweli, kama tunataka kufanya mabadiliko tufanye mabadiliko ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lilikuwa tunapoweka kodi pengine tuzuie korosho ghafi zisiende nje, tusiwape watu kazi kwenye viwanda vyao, tuzalishe viwanda vya ndani kama viwanda vya ndani havijafunguliwa tatizo liko wapi? Leo Wabunge, hivi Serikali ya Awamu ya Tano ina shida ya kukamata mtu? Wabunge leo wanaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba walioiba wakamatwe jambo hilo si lifanyike mara moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana walioiba wapo, wanafahamika, walioua hivi vyama wapo na wanafahamika, wameumiza familia za watu, wakamateni,

wapelekeni mahakamani. Hivi leo mpaka mtu anaomba kukamatwa, Serikali hapa mko wapi? Kamateni hawa watu wapo na wengine hela hizo za wizi kule zimewaingiza Bungeni kamateni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye makusanyo ya Serikali tuliweka tozo ya maji, hela ile iendelee kutoka kwenda Wizara Maji ili wananchi wapate maji. Bunge hili vitu vyote inavyoamua vifanyiwe kazi na Serikali vituletee manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wamezungumza sana na mimi nataka nizungumze. Kwanza mimi licha ya kuwa Mbunge ni mjumbe wa *NEC* wa Chama kinachotawala. Humu ndani tunapochangia tujiepushe sana kuingilia kazi za watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kwamba CCM ikifanya hivi itashindwa sisi Wabunge humu ndani hakuna mwenye madaraka ya kuizungumzia CCM. Wako watu waliochaguliwa wanaofanya tathmini ya chama na wanaotoa matamko ya chama, tuwaachie waendelee kufanya tathmini hiyo. Kazi yetu sisi Wabunge wa CCM ni kuikosoa, kuirekebisha, kuisimamia Serikali na kuitetea pale tunapoona inaonewa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za nje tutakwenda kupambana nazo nje. Hapa hakuna Mbunge wa CHADEMA hata siku moja amewahi kusimama na kusema CHADEMA itashindwa kwa uamuzi huu, sijawahi kusikia. Kwa hiyo, kwa CCM, nasimama sasa kama *m-NEC,* bosi wenu, napiga marufuku kwa Mbunge wa CCM kuzungumzia chama humu. (*Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Sema, sema.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni chama chenye Serikali, tunavyo vikao vya kukosoana, tutavitumia hivyo si ndani ya Bunge. Ndani ya Bunge tuzungumze maslahi ya wananchi waliotuchagua, tuyazungumze kwa nguvu kwa msisimko lakini kuweka CCM

kwenye hatari ya kushinda au kushindwa si jambo tunalo liruhusu kuzungumzwa humu ndani ya Bunge. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wabunge wangu hamna lugha ya kumsifia Rais na kukitetea chama nyamazeni kimya lakini msizungumze kukikosoa chama kwa nia ya kukidhalilisha humu. Wasemaji wa CCM hawamo humu, tutazungumza nao kule nje na wao watasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ku-*boost* uchumi wa ndani, Mheshimiwa Dkt. Mpango, mimi sijasomea uchumi, lakini ukilipa wakandarasi wa ndani, watu waliofanya kazi wanaoidai Serikali utau-*boost* uchumi. Watu wameleta madeni mmeyahakiki, Mheshimiwa Rais amesema mnatoa shilingi bilioni 200 kuanza kuwalipa hamlipi, nyumba zao zinauzwa, haiwezekani. Lazima kuwe na utaratibu wa kuu-*boost* uchumi wa ndani, unapowalipa watu ambao wamefanya kandarasi za ndani una-*boost* mzunguko wa pesa kwenye nchi. Jamani hata kama hukwenda shule mtu unaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaishauri Serikali badala ya kuendelea kila siku kufanya uhakiki juu ya uhakiki, wale ambao tayari mmeshakubali kwamba hawa madeni yao ni sawa walipeni, shida iko wapi? Mkiwalipa watafanya biashara wataendelea kukopa. Mpaka sasa hivi kuna watu nyumba zao zimeshindwa kuuzwa kwa sababu hakuna mtu mwenye uwezo wa kuzinunua. Sasa hii biashara gani? Kama wameleta madeni yao na mmeshayafanyia kazi walipeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo ya maji tumesema ikusanywe zipelekwe Wizara ya Maji ili watu wapate maji, lakini wakandarasi wanaoshughulikia hizo kazi hawalipwi, sasa watasambazaje maji? Wakandarasi wa umeme hawalipwi watasambazaje huo umeme? Mpeni Waziri pesa yake ili apeleke kwa wakandarasi wananchi wapate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kazi zime-*stop* kwa sababu tu hela haishuki, lakini hela ikishuka kazi kubwa itafanyika na watu watamaliza miradi yao, wataomba mingine na wananchi wataendelea kutumia. Badala ya vijiji vyote kupata umeme, sasa hivi nyumba tisa, maana yake nini? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Yosepher Komba, Mheshimiwa Lathifah Chande na Mheshimiwa Rose Kamili.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Niliwataja Mheshimiwa Yosepher Komba, Mheshimiwa Lathifah Chande na Mheshimiwa Rose Kamili.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda Kiti kimebadilisha muda wa uchangiaji na sasa uchangiaji sasa utakuwa dakika tano tano. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Yosepher Komba.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naomba nimshukuru Mungu kwa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafuatilia mjadala wa bajeti humu ndani hasa hii Bajeti Kuu kuhusiana na suala la fedha za korosho zaidi ya shilingi bilioni 200. Nimeangalia *Finance Act* ya 2010, nimeona hilo suala limeandikwa kwenye

*section* 17A kwamba ni suala la kisheria. Pia nimekuwa nikijiuliza kwa nini Serikali wanafikia hatua ya kuleta mvutano wote huu. Nimepata jibu moja kwamba Serikali imekuwa na tabia ya kuwa na wivu na wananchi. Chochote ambacho wananchi wanakigundua au chochote ambacho wananchi wanapatanacho faida mara nyingi Serikali inaingilia. Wakulima wa korosho wamejitahidi kwa nguvu zao wamezalisha, mmeweka *export levy* wamelipa, badala ya Serikali kuendeleza hili zao wanaona hawa wakulima wa korosho wananapata faida wanataka sasa hivi wachukue asilimia 100 wakati asilimia 65 imewashinda kurudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasema Serikali ina wivu kwa sababu tumeona kwenye vyanzo vya mapato vya halmashauri. Halmashauri zetu zilikuwa zinakusanya vizuri sana baada ya Serikali kuona kwamba halmashauri zinafaidi, zinafanya vizuri kwenye mapato wameamua kuingilia kati na matokeo yake tunayaona. Kwa sasa halmashauri zetu zinakufa, zinaishi kwa shida, kwa sababu mapato ambayo Serikali wanayachukua kwenye halmashauri zetu ya mabango na majengo hawarudishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika suala la madeni ya Serikali, Serikali ina Deni la Taifa ambalo sasa hivi ni *almost fifty trillion* kwenda juu. Serikali vilevile inadaiwa na wakandarasi zaidi ya shilingi bilioni tisini na moja. Pia Serikali inakopa mikopo ya biashara ambayo kwa namna moja au nyingine haikuzi uchumi kwenye kile kiwango kinachotakiwa na Serikali inadaiwa na watumishi wa umma. Serikali ina madeni meng ambapo ukifuatilia madeni haya hawakupaswa kuwa nayo. Kwa mfano, mmetafuta wafanyakazi hewa mmewatoa lakini wale ambao siyo hewa bado wanawadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango umejinasibu na Wizara yako kupitia *TRA* kwamba ninyi mnakusanya mapato, mnavuka lengo. Kama mnavuka lengo kwa nini mnakuwa na madeni mengi kiasi hiki kwenye Wizara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* imekuwa ni chanzo cha matatizo kwa wafanyabiashara hasa kwenye sekta binafsi. Nimejaribu kupitia hapa kidogo kodi ambazo mtu ambaye anataka kuanzisha biashara au mwekezaji anatakiwa alipie, kuna utitiri wa tozo. *TRA* wana tozo nyingi na mamlaka nyingine nazo wana tozo nyingi kiasi kwamba mtu kabla hajaanza biashara nusu ya mtaji aliokuwa nao inabidi alipie kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia ukitaka kuanzisha biashara Tanzania lazima usajili biashara *BRELA* ambapo si bure; ulipe *TRA* Kodi ya Mapato (*Income Tax);* ulipe Kodi ya Zuio *(Withholding Tax);* ulipe *Pay as You Earn (PAYE);* ulipe gharama za *OSHA (Occupational Health and Safety Authority);* ulipe Kodi ya Ujuzi *(Skill Development Levy* ); ulipe leseni ya biashara katika Manispaa au Halmashauri; ulipe gharama za zima moto (*fire);* ulipe kwenye Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)*; ulipie kununua vyeti ya *TBS* na lazima ulipe kununua *EFD mashine.* Hizo ni baadhi ya tozo ambazo wafanyabiashara wanatozwa na mamlaka mbalimbali za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huo, hayo mapato ambayo mnayahangaikia na ambayo mnasema mtayakusanya kwa kiwango cha juu hamtafikia lengo kwa sababu mmekuwa wasumbufu sana kwa wafanyabiashara. Mkiona mfanyabiashara ameongeza mtaji wake au biashara imekuwa ndipo *TRA* watapishana usiku na mchana kwa huyo mfanyabiashara. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri, kaa vizuri na wafanyabiashara hasa sekta binafsi waambie hao *TRA* wako tunahitaji mapato kwenye nchi hii kwa ajili ya maendeleo na hatuhitaji usumbufu ambao si wa lazima kwa wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee suala lingine la vyanzo vya mapato vya halmashauri. Nimeliongea hapa mwanzoni lakini bado kuna shida kubwa ya ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida kubwa ya vyanzo hivi vya mapato ambavyo halmashauri wameachiwa na Serikali Kuu lakini hata vile ambavyo Serikali Kuu imechukua ikasema itarudisha ...

**MWENYEKITI**: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Lathifah Chande, Mheshimiwa Rose Kamili na Mheshimiwa Katani wajiandae.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, napenda kuzungumzia kuhusiana na suala zima la *export levy* kwenye zao la korosho. Awali ya yote, napenda kuipongeza Bodi ya Korosho kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kuweka bei elekezi ambayo iliweza kuonesha mwanga kwa mkulima wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uliwekwa mfumo ambao ulipitishwa hapa Bungeni wa hii *export levy* ambapo asilimia 65 ilikuwa inatakiwa irudishwe kwa wakulima kwa ajili ya kuendeleza zao hili la korosho. Mfumo huu ulienda vizuri kiasi kwamba pembejeo na dawa mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza zao hili la korosho zikawa zinapatikana kwa bei nafuu. Vilevile hata vituo vyetu vya utafiti, mfano mkubwa Kituo cha Naliendele kiliweza kufanya utafiti wa zao hili. Kwa muda mrefu tulikuwa na vituo hivi vya utafiti lakini kutokana na ukosefu wa fedha havikuwa vinaweza kujiendesha. Safari hii ilipatikana miche iliyopandwa kwenye maeneo mbalimbali nje ya Kusini na sasa mikoa mbalimbali ina uwezo wa kuzalisha zao hili la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuja na mfumo huu sasa wanataka kubadilisha ile asilimia 65 ambayo ilipaswa irudishwe kwa wakulima ipelekwa Serikali Kuu, sioni wana dhamira gani. Kwanza ndani ya miaka miwili zinadaiwa takribani shilingi bilioni 211, fedha ambazo mpaka leo hii hazijarudishwa kwa ajili ya kufanya mambo ya maendeleo katika sekta hii ya korosho. Hili mnalotaka

kulipitisha sasa hivi hatuwezi kukubaliana kwa sababu kama ni suala la kusema kumekuwa na ubadhirifu katika sekta ya korosho, kwa nini Serikali ambayo ndiyo *law enforcers,* yaani ndiyo imeshikilia dola, wana uwezo wa kujua nani aliyeiba pesa, pesa zimekwenda kwa nani, kwa nini wasifanye *investigation* ya kutosha? Kwa nini wasichukue jukumu la kuweka jicho zaidi kwenye Bodi ya Korosho kama ndiko kwenye ubadhirifu au kwenye hivyo vyama vya msingi lakini zoezi zima hili la kupeleka fedha liendelee kwani ndilo hilo ambalo limeweza kuwakwamua Watanzania wanaoishi katika mikoa ya Lindi, Ruvuma pamoja na Mtwara baada ya mambo mbalimbali kujitokeza katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuja mradi wa *LNG* ambao tulitegemea kabisa kwamba ungeweza kuwakwamua wana-Kusini, leo hii ule mradi hatuelewi umeishia wapi. Tuna *Selous Game Reserve* ambapo sehemu kubwa ya hifadhi hii iko katika maeneo ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kwa asilimia kubwa lakini makao makuu yameenda kupelekwa wapi Ruaha. Sasa hivi hii pesa asilimia 65 nayo mnataka kuitoa, mnamaanisha nini? Maana yake ni kwamba Serikali haina dhamira nzuri kwa watu wa Kusini, mnataka mtupeleke wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hili suala mliangalie kwa undani zaidi na ikibidi mtafute njia ya kufanya *control and monitoring,* kwa sababu hii asilimia 65 hata mkisema ipelekwa Serikali Kuu kama ni ubadhirifu bado ni vilevile zitaibwa zikiwa hukohuko. Kikubwa itafutwe *mechanism* ya kufanya *control and monitoring* ili fedha hizi ziweze kuwa na usimamizi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, mfano naweza nikasema leo hii tuwe tuna shamba Njombe na kuna mtu amefanya ubadhirifu, mnafanya nini hapo? Mnatafuta njia ya kulihamisha lile shamba liende Dar es Salaam, ni suala ambalo linawezekana? Kusema kweli hili ni suala ambalo linahitaji kuangaliwa na hatujui labda ni *conspiracy* ya watu wachache tu na dhamira kuu tunaona ni kwa ajili ya kuwakandamiza wana-Kusini kwa sababu zao lililobaki ni hili

ambalo tunalolitegemea, hatuna kitu chochote ambacho kinaweza kuwezesha uchumi wa watu wetu wakaweza kukidhi maisha yao katika Kusini yetu. Limebaki zao hili ambalo leo hii sijui mnataka kutupeleka wapi. Wana-Kusini tutaishia kuwa maskini mpaka lini? Tunaomba hili liangaliwe kwa dhati na Serikali na tunakemea kwa nguvu zote suala hili, naomba itikadi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Rose Kamili ajiandae Mheshimiwa Katani.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha. Najikita kwenye maeneo matatu ambayo ni kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike wazi kwamba umuhimu wa sekta hizi za kilimo, mifugo na uvuvi ni kwamba zinaajiri watu wengi sana na pato la Taifa pia linapatikana kiasi cha asilimia 30.1. Kwa kuwa hii sekta inaajiri watu zaidi ya asilimia 66, Waziri wetu wa Fedha tunaomba utuambie vizuri hizi sekta umezitengea kiasi gani cha fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake imeonesha wazi kabisa kwamba kilimo umewapa asilimia 0.4, hivi kweli watu 66.6 ambao wanaajiriwa na sekta hii ya kilimo, mifugo na uvuvi, umewapa 0.4 wanawezaje kufanya kazi? Maana yake hata wewe hapo ulipo umeajiriwa na hii sekta kwa sababu unakula mchele, nyama, samaki na kila kitu, umeajiriwa na sekta hii. Sasa iweje utenge kiasi hicho cha fedha? Kwa nini uwadharau wanyonge na wafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa mifugo katika bajeti iliyopita umewapa *zero* kwenye masuala ya maendeleo leo umewatengea 0.1. Wataendelezaje jamii

hiyo yote ambayo ni asilimia 66.6 ambao ni Watanzania walioajiriwa na hizi sekta? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa uvuvi umewapa asilimia 0.06. Sasa Mheshimiwa Waziri mwenzako kwa nini asitembee na rula? Ataendeshaje hiyo sekta ya uvuvi ambayo inahitaji fedha za kutosha nawe umetenga kiasi hicho? Kwa kweli tunaomba utupe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa korosho wamelalamika ni kilimo nasi pia tunalalamika kwamba ni kwa nini hizi sekta umezionea kiasi hicho? Mheshimiwa mwenzangu dada yangu anasema tukimtaja Waziri Mkuu hapa hahusiki, Waziri Mkuu ndiyo Mwenyekiti naye atuambie alipokaa na Wizara zake hakuliona hilo la kutengewa hizo 0.06, 0.1 na 0.4? Ni kwa nini mtufanyie hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Wizara zinatakiwa kwa kweli ziweze kuajiri watu wengi. Hizi Wizara zingepata fedha za kutosha na kupewa kipaumbele ni wazi kabisa kwamba tungekuwa na asilimia 60 ya pato la Taifa, ukweli wa Mungu, kwa sababu wote tunatumia kilimo. Naomba nitoe mfano wa Hanang. Hanang tuna mashamba ya *NAFCO,* tuna *Basutu Plantation* halina mtu yeyote, ni shamba la Serikali. Je, mngeweza kuwekeza pale mkaweka viwanda vikubwa wangekuwa wameajiri watu wangapi wakasaga unga, wakakamua mafuta ya alizeti na ambao wangefanya kazi kwenye kiwanda cha ngozi na cha kuchakata nyama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli nyie mmekaa tu, mashamba ya Serikali yapo, mmeyabinafsisha wenyewe, basi muwekeze pale halafu unaipa mizigo halmashauri, unasema halmashauri waanze kujenga masoko, waanze kujenga sijui mabanda ya nini huku umeshachukua ushuru wao wafanye kitu gani? Tunaomba mtuambie kwenye suala la viwanda mmefanya nini? Watanzania ambao wanategemea kilimo mnawasaidiaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *Basutu Plantation* hutalipia hela yoyote ya kwamba tunataka kulipia viwanja

na lina eka 13,000. Kwa nini hujafikiri muda wote na una Msajili wa Hazina pale ofisini kwako, hajakueleza kwamba kuna shamba ambalo linahitaji viwanda pale? Mngekwenda kuwekeza na tuna uhakika Watanzania wote wangeajiriwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunalalamika hapa tuna vijana wanaomaliza shule 800,000 hawana ajira, je, ungefungua hivyo viwanda vikubwa si wangepata ajira wala wasingehangaika? Sasa hivi mnaanza kutupa kazi ngumu ya kuanza kugombana na nyie, tunagombana kwa kitu gani? Ninyi hapo mnaishi kwa kodi ya wananchi, sisi Wabunge tunaishi hapa Bungeni kwa kodi ya wananchi, sasa kama tunaishi na kodi ya wananchi hawa hawa wa asilimia 66.6 kwa nini mmewekeza 0.06, 0.4... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Katani.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki, dakika tano.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kupata nafasi kujiunga na wenzangu katika kuchangia hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimame na sheria. Sheria Na. 18 ya mwaka 2009 ya tasnia ya korosho, kifungu cha17 ndiyo ilitoa tamko rasmi la kutaka asilimia 65 ya mapato ya

*export levy* iende katika mikoa inayolima korosho. Bila kutaka kuzungumza lolote mikoa inayolima korosho Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, hao wengine baada ya kuona mafanikio wameingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nashauri busara itumike zaidi, ukitumia busara utaepusha migogoro. Migogoro hii inakuja na sababu nyingi zilitengenezwa sheria za hovyo ambazo ziliitenga Mikoa ya Lindi na Mtwara mpaka tunafikia katika maamuzi haya. Walitengeneza Sheria ya Madini, sungura wa mgodi au miradi ya *social* iende maeneo ya migodi tu, Lindi na Mtwara isiende. Wakaleta miradi ya TANAPA, kwa vile hatuko katika hifadhi hizo wakapeleka huko kwenye hifadhi na Lindi na Mtwara hatuombi chochote. Hatuna ruhusa ya kupata shule, hatuna ruhusa kupata maji na miradi yoyote ya maendeleo wanayoipata mikoa ya wenzetu sisi hatuna ruhusa kupata lakini tulinyamaza tukajua pengine kuna siku watatutambua Serikali, Serikali imeamua kunyamaza kimya. Wabunge wakaona ni haki yao watu wa Kusini ni wa kubakia wanalalamika, sisi hatulalamiki, tunatumia vigezo vya kisheria na sheria itambulike ili iwasaidie watu wa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati imekuja hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu niliuliza, umeletwa mradi mkubwa wa Selous ambao umeingiza mabilioni kwa kujenga barabara na maendeleo mengine. *Two third* ya *Selous* iko Lindi na Mtwara, mradi ule umepelekwa Ruaha wakati Ruaha kuna *TANAPA*, umepelekwa Udzungwa na Mikumi wakati Udzungwa na Mikumi kuna *TANAPA*. Hii yote ni fujo za makusudi na sheria za hovyo hovyo zinazowafanya watu wa Kusini wakate tamaa. Tufike mahali tujiulize, tutaendelea kuvumilia vitu kama hivi mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushauri wangu. Ushauri naotoa, miradi yote ya ustawi iliyoko katika migodi ivunjwe isaidie Tanzania nzima. Miradi ya *TANAPA* ya uhifadhi isaidie Tanzania nzima. Hii ni miradi ambayo inawanufaisha

wachache na wachache waliofaidika wameona ni haki zao za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge walitembea kwenda Liwale, inatia aibu, Mbunge ndiyo anaingia leo kutoka Liwale, tangu mvua zimenyesha alikuwa hawezi kwenda Liwale hakuna barabara. Unasema imeletwa pesa shilingi bilioni 600 kustawisha utalii Kusini, Kilwa haipo, Liwale haipo halafu unataka tuseme nini? Ni maumivu ya muda mrefu, watu wa Kusini tunaonekana kama watu ambao hatuna maendeleo, hatujitambui, kumbe kuna mikoa mingine imekuwa *boosted. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo tunaona mwendokasi wa treni kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, yale mafanikio lazima tuyapendelee yawe makubwa tunasema ahsante, Mji wa Dodoma unaendelea tunasema ahsante, lakini Lindi ni katika mikoa nane ya *Southern Province* kaiangalie Lindi ni sawasawa na Kibaigwa. Tumefanya makusudi kudhoofisha Mikoa ya Kusini isiendelee. Tulitegemea Mtwara katika miradi ya gesi ingefika mahali sasa hivi Mtwara imerudi tena *zero*. Lindi tumeleta mradi wa *LNG,* mikataba imesimama, hakuna *LNG*, watu wamechukuliwa ardhi zao, hakuna maendeleo ya *LNG*, ahadi na mipango ambayo haitekelezeki Kusini imezoeleka.Tufike mahali tujiulize, kuna nini Kusini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa nyuma walisema sisi tena hatuitaki Tanzania tunataka twende Tanganyika yetu. Hoja hii ililetwa ili Serikali ione watu Mikoa ya Lindi na Mtwara wana kilio cha muda mrefu. Ushauri naoutoa, naomba kwa busara zote hata kama mtataka kubadilisha sheria lakini hizi shilingi bilioni 201 zipelekwe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nianze moja kwa moja kwenye suala hili la korosho. Watu wa Mikoa ya Kusini kutokana na athari za kihistoria wamefikia mahali wamekuwa na unyonge *(inferiority complex). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitazama wanaoongoza Serikali naona watu wenye hekima na busara kubwa na nashangaa ni kwa nini mpaka sasa wameachia mjadala huu ukafika hapa. Ilikuwa itumike busara ndogo tu kuona ukweli wa jambo hili. Suala la *export levy* kwa korosho ni la kisheria na sheria inafahamika labda kama wanatokea watu wakasema kwamba sisi tunatafsiri vibaya sheria lakini haeleweki tatizo ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nishauri kwamba suala hili halina haja ya kutupeleka huko tunakotaka kwenda. Busara itumike, watu wa Kusini wapate pesa zao, mjadala uishe, lakini kama mnataka tuendelee hivi basi sisi suala la kupinga tumezoea toka enzi za Majimaji. Tutapinga na maandano aliyoyaitisha Mheshimiwa Bwege tutaandamana lakini kama mnataka haya yasitokee basi mutupe pesa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa, amefanya kazi kubwa kwenye tasnia ya korosho. Mafanikio tunayoyaona leo kwenye korosho kwa kiasi kikubwa ni usimamizi wake. Si korosho tu, leo kuna hoja ya ufuta, nilimuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusiana na suala la ufuta, akatoa maelekezo kwamba mikoa yote inayolima ufuta iingie katika mfumo wa stakabadhi ghalani au kukusanya na kuuza ufuta kwa njia ya mnada. Wakaitishwa Wakuu wote wa Mikoa inayolima ufuta kilichotokea mikoa mingine yote wakasema sisi hatutaki Lindi peke yake tumekubali. Mpaka sasa hivi navyozungumza bei ya ufuta imefikia Sh.2,815 na tayari kuna ufuta unatoka leo Dodoma kupelekwa Kilwa, nikupongeze sana Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hili suala la korosho linaloendelea dhuluma hii sisi hatuwezi kukubali. Wanachokisema watu wa Kusini ni kwamba, Kawawa aling'oa reli na Majaliwa anaua korosho, kwa hiyo ukae ukifahamu hilo. Kawawa aling'oa reli, Majaliwa anang'oa korosho, ujumbe umefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la Serikali za Mitaa. Najiuliza kwani Serikali ya CCM ina mpango gani na ustawi na uwepo wa Serikali za Mitaa? Mbona kuna kila dalili ya kutaka kuua Serikali za Mitaa? Kwa hali iliyopo sasa kama Serikali za Mitaa zinaondolewa mapato yake, kwa mfano, sisi watu wa Kilwa leo hii tayari tumepewa taarifa *service levy* ya gesi itachukuliwa na *TRA,* ambayo tulikuwa tunapata kati ya Sh.500,000,000 - Sh.700,000,000 kwa mwaka, ukituondolea hiyo tunabakiwa na nini? Kama Serikali haitakuwa na nidhamu ya mipango inayopangwa na Bunge lako Tukufu basi Serikali za Mitaa zinaenda kupotea. Kwa sababu tunakaa hapa tunapanga, lakini kinachotokea ni kwamba mipango tunayopanga haitekelezwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iwe na nidhamu ya mipango tunayoipanga. Kama wanaamua kutumia *Treasury Single Account* kwamba fedha zitachukuliwa kupelekwa Mfuko Mkuu basi wawe na nidhamu ya kuhakikisha kwamba pesa hizo zinarudi katika Halmashauri zetu kwa ustawi wa halmashauri. Kwa hali iliyopo sasa ni kana kwamba tupo katika ule wakati wa madaraka mikoani. Tulishapiga hatua sana, tulikwenda katika kuzirejesha Serikali za Mitaa lakini baadaye tumekwenda katika maboresho ya Serikali za Mitaa, Serikali lilitumia nguvu kubwa katika dhana ile *D by D* lakini sasa hivi ni kama tunarudishwa nyuma. Kwa hiyo, niombe sana kwamba Serikali iwe na nidhamu na mipango tunayopanga ili basi ustawi na uwepo wa Serikali za Mitaa uendelee kubaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho nizungumzie kuhusiana na suala zima la upandaji wa madaraja kwa

watumishi. Tunasema uchumi unakua, Mheshimiwa Dkt. Mpango nachokwambia ni kwamba tangu mwaka 2015 mpaka sasa hivi watumishi wengi na hususani walimu hawajapanda madaraja au kama walipanda basi kuna kundi limepanda na kundi lingine halijapanda. Watu walioanza kazi siku moja kuna mwingine amepanda daraja na mwingine hajapanda daraja. Naomba uliangalie sana suala hilo lakini pia uwaangalie watu ambao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Salehe (Alberto).

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nitakuwa na mambo mawili moja *just in passing* na lingine nitali-*pursue* kwa undani kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *in passing* ni kuunga mkono hoja ya Wabunge wa Kusini. Tunaamini kwamba wana haki na Serikali ina wajibu wa kuwarudishia pesa yao. Hilo tutawaunga mpaka dakika ya mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho nataka kukizungumzia kwa undani ni juu ya kile nachokiona cha kutokuwepo na mfungananisho wa kiuchumi baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kiasi ambacho uchumi wa nchi hizi mbili inaonekana waziwazi kwamba hazisomani lakini tuna-*disadvantage of Zanzibar.* Kwa muda wote huu tunaona kwamba upande mmoja ambao ni nchi kubwa, ina soko kubwa, ina watu wengi, haiko tayari kuifungulia Zanzibar soko na biashara kiasi ambacho Zanzibar ina-*suffer* kwa hali iliyoko hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo inasababishwa na mambo matatu. Mimi si mchumi lakini *it is not rocket science* kufikiri hivi ninavyofikiri. Nchi hii tunaambiwa ina *fiscal policy* na *monetary policy* moja *with slight changes* kwa Zanzibar. Pia tuna *one currency, one tax regime,* soko moja na *one*

*sovereign power.* Juu ya yote yanayofanyika utaona mambo mengi hayaendi sawa. Uchumi mkubwa hauusaidii uchumi mdogo, lakini pia soko kubwa halisaidii soko dogo, Zanzibar haifaidiki na kuwemo kwenye Muungano, ni sawasawa na pengine tungekuwepo kwingine kokote kule kwa hali iliyopo hivi sasa. Kama tungeweza kufananisha kwamba Tanzania Bara ni uaridi tunukie basi tunanuka vundo kuliko kunukia harufu nzuri, hatufaidiki lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni tatizo la kibajeti. Tukitengeneza bajeti ya Muungano ina athari kubwa kwa Zanzibar. Kuna athari za kikodi, mikopo, kiuwekezaji na kiurari. Kwa hali tulivyo sisi watu milioni moja na laki tano, lazima fedha yetu nyingi inakuja huku kununua vitu kwa hiyo *balance* ya fedha kule inakuwa ni ndogo, kwa hiyo, muda mwingi mzunguko wa fedha unakuwa mdogo Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna athari ya kibiashara na athari ya sisi Zanzibar tumekuwa dampu ya biashara ya Tanzania Bara. Siku moja, kama miaka mitatu nyuma, Waziri wa Biashara wa Zanzibar alikuwa Mazrui akawa anasema, kinyume na watu wanavyofikiri, Zanzibar ndiyo wanunuzi wakubwa wa mazao ya wakulima wa kutoka Bara. Kwa sababu ya mahitaji yetu, watu wengi wanakuja kununua bidhaa huku na zinakwenda kule, matokeo yake ni kwamba hatufaidiki. Kwa sababu pamoja na kufanya hivyo lakini bado kila mwaka Zanzibar haishirikishwi katika Bajeti Kuu ya Tanzania kwa maana ya uongozi wa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wawili hapa wamezungumza, jana alizungumza Mheshimiwa Saada na leo amezungumza Mheshimiwa Khadija Nassir, wanasema kwamba Zanzibar ushirikishwaji wake ni mdogo sana, kwa hivyo, hatufaidiki katika hili. Mimi nakwambieni kwamba itafika siku mtaona tabu na mtaona shida kuhusishwa na Zanzibar kwa sababu wakati huo sisi tutakuwa *so backward.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitatu nyuma Mheshimiwa Dkt. Shein aliwahi kusema katika mahojiano,

kila nikienda Tanzania Bara naona mambo yanabadilika tu, kwa maana ya kwamba kule hatufanani kabisa na huku. Itafika wakati kwamba sisi tutakuwa tuko nyuma sana na mtaona aibu kusema Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano kwa sababu ya kutuacha nyuma kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine baada ya bajeti na zile sera kuna suala la Serikali yenyewe ya Muungano. Kuna tatizo hapa, wengi tunaamini kwamba Serikali ya Muungano iliyopo sasa hivi ni Serikali ya Tanganyika inayoisaidia Serikali ya Mungano kwa kiasi kikubwa. Kwa sababu kwanza karibu asilimia 90 ya Wizara ni za Tanganyika, si Wizara za Muungano, zilizobakia tatu, nne ndizo za Muungano. Kwa hivyo basi *thinking* yake inaifikiria zaidi Tanganyika kuliko kuifikiria Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa si hivyo kwa nini basi Serikali hii ya Muungano inanyang'anyana mapato na *partner state* ya Zanzibar? Mbona Serikali ya Muungano haijawahi kuwekeza Zanzibar? Mbona Serikali ya Muungano haijawahi kutengeneza *stimulus package* yoyote ya kuisaidia Zanzibar? Mbona Serikali ya Muungano inashindwa, mwaka juzi nilisema hapa angalau tupelekeni mradi kielelezo mmoja Zanzibar ambao ungesaidia kuajiri maelfu ya watu Zanzibar na ingepunguza tatizo la ajira. Hamfikirii jambo hilo kwa sababu mnafikiria zaidi Tanganyika kuliko kuifikiria Zanzibar. Kwa hivyo, ndani ya akili yenu au ndani ya *thinking* yenu Zanzibar si sehemu ya Muungano ni sehemu ya kitu kingine kabisa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Naam.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri kuna *options* mbili. Moja, muiachie Zanzibar iendeshe uchumi wa visiwa kama Singapore na Mauritius na nyingine basi…

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga ajiandae Mheshimiwa Joseph Mhagama.

**MHE.GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba nichangie machache niliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi alisimama rafiki yangu Mheshimiwa Nassari na kulaumu kuwa vikao vya Chama *(party caucus)* ndiyo vinaua mijadala mingi ya Bunge. Mimi nataka nimwambie kuwa kwenye *party caucus* ndiko tunakohoji masuala ya msingi ya chama na Serikali, kule ndiko tunakopata majibu. Hata wao kwa kutokuwa na vikao vya chama mpaka leo hii wanashindwa kupata majibu wapi pesa za ruzuku zinapoelekea. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini kaa kwanza. Mheshimiwa Mlinga hebu jielekeze kwenye hoja ambayo ipo mbele yako.

**MHE. MHE.GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Hoja iliyopo hapa ni masuala ya bajeti, hakuna masuala ya vyama hapa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sasa nataka nijielekeze kwenye Kamali. Mimi ni moja ya Wabunge ambaye nawakilisha vijana wengi wa nchi hii ambaye nachukia kamali kwa sababu inadumaza akili za vijana wenzangu. Kwa sababu Serikali mmekomaa na kamali haya, endeleeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongee machache. Kamali zetu hizi uratibu wake kwenye *Gaming Board* kuna vitendo vya rushwa vilivyokithiri. Kwa nini nasema hivyo? Kuna kamali ambao leseni wanatozwa kodi asilimia 6 na wengine asilimia 30 na michezo inafanana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu, kwa nini linatokea hili na hawa watu wanaofanya hivi wanachukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ni mfanyabiashara wa Kariakoo, hili nataka niongee kwa watu wa *TRA.* Mwaka juzi nilipewa makisio ya kodi Sh.500,000, mwaka jana Sh.1,000,000, mwaka huu Sh.2,500,000. Ukiangalia katika hali ya kawaida kila mwaka unavyozidi kuendelea biashara inazidi kuwa ngumu lakini kiwango cha kodi kinakuwa kikubwa. Nataka hawa watu wa *TRA* hizi *statistics* wanazozitumia kutoza kodi ni za nchi gani kwa sababu kwa Tanzania hali inazidi kuwa ngumu na kodi inazidi kuwa kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee suala lingine kuhusu taasisi za umma. Juzi *TTCL* waliwasilisha maduhuli kwa Serikali ya shilingi bilioni 1.5. Tunajua taasisi zetu nyingi za umma zimewekeza katika taasisi za kibenki, *insurance* na nyinginezo. Nataka nikuhakikishie hakuna sehemu ambayo tunaibiwa fedha kama kwenye magawio ambayo taasisi zetu za umma zimewekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliongea rafiki yangu Mheshimiwa Jesca Kishoa, ni kweli, hata Mheshimiwa Rais aliongea wakati anafungua Tawi la Nyerere hapo NMB kuwa kila mwaka mapato yale ya Serikali lile gawio liko *constant* na benki ina-*declare* imepata faida zaidi lakini faida ambayo inapata Serikali ni ileile. Sasa michezo ambayo inafanyika ni kwamba wanatoka wakubwa wa Serikali wa yale mashirika wanaenda kukaa kwenye hoteli na watendaji wa zile sehemu ambazo wamewekeza hela katika zile taasisi binafsi wanakubaliana, kama faida imeingia shilingi milioni 100 wanasema sasa hapa tu-*declare loss,* wanatengeneza *loss fake* matokeo yake hela nyingi wanagawana wao na

mashirika ya umma wanapata pesa kidogo. Mheshimiwa Waziri tulishawahi kuongea hili na nimekupa taarifa, nami nakusanya *data* zangu siku nikizipata nakuja kuzimwaga Bungeni ni mashirika yapi ambayo yanaidanganya Serikali kuwa hayapati faida wakati yanapata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee suala lingine la samaki. Sasa hivi wananchi wetu wa Tanzania ambao ni walaji wakubwa wa samaki wamekumbwa na kizungumkuti. Kuna hali ya sintofahamu, watu hatuli samaki, Wizara wanakamata kila mtu ambaye anavua na anayekula samaki. Nataka nimwambie Waziri samaki wakiisha tutakula kuku kwa hiyo atuachie tufaidi samaki wetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni hali ya uchumi. Ukisikia Tanzania hali ya wananchi ni ngumu ndiyo unasikia uchumi umepanda. Tanzania ni nchi pekee ambayo kipimo cha uchumi ni wananchi kuwa na hali ngumu. Kama hali yenyewe ndiyo hivi hatuna haja ya kuupandisha uchumi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Rose Tweve, Mheshimiwa Moshi Kakoso na Mheshimiwa Hamida Abdallah wajiandae.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, naomba niipongeze Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuchukua jitihada za makusudi kabisa kuhakikisha tunatengeneza mazingira rafiki kwa wawekezaji ambao wanataka kuja kuwekeza hapa nchini. Mmeweka *incentive* za kutosha hasa kwa wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza kwenye viwanda vya dawa na ngozi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kwa Mheshimiwa Waziri ningependa twende mbali zaidi, tutengeneze haya mazingira mazuri kwa wawekezaji ambao wamewekeza

tayari na ambao wanataka kuja kuwekeza kwenye viwanda ambavyo vina-*process products* zote zinazotokana na maziwa. Mheshimiwa Waziri atakubakuliana nami kwamba sekta hii ya maziwa inagusa Watanzania wengi, tumesema *up to sixty to seventy percent* ya Watanzania wanajishughulisha na shughuli aidha za kilimo, uvuvi na ufugaji. Hata hao wakulima utakuja *majority* tayari wana ng'ombe ambao wanazalisha maziwa, ukija hata wafanyabiashara, hata humu Bungeni kuna wengine wana mashamba na ng'ombe ambao wanaweza kuleta maziwa. Vilevile hata ndugu zetu ambao wameajiriwa wana ng'ombe mmoja ama wiwili ambao wanaweza kuzalisha maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama nchi tuna uwezo wa kuzalisha takriban lita *2.4 billion* za maziwa. Ndiyo maana nimesema kama nchi tuchukue jitihada za makusudi kuhakikisha tunatengeneza mazingira rafiki. Kwa sababu tayari tuna *raw materials* ambayo itaweza kupelekwa kwenye hivi viwanda kuweza kuwa *processed* ili Watanzania waweze kunywa maziwa ambayo ni safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sasa si nzuri. Pamoja na kuwa tuna hizi lita za maziwa bilioni 2.4, tuna viwanda ambavyo vina *process* maziwa haya, *it's only 3%* ambayo inaweza kuwafikia hawa wawekezaji ambao wamewekeza kwenye hivi viwanda vya maziwa, hii 97% inaishia mtaani. Tatizo ni kwamba sekta hii si rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri turasimishe sekta hii. Tukirasimisha, moja, tutatengeneza miundombinu rafiki ambayo itamhakikishia soko hata huyu mwenye lita moja au mbili ambapo kutakuwa na *collection centers* za kutosha ili zimhakikishie *raw materials* huyu mwekezaji wa kiwanda. Pale mkoani kwetu Iringa tuna kiwanda kikubwa cha *ASAS*, tukitengeneza *collection centers* za kutosha zitamhakikishia hata huyu mtu mwenye lita moja au mbili atauza maziwa yake na kuweza kupata kipato cha kutunza familia yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mwitikio wa unywaji wa maziwa nchini mwetu uko chini sana. Hawa wenzetu wa *WHO* wanashauri kuwa *at least* binadamu anywe lita 200 kwa mwaka. Sasa sisi hapa kwetu bado tuko nyuma, unywaji wetu nadhani ni lita 47 kwa mwaka wakati Kenya ni lita 130. Kwa hiyo, inabidi twende mbali zaidi kuongeza kasi ya unywaji wa maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida hapa ni bei iko juu. Kwa sababu sasa hivi mlaji ndiye anabebeshwa hii *VAT* kulipa 18% . Wenzetu wa Kenya maziwa ni *zero VAT.* Nadhani mwaka 2013/2014 tuliweka *zero VAT* kwenye maziwa. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri tuweke *zero VAT* kwenye maziwa na hii itatusaidia hata ile *competition* kati ya Wakenya na sisi maziwa yanapokuja sokoni. Sasa hivi Wakenya maziwa yao hapa wanaleta kwa 2,800 lakini sisi maziwa yetu yakienda sokoni yanafika 3,500, kwa hiyo ime-*discourage* sana unywaji wetu wa maziwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Mheshimiwa Waziri utakapokuja kufanya *winding up* hapa naomba ulitolee ufafanuzi kuhusu wauzaji wa maziwa ya mtindi. Hawa watu wa *TRA* wamekuwa ni kero sana kwa hawa wauzaji maziwa hasa ya mtindi. Kwa sababu sheria inaonesha kwenye maziwa ya mtindi hakuna *any additive* ambazo zimewekwa kwenye haya maziwa, lakini wao wamawa-*force* hawa watu wanaosindika maziwa kuweza kulipa *VAT.* Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba atoe *clarification* ili kuwaweka hawa wenzetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nashukuru kwa kunipa nafasi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Hamida Abdallah, Mheshimiwa Katani, Mheshimiwa Ally Keissy, wote dakika tano tano.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa kutekeleza miradi mingi ya maendeleo ikiwemo miradi ya ujenzi ya barabara, miradi ya uchukuzi kwa maana ya ujenzi wa reli na ununuzi wa ndege na viwanja vya ndege. Pia ipo miradi mingine ambayo imetekelezwa ya Serikali hasa miradi ya afya na maji. Tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye ushauri kwa Serikali. Ni vyema sasa Serikali ikaelekeza mipango ya kutekeleza miradi ambayo itakuza uchumi kwa Taifa letu. Serikali ikiwekeza kwenye sekta ya kilimo ina nafasi kubwa sana ya kuzalisha walipa kodi wengi, kwani eneo hili lina watu wengi wanaoitegemea sekta ya kilimo. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali iwekeze mtaji mkubwa sana kwenye sekta ya kilimo ili iweze kuajiri Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye miradi ya sekta ya mawasiliano. Sekta ya mawasiliano ikisaidiwa vizuri na Serikali ina nafasi kubwa sana ya kutoa mchango mkubwa kwa Taifa kwani yapo mashirika ambayo yakiwezeshwa na Serikali yana nafasi kubwa sana ya kutoa mchango mkubwa sana wa Pato la Taifa. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali ielekeze nguvu kwenye maeneo hayo ili yaweze kuwasaidia Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni la uvuvi na ufugaji. Ni vyema sasa Serikali ikaangalia kwa umakini zaidi eneo hili na iweke mpango mkakati wa kukuza sekta ya uvuvi. Sekta ya uvuvi ina nafasi kubwa sana ya kutoa mchango kwa pato la Taifa. Ni vyema Serikali mkaangalia kwa makini zaidi, mkawaandaa wavuvi, hasa wadogo wadogo, lakini mkawa na *plan* ya kuwasaidia wavuvi wa uvuvi wa bahari kuu ambao unahitaji vitendea kazi. Wavuvi wakipatiwa vitendea kazi hivi wana nafasi kubwa sana ya kutoa mchango mkubwa sana wa pato la Taifa kwani sekta hiyo ina nafasi kubwa na haijatumika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ufugaji. Kwenye ufugaji ni lazima tuwe na mpango wa kuandaa viwanda vya usindikaji wa maziwa na ngozi ambavyo vitasaidia jamii ya wafugaji. Hata hivyo, ili tuweze kuwa na pato zuri ni vyema Serikali ikawekeza kusaidia jamii ya wafugaji, hasa kwa kuwatengenezea mazingira mazuri ambayo yatawafanya wafugaji hao wasiwe wa kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaishauri Serikali iwekeze kwenye reli hasa ile reli ya Mtwara – Liganga – Mchuchuma. Reli hii ina nafasi kubwa sana ya kukuza uchumi. Tukianza kuchimba chuma na makaa wa mawe ambayo yako kule kwa kiwango kikubwa kuna nafasi kubwa sana ya kubadilisha maisha ya Watanzania wote na kupata rasilimali kubwa ambazo wananchi watanufaika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii naizungumzia kwa upana na urefu kwa sababu ni reli ambayo itafungua maendeleo makubwa sana Ukanda wa Kusini lakini tutakuwa na nafasi ya kuweza kuchimba chuma ambacho kimsingi kitawasaidia Watanzania wote. Bei ya bidhaa za ujenzi kwa sasa ni kubwa sana lakini kama tutawekeza tukawa na viwanda vya chuma na mbolea, vitasaidia sana kutengeneza ajira hapa nchini na kuwafanya wananchi wote waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri eneo la bandari...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia, ahsante.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiomba Serikali iendelee na ujenzi wa bandari ile ya Bagamoyo ambayo ina nafasi kubwa sana ...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Umetumia dakika tano vizuri sana, hongera sana. Ume-cover maeneo zaidi ya nane. Tunaendelea na Mheshimiwa Hamida na Mheshimiwa Katani.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa sababu dakika nitakazoongea ni chache sana, naomba moja kwa moja niendee kwenye hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru sana Serikali kwa kupunguza tozo kwa wazalishaji wa chumvi. Kilio hiki tulileta kwa Serikali na Serikali imeweza kusikiliza, imeweza kupunguza tozo ambazo zilikuwa ni kero kwa wazalishaji wa chumvi, kwa hiyo nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze sana Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuweza kuchambua na kuishauri Serikali katika mambo mbalimbali ambayo wameona ni changamoto sana. Tunayo mifuko iliyoundwa kisheria. Tunao Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Maji, Mfuko wa Umeme Vijijini, Mfuko wa Maendeleo ya Reli na Mfuko huo wa Uendelezaji wa Zao la Korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imeweza kuchambua mifuko hii ambayo ipo kisheria na wameona kuna upungufu na changamoto mbalimbali na wameweza kuishauri Serikali. Cha kusikitisha ni kwa nini Serikali inapokusanya fedha hizi wanashindwa kurudisha katika mifuko hii, shida iko wapi? Nguvu ambayo wamepata wenzetu wa Kamati ya Bajeti wamesimamia sheria. Mimi nashindwa kumuelewa Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwa nini anaona taabu kurudisha fedha hizi kwenye mifuko hii? *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa sana ya maji Tanzania, pia tuna tatizo upande wa *REA.* Tumeona namna ambavyo umeme haujawafikia Watanzania wote vijijini na *REA* inakosa fedha. Mimi nashindwa kushangaa kwa nini inakosa fedha wakati sheria

ipo na tulishapitisha tozo mbalimbali kwa ajili ya mfuko huu wa *REA* na Mfuko wa Maji. Kwa hiyo, suala la tasnia ya korosho, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Mikoa hii ya Lindi na Mtwara wamezungumzia kwa mapana sana, nami niko nyuma yao nawaunga mkono asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ujenzi wa barabara. Tuna barabara inayotoka Ng'apa – Rutamba – Milola kuendelea mpaka Ruangwa. Nasikitika sana, wananchi wale wamepewa *notice* ya siku 14 wavunje nyumba zao wenyewe na asiyevunja atatozwa *fine.* Hivi nani anaweza kujenga nyumba kwa siku 14 akaweza kuhamia? Huku tunakokwenda si kwema kwa sababu hatuwatendei haki wananchi wetu na tunajua maeneo ya majiji, manispaa, halmashauri zingine lazima wananchi wajenge katika maeneo ambayo tayari yamepimwa. Cha kushangaza, Serikali haijawaandalia mazingira wananchi hawa sehemu gani wanaweza kuhamia kwenda kujenga nyumba ambazo wataweza kuhamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi, wananchi hawa hawajapata fidia. Hivi unavyomwambia ahame kwa siku 14, hujampa fidia, unategemea anaenda kujenga na nini? Kwa hiyo, wakati wa majumuisho napenda Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano atuambie wameandaa mazingira gani ya wananchi hawa kuhama na kwenda kujenga maeneo mengine na kupisha mradi huu wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia, malizia.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wananchi wa Likong'o hawajapata fidia zao kupisha eneo la mradi wa *LNG.* Hili tumelizungumzia kwa muda...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Katani ajiandae Mheshimiwa Keissy.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuweka sawa kidogo baadhi ya wachangiaji na kwa nini Mheshimiwa Dkt. Mpango mmeona ameleta sheria mpya ya kufanya *amendment* kwenye sheria hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, changia nitazame mimi, usiwanyooshee watu vidole, ukipenda ninyooshee mimi kidole.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Korosho Na.18 ya 2009 ukiisoma pamoja na Sheria ya Fedha Na.15 ya mwaka 2010, kifungu cha 17A(1), (2)(a),(b) na (3), nataka nisome ili iwe vizuri zaidi watu waweke kwenye rekodi na kwa nini imeletwa *amendment* na Mheshimiwa Dkt. Mpango. Ameleta baada ya kujua kwamba fedha tunazozisemea 65% zipo kisheria, ndiyo maana ameleta *amendment* hapa. Sasa wale wanaochangia nje ya sheria, wanaosema maneno haya ya kusema hizi fedha zisiende, wanasema hizi fedha ni za Mfuko Mkuu wakati hii ni sheria ambayo imetungwa na Bunge hili, wanapotosha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lazima liwe wazi kwamba wanawapotosha Watanzania kuonesha kwamba watu wa Kusini wanazitaka fedha za korosho kwa ajili ya maendeleo ya Kusini. Wenzangu wameshasema korosho hizi tunazozungumza wakati tunasoma jiografia miaka ya nyuma tulikuwa tunasema kilimo cha pamba Mwanza, kilimo cha korosho Mtwara, tukisema mpunga tunataja na maeneo mengine. Kwa hiyo, *historical background* inabeba korosho kwamba ni zao la Mtwara, Lindi na maeneo ya Kusini. Kwa hiyo, watu wa Kusini kuizungumzia korosho kwa uchungu wana kila sababu ya msingi kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudi kwenye rekodi ya uzalishaji wa korosho tunazozungumza. Msimu wa korosho 2011/2012 uzalishaji wa Taifa letu ni tani 158,000. Katika hizo tani 140,000 zinatoka Lindi na Mtwara maana yake ni tani 20,000 tu zinatoka mikoa mingine hiyo 15 inayobaki. Mwaka 2012/2013 tumezalisha tani 127,000 lakini tani 121,000 zinatoka Lindi na Mtwara maana yake tani 6,000 tu zinatoka kwenye mikoa 15 inayobaki, mikoa miwili imezalisha tani elfu ishirini na ngapi hizi. Msimu uliopita mwaka 2016/2017 tumezalisha tani 265,000, katika tani hizo Mtwara na Lindi tumezalisha tani 192,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Lindi na Mtwara korosho ndiyo siasa yao, ndiyo uchumi wao, ndiyo maendeleo yao. Anapotokea mtu kutaka kuchukua fedha za korosho ambazo ziko kisheria huyo mtu ni adui namba moja wa Mtwara na Lindi. Mheshimiwa Dkt. Mpango nikuambie tu, hizi fedha tusipozipata usikanyage Mtwara na Lindi kabisa kabisa, mimi nakuambia kabisa. Mtwara na Lindi zimekuwa sehemu ambazo zimeachwa nyuma, hata fedha za kisheria nazo unazichukua? Wewe ni Waziri wa ajabu ambaye sijawahi kumuona ambaye huna huruma na Watanzania. CCM mnasema mnawajali wanyonge, wanyonge gani kama fedha za wakulima wa korosho hampeleki? Wanyonge gani kama fedha za maji hampeleki? Ni wanyonge gani Serikali ya CCM mnasema mnawapenda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, jielekeze kwenye hoja.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Ni wanyonge wa aina gani? Watanzania wa wapi? Wanyonge wa Tanzania ni wakulima wanaolima kwa jembe la mkono, korosho hailimwi kwa trekta Dkt. Mpango, korosho inalimwa na jembe la mkono, nenda Mtwara na Lindi ukaangalie, nenda maeneo wanayolima korosho uangalie, unachukua fedha zao huna huruma? Umeitwa kikao cha bajeti zaidi ya mara nne, huji. Umechukua fedha za korosho, tunataka fedha za korosho Mtwara, tunataka fedha za korosho za Tanzania. *(Makofi)*

*(Mheshimiwa Mbunge alikuwa akiongea huku akilia)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapotosha umma, mnapotosha Watanzania kwa *interest* ya nani? Mmekuja Bungeni wote kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania, kusimamia maslahi ya Watanzania lakini Wabunge mnakuja mnashangilia, mnashangilia Watanzania kuonewa, mnashangilia Watanzania kwenye haki yao ya msingi ya kisheria wasipate fedha zao, watu mnakaa na *party caucus* kwa ajili gani? Mheshimiwa Dkt. Mpango nikuombe sana.

*(Mheshimiwa Mbunge alikuwa akiongea huku akilia)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napata shida, hawa Wabunge wanaotoka Jimbo la Ikulu ni matatizo makubwa kwa sababu hawapigiwi kura na wananchi. Jimbo lao liko Ikulu ndiyo maana tunapata shida hii. Angalia Wabunge waliochaguliwa na wananchi, wana huruma, wanapanga mipango yao ya maji, fedha haziendi, Mpango unakwamisha maendeleo ya nchi hii, Dkt. wa ajabu sana. Nikuombe sana mzee wangu, kama kiti kimekushinda, achia waje wengine watu wapate maendeleo yao kwa fedha zao. Mambo gani unayafanya Dkt. Mpango? *(Makofi)*

*(Mheshimiwa Mbunge alikuwa akiongea huku akilia)*

**MBUNGE FULANI:** Toa machozi!

**MHE. KATANI A. KATANI:** Tumezungumza tangu kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo, tukakuomba uje kwenye Kamati ya Bajeti mara tatu Mheshimiwa Dkt. Mpango unakimbia kuja. Fedha za korosho ziko wapi? *(Makofi)*

*(Mheshimiwa Mbunge alikuwa akiongea huku akilia)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Keissy ajiandae Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa mimi nampongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu, Ndugu Dotto na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumzia namna ya kutafuta pesa. Kusema kweli leo Marekani ni nchi tajiri sana inapiga marufuku vitu vya kutoka China na kuviwekea kodi kubwa. Sisi nchi yetu tunaagiza mchele kutoka nje wakati tuna mchele wa kutosha, tunaagiza nyama, samaki, maziwa na nywele za bandia ambazo hazistahili kuagizwa katika hichi. Ndiyo maana dola yetu inapanda kila kukicha. Tunaagiza *furniture* wakati tuna mbao za kutosha katika nchi yetu. Hivi vitu vya namna hii vipigwe marufuku. Leo Marekani inapiga marufuku vitu vya kutoka China na sisi tupige marufuku vitu kama hivi ili dola yetu ipande na vitu vyetu viweze kuuzika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia *own source* za halmashauri kunyang'anywa. Mimi nashangaa anasimama Mbunge kabisa anasema *TARURA* imenyang'anya *own source* ya halmashauri, *TARURA* wapi na wapi? Ni pesa ilikuwa inatoka Serikali Kuu inakwenda kwenye barabara, halmashauri wanazifanyia kazi kule, leo unasimama kabisa Mbunge na heshima zako unasema *TARURA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ufisadi nchi hii bado uko pale pale, nazungumza kwa ukweli kabisa, anasimama Mbunge au Diwani anatetea Serikali isifanye uhakiki kuhusu waliokuwa wanaga pembejeo. Juzi tu Diwani wangu kanipigia simu wa Kata ya Mtenga, kasema mzee wasilipwe kwa sababu hawakugawa mbolea kata nzima lakini wanaandika majina ya bandia ni lazima Serikali ihakiki upya, huu ugawaji wa mbolea siyo halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano tu Bodi ya Korosho wanayopigia kelele, kuna kampuni inaitwa HAMASI, nenda *BRELA* kaitafute imechakachua mbolea kule kwako imechukua mpaka shilingi milioni 800 mpaka leo ina hasara lakini wanaitetea. Nashangaa Wabunge wa Kusini hawaisemi hii kampuni, imepewa tenda ya magunia Nachingwea, imebadilisha jina, hii kampuni ni ya mafisadi. Leo wameagiza magunia Sh.2,800 wanauza gunia Sh.4,500, wamejipatia zaidi ya shilingi bilioni 3 kuwanyonya wakulima wakorosho lakini Wabunge hawasemei hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi wanajilipa dola 600 wakienda nje wakati hata Rais halipwi dola 600. Mikutano ya ndani wanajilipa Sh.500,000, mkutano mkubwa wanatumia mpaka shilingi bilioni 5, 6 hao wadau wa korosho lakini Wabunge hawasemi. Hii nchi lazima tuambizane ukweli. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Muda wetu mdogo hakuna taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anadanganya sasa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi zote nchi nzima zichunguzwe ni wabadhirifu wa hali ya juu. Bodi za zamani hizi baadhi ya Wabunge walikuwepo wanajilipa posho za ajabu ajabu. Bodi zote zichunguzwe na ikiwezekana wote waliojipangia posho za ajabu ajabu wapelekwe Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuhusu mbolea. Nimezungumza habari ya mbolea ya mijungu, Sumbawanga walipeleka ya shilingi milioni 320 haikuuzika. Ajabu Kiwanda cha Mijungu kikalipwa shilingi milioni 320 na mpaka leo mbolea iko Sumbawanga inaoza. Nchi hii tunakwenda wapi, tunajipeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu samaki, Ziwa Rukwa kuna mamba wa ajabu, kwa nini wasivune mamba wale wakapandikiza samaki kuliko kuhangaika kuagiza samaki nje. Tuna Ziwa Rukwa kubwa kabisa tupandikize samaki tupunguze mamba ambao wanamaliza samaki katika Ziwa Rukwa. Ukiingiza mkono unaliwa na mamba, tupunguze mamba tupandikize samaki, tutaondokana na tatizo la samaki katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuharakishe kujenga reli ya kati haraka iwezekanavyo tuokoe uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme, lazima umeme wa Rufiji utekelezwe, mikoa mitatu inatia hasara Serikali, Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma tunatumia mafuta ya *diesel* ili kuendesha *generator,* hata kiwanda hakiwezi kuendeshwa na sisi ifanyike haraka tuingizwe kwenye gridi ya Taifa. Tukikalia ma-*generator* kila siku yanaingiza hasara kwenye Shirika la *TANESCO*. Haraka ifanyike tupate umeme kutoka Mbeya kwenda Kigoma kupitia Rukwa na Katavi ili tuokoe pesa za Serikali maana ma-*generator* yanakula mafuta mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kitu kingine nashangaa sana Serikali, pale Panamawe tumekabidhiwa majengo yalikuwa ya wakandarasi thamani yake ni shilingi bilioni 1.6. Mkurugenzi wa *VETA* kutoka Mbeya amethibitisha majengo yanafaa kufanya Chuo cha *VETA* na tuna heka 50, wanataka tu shilingi milioni 500 … *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Keissy. Tunaendelea na Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Dkt. Chegeni na Mheshimiwa Mwamoto wajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikuombe Mheshimiwa Dkt. Mipango ukisikia hizi kelele za watu wachache uamini kwamba Watanzania walioko huko nje na hasa wananchi wa Mtwara na Lindi wanaakili na wanachuja mwishowe watakuja kujua ni nini ulichokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi, sheria siyo *glass*, kama ilitungwa sheria ambayo Serikali haioni kama ina manufaa kwa wananchi wa Mtwara na Lindi walima korosho ni lazima tuibadilishe. Wabunge wanaopiga kelele hizi, nataka niseme, hivi kama hizi pesa zingekuwa zimeibiwa, hazijulikani ziliko, mkaleta hiyo hoja humu ndani tungewaunga mkono. Inakuwaje Serikali imegundua watu wanafuja pesa na ni Wabunge, kwa nini msije kulalamikia *go-down* lililojengwa Mkurunga, Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa aligundua *go-down* la shilingi bilioni... *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sasa hivi, hebu kaeni chini, muda uliyobaki ni mdogo sana.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisimama na kuongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Kaeni chini, kaa chini. Mheshimiwa Katani kaa chini, kama unataka kulia nenda kalie nje. Mheshimiwa Selasini unasemaje, ni utaratibu au taarifa.

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utaratibu. Kanuni ya 64(1), hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anasema fedha za korosho zimeibiwa na baadhi ya Wabunge wamo. Kwa sababu hiyo naomba kiti chako kimuombe ataje hao Wabunge vinginevyo... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo Bunge zima litaingia katika kashfa.

**MWENYEKITI:** Nimekuelewa. Mheshimiwa Musukuma endelea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nilindie dakika zangu. Kaka yangu Mheshimiwa Selasini nakuheshimu sana na unafahamu, lakini nikwambie katika wasioogopa kusema ukweli Musukuma ni namba moja, hili suala tuna-*Finance Bill* keshokutwa.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Ongelea pamba.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa hayo majina hapa unayoyataka.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindike dakika zangu.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Wameingia mbwa humu ndani au?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, anatuita mbwa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wananchi wa Mtwara na Lindi watulie wakati Serikali inatengeneza sheria ambapo pesa zitarudi kwao moja kwa moja. Hawa ni wapiga *deal* wanataka pesa zirudi kwenye mfuko, wakatende matendo ambapo hawawasaidii watu wa Mtwara. Miaka 10 mnapewa hizo pesa mmewafanyia nini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mnapeleka makampuni yenu mnapiga...

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa upande huu, mimi sishindwi kutoa watu wote nje.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Kaa kimya. Nikisimama mimi huwezi kunijibu.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Yaani sisi ni mbwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, wewe Mheshimiwa Sophia kaa kimya.

Waheshimiwa mchangiaji anachangia yale anayoyajua.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Anatuita sisi mbwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ryoba sijakusemesha, hajaitwa mtu mbwa sijasikia mimi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MWENYEKITI:** Nasema sijasikia.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Amesema.

**MWENYEKITI:** Natoa *warning* ya mwisho, hii kupiga miluzi, kusema uuu, iwe mwisho sasa. Nitakwenda kwenye *Hansard* nitajiridhisha. Mheshimiwa Musukuma.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bunge lina Kanuni...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hebu subiri, Mheshimiwa Rashid Abdallah nimekuona, yeyote nitakayemtoa atatoka tu.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, yeyote nitakayemsema ndiyo huyo huyo. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bunge hili lina Kanuni ambazo zinatuelekeza kutumia kauli za kibunge, sasa ukisikia 'uuu, uuu' sijawahi kuona kwenye Kanuni, hizi ni dalili za watu kugeuka mbwa Bungeni. Kwa nini walie 'uuu' imeandikwa Kanuni gani, hiyo siyo lugha ya Kibunge.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Mbwa mwenyewe.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, jielekeze kwenye hoja ambayo iko mbele yako. Sidhani kama kuna umuhimu wa kuanzisha fujo ndani ya Bunge kwa hoja ambazo zishaeleweka na Serikali wana majibu sahihi.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nimalizie kwa kuwaomba wananchi wa Mtwara na Lindi watulie wakati Serikali ikiandaa utaratibu mzuri wa pesa zao...

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Wewe nani?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chegeni ajiandae Mheshimiwa Mwamoto.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Wewe changia *disco*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linaloendelea ndani ya ukumbi wa Bunge halifurahishi na halipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ni kwa sababu gani kuna tabia ya kutokutulia ambayo ni tabia inayotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na wewe kama Mwenyekiti unapotoa maelekezo ndani ya Bunge hili lakini Wabunge wameendelea kupuuza maelekezo yako. Naomba mwongozo wako inapotokea hali ya namna hii ni hatua gani zichukuliwe ili Bunge liendelee kuwa na heshima na utulivu wakati shughuli za Bunge zinapoendelea? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip,* hatua zitachukuliwa, subiria. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, unajua wakati mwingine ukiwa na busara nyingi unaonekana kama vile unayumbayumba siyo kama hatuwezi kuwatoa watu wote wanaofanya fujo, tunategemea ninyi ni watu wazima, mnajiheshimu na mnajua Kanuni za Bunge. Wala haina haja kila saa *Chief Whip* asimame au mimi nisimame...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Unaona, maana wengine mnawashwawashwa tu humu ndani. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa chini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sasa hivi hakuna utaratibu.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, mbona umemruhusu Mheshimiwa Jenista?

**MWENYEKITI:** Haya unasemaje, sema.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawasemea hawa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nazungumza na Mheshimiwa Selasini. MheshimiwaJesca, Mheshimiwa Haonga *last warning*. Unajua mara nyingi nakuwa *patient* sababu naleta ubinadamu tu, lakini naonekana na mimi nayumba kwenye kiti ambapo siyo jambo zuri. Ninyi bado Wabunge wadogo sana, ndiyo kwanza mna miaka miwili tu ndani ya Bunge hili. Mimi nazungumza na *Chief Whip* siyo ninyi. Mheshimiwa Bobali na Mheshimiwa Katani kama bado unataka kulia, kalie nje. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakuunga mkono kwamba Bunge hili ni Bunge la Kanuni na nawaomba wenzangu tuwe watulivu na tukisikilize kiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilichotaka kusema ni kwamba katika kuchangia Mheshimiwa Musukuma na hili namwomba *Chief Whip* wa upande wa CCM akishauri kiti chako vizuri. Kanuni ya 65(1) inasema isipokuwa kwa idhini ya Spika, Mbunge yeyote hataruhusiwa kusema zaidi ya mara moja juu ya hoja inayozungumzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Musukuma katika hoja hii alikwishachangia, sasa anachangia mara ya pili jambo linaloonyesha kwamba kuna mbinu ovu ambayo inatumika katika kuwapanga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante nitalifuatilia. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Chegeni ajiandae Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Kwanza napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Fedha. Nchi kama nchi tumetoka mbali tunapaswa twende tunakotaka kuelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii pamoja na changamoto zake na hasa katika kukusanya mapato, mapato yamekuwa yakipungua kwa mfano mwaka jana kwa asilimia 14, hii ni changamoto ya kimapato. Naomba tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha jitahidi kuongeza vyanzo vya mapato ambavyo vinatasaidia kuongeza fedha ili tuweze kupata bajeti ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili wala siyo tatizo, kwenye hotuba hajagusa sana suala la kilimo, amelitaja tu kwamba kuna kilimo lakini hajagusa popote pale. Kwa mfano, tunasema tuna Sera ya Uchumi wa Viwanda maana yake ni kwamba tunaongeza tija kwa wakulima, tunaongeza uchumi wa nchi hii, tunaongeza ajira kwa watu wetu na tunaongeza fedha nyingi za kutoka nje, lakini Mheshimiwa Waziri hajalizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masikitiko yangu ni kwamba leo hii mkulima wa pamba, leo kuna watu wa korosho, katani na tumbaku wanapiga kelele na watu wa pamba na sisi tunapiga kelele. Kwa sababu mkulima wa pamba badala ya kupata tija katika kuzalisha pamba anapata tatizo kubwa sana, naomba sana Mheshimiwa Waziri uliangalie suala hili. Sera ya *C to C* (*Cotton to Cloth)* haijatekelezwa. Tulisema kwamba tutahakikisha mkulima anapata bei nzuri, *ginneries* wanapata bei nzuri, viwanda vya nguo vinazalisha nguo zetu na tunavaa nguo zetu. Kwenye bajeti hii Mheshimiwa Waziri sijaona mkakati wowote tunatokaje hapa tulipo, sasa hii ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema tujitahidi kuwa na sera kwamba tununue bidhaa za ndani, tuzalishe bidhaa za ndani na tuongeze ushuru mkubwa kwa bidhaa kutoka nje. Kwa mfano, tuna viwanda vya nguo ambavyo vingi vimekufa lakini kwa kweli bila kuwa na jitihada za makusudi hatuwezi kuvifufua. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine tumekuwa tukisema kwamba tunaongeza ajira, ajira zipi? Wenye ajira nyingi ni wakulima, bila kuwasaidia wakulima hawa kupata bei nzuri waweze kuuza mazao yao vizuri, hatutaweza kuwasaidia wakulima na hata ajira hatuwezi kuzipata. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri hebu tekeleza hili. Nchi zingine kama Bangladesh unakuta viwanda kama vya nguo vina mpaka ruzuku ya umeme, ya kuzalisha nakadhalika lakini sisi hapa mzalishaji anapata gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la kuongeza bajeti yetu ya Serikali. Baadhi ya wajumbe wamechangia kuhusu mashirika na taasisi zetu, kwa kweli tunahitaji tuwe na kipaumbele kikubwa sana. Tunatoza sana kodi wananchi lakini kuna hela ambayo tumewekeza zaidi ya shilingi trilioni 48 kama mitaji kwenye taasisi na mashirika yetu haya. Mheshimiwa Waziri wa Fedha imarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina ili ifanye kazi vizuri, haya mashirika yatalipa pesa nyingi sana. Kwa sababu shirika kama Serikali ina hisa kule ina maana kuna *revenue stream* kubwa tu ambayo tunaipata pale, kuna gawio, kuna 15% ya *gross turn over* na *access capital* yote ni hela ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/2015 ni mashirika 24 tu yalilipa gawio kwa Serikali *out of* 91, ni aibu. Mwaka 2015/2016 mashirika 25 tu ambayo yalilipa shilingi bilioni 249.3. Mwaka jana ni mashirika 38 tu yamelipa shilingi bilioni 677 lakini tuna mtaji mkubwa sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha tumia *avenue* hii kuweza kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine kuna *issue* ambayo hamjaigusa, pesa nyingi ya maendeleo inayowekezwa kwenye mashirika haya haionekani kwenye bajeti kuu. Naomba tu-*integrate,* hata pesa ambayo taasisi zinawekeza ni sehemu ya fedha ya maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri hebu angalia vizuri Ofisi ya Msajili wa Hazina, mpatie nafasi. Baadhi ya nchi unakuta kuna Waziri... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waziri anayeshughulikia *public enterprises* ambaye yeye kukicha...

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwamoto, Serikali mjiandae.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, nitachangia dakika kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu. Kwa kweli mmefanya kazi kubwa, niwaombee tu kwamba hayo madongo mnayopigwa ni kawaida. Kwa sababu mpo kwenye fedha, siku zote mtu anayeshika fedha huwa anaonekana ni mbaya tu. Kwa hiyo, msiogope kuonekana wabaya kwa ajili ya kuokoa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, nipongeze bajeti ya mwaka huu nafikiri ni nzuri kuliko zote ambazo nilishawahi kuziona. Kama itatekelezwa ilivyo basi inakwenda kumkomboa mnyonge, hii ni bajeti ya wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nitoe ushauri tu. Kwa kuwa tumeshaamua kwenda kwenye nchi ya viwanda

tuhakikishe fedha ambazo zitapatikana tuwe na maji, umeme na mawasiliano ya uhakika na tuboreshe miundombinu yetu. Hapo ndipo sasa unaweza ukajenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekkiti, niipongeze pia Serikali kwa kutengeneza akaunti shirikishi. Nchi zote duniani zimekuwa zikitumia muundo wa akaunti shirikishi. Kwa mfano, kabla ya hapo kuna halmashauri zaidi ya 151 kila halmashauri ilikuwa na akaunti zaidi ya 10, kulikuwa na akaunti zaidi ya 1,510. Sasa leo tunakwenda kuwa na akaunti 151 na zinakwenda kwenye mfuko mmoja. Niwaondoe tu wasiwasi Wabunge wenzangu kwamba haya ndiyo mambo yako Afrika Mashariki na duniani kote, kwa hiyo, tunakwenda jinsi ambavyo tunatakiwa twende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna kitu kinaitwa kodi ya majengo. Kodi hii kama tukikusanya vizuri tunaweza kupata fedha ambayo inaweza ikasaidia kwenye uchumi wetu lakini jinsi tunakusanya sio sahihi. Ukienda nchi nyingine zilizoendelea hawakusanyi kama tunavyokusanya sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kingefanyika, kwa mfano, kwa mwaka unalipa Sh.36,000 ingeweza kugawanywa hiyo kwa 12 ukapata Sh.3,000. Hizo Sh.3,000 zingeweza kuwekwa kwenye kodi ya umeme. Kwa sababu sasa hivi kila mtu anaenda kuwa na umeme na atalipa, kwa hiyo, yule mtu hataumia kwa sababu atalipa Sh.3,000 kila mwezi. Kwa hiyo, unakuta umekusanya kwa uhakika na fedha inakwenda kwenye mzunguko bila kupoteza hata senti tano. Njia ambayo inatumika sasa hivi tunaenda kupoteza mapato mengi. Nimefanya hesabu hapa nikipata nafasi nitakaa na Waheshimiwa ili muone kiasi gani kinapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekwenda mbele zaidi hata kwenye viwanja tungeweza kukusanya kwa njia hiyo, lakini hata hospitali. Kwa mfano, leo mtu amepata ajali na hana bima ya afya, yuko hospitali anatibiwa, sasa kama yule mtu ana namba ya nyumba yake na bili ya umeme analipa, inaingizwa kwenye bili ile ya umeme anaweza akalipa bili ya

hospitali. Mkikaa vizuri wasomi wa uchumi mnaweza mkatengeneza utaratibu mzuri na watu wakalipa bila kuwa na kelele yoyote. Niombe tu kwamba nchi yetu lazima tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ni hili ambalo limetokea sasa hivi. Sisi Wabunge tuna mhimili wetu na tunaheshimika sana na jamii lakini mambo tunayoyafanya wanaoangalia tunazidi kujipunguzia heshima. Sasa hivi ukitembea huko Mbunge unaonekana ni mtu wa ajabu tu, mtu ambaye unaweza ukafanya kitu ambacho hata mtoto mdogo hawezi kufanya. Naunga mkono kabisa suala la kuzuia kuonyesha *Bunge Live* kwa sababu jambo hili kama wataona tunajionesha sisi tulivyo na tabia ya mtu inaonekana. Niombe tu Waheshimiwa Wabunge mmeaga kwenu, hapa tufanye kazi kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono suala hili la leo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo muhimu. Nawakumbusha tena shughuli ya Mtukufu Aghakan iko leo na itafanywa *immediately* baada ya Bunge kuahirishwa. Kwa hiyo, Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria kwenye shughuli hiyo katika viwanja vya Bunge ambavyo siku zote tunafanyia shughuli zetu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Tizeba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyojipanga ndani ya Serikali tunaomba aanze Mwanasheria Mkuu wa Serikali halafu tutaendelea na Mawaziri.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuanza kuwa mchangiaji upande wa Serikali. Kwa kuwa hii ni Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali naomba nijielekeze zaidi kwenye masuala ya kisheria na nitaelekeza hoja yangu kwenye hili suala la *export levy* kwa sababu limezua sintofahamu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, naomba nianze kwa kizirejea sheria mbalimbali ambazo zimekuwa zinahusika na suala la *export levy.* Nitajaribu kupita kwa harakaharaka ili tujue tulipo hapa tumetokea wapi katika sheria. Nizitaje harakaharaka, *Cashewnut Board of Tanzania Act* ya 1984, *Cashewnut Marketing Regulations* za 1996 na Maelekezo ya Serikali ya mwaka 1998. Halafu turejee kidogo kesi iliyofunguliwa na Mfuko wa Korosho ya mwaka 1999, kuna maamuzi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa. Kisha twende Waraka wa Baraza la Mawaziri Na.42 wa mwaka 2005, *Finance Act* ya 2006, *Cashewnut Industry Act* ya 2009, *Crops Laws (Miscellaneous Ammendments) Act* ya 2009, *MoU* ya Wadau wa Korosho ya tarehe 10/05/2010 na *Trust Fund* iliyotengenezwa baada ya *MoU* hiyo halafu *Finance Act* ya 2010 na mwisho nigusie changamoto za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa haraka kabisa nikianza na *Cashewnut Board of Tanzania Act of 1984.* Sheria hii ilikuwa na vifungu vya 6(1)(d), 7(1), (2) ambavyo vilianzisha *levy* na *levy* hii ilikuwa haibagui kati ya korosho zilizobaguliwa na ambazo hazijabanguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Cashewnut Marketing Reguations* za 1996 ambazo zilitengenezwa kupitia *GN. No.* 369 na zenyewe zilikuwa na *provisions* zinazogusa masuala ya *export levy.* Pia hazikutofautisha kati ya korosho iliyobanguliwa na ambayo haijabanguliwa na ilitoa *charge* ya 3% ya mauzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huohuo 1996, wadau mbalimbali wa korosho ndiyo walianzisha Mfuko wa kwanza wa Korosho. Mwaka 1998 baada ya kutokea ubadhirifu katika Mfuko huo wa Korosho, Serikali iliagiza kwamba ile Bodi ya Korosho isipeleke pesa kwenye mfuko huo. Kuanzia mwaka 1996, Bodi ya Korosho ilikuwa ikikusanya

yale makusanyo inapeleka kwenye mfuko huo. Mwaka 1998 Serikali ikatoa maelezo kwamba sasa Bodi isipeleke tena fedha kwenye mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Korosho haukuridhika na maelekezo hayo ya Serikali na ukafungua kesi Mahakama Kuu, ni kesi Na.204 ya mwaka 99. Uamuzi wa Mahakama Kuu ulikuwa ni nini katika shauri hilo? Ningetamani kusoma uamuzi huo wa Mahakama, muda hautoshi, lakini ni-*summarise* tu mambo makubwa ambayo Mahakama Kuu ilisema ni matatu. Kwanza, makusanyo yote yale ya 3% ni fedha za umma na siyo fedha za mfuko. Pili, Mahakama Kuu ikasema Bodi ile ya Korosho inakusanya fedha hizo kwa niaba ya Serikali. Tatu, Serikali ndiyo yenye mamlaka ya kuamua matumizi ya fedha hizo. Haya yako katika hukumu ya Mahakama Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mahakama Kuu kutoa uamuzi huo, Mfuko wa Korosho haukuridhika, ulikata rufaa Mahakama ya Rufaa. Mahakama ya Rufaa mwaka 2001 ilitoa hukumu yake na ikakubaliana na kusisitiza yote yaliyokuwa yameamuliwa na Mahakama Kuu. Huo ukabaki ndio msimamo kuhusiana na hiyo *export levy,* ni fedha ya umma, Bodi inakusanya kwa niaba ya Serikali, Serikali ndiyo yenye mamlaka ya kupanga matumizi ya fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005, Baraza la Mawaziri kupitia Waraka Na.42 wa Juni mwaka huo, lilitoa Waraka ambao ulikuwa unafuta mifuko ya mazao yote na ulikataza wakulima kutozwa tozo zote kwa ajili ya kuiendeleza mifuko hiyo. Pia ukasema Bodi mbalimbali za mazao zigharamiwe na Serikali ila kwamba ushirika uimarishwe. Waraka huu kimsingi ulifuta ule Mfuko wa kwanza wa Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende kwenye *Finance Act* ya 2006, kifungu cha 4 kiliongeza kifungu 10A katika ile sheria ya mwaka 84 niliyoitaja ikawa inaweka kitu kinaitwa *export levy* kwa korosho isiyobanguliwa na ikaweka thamani ya 10%. Sheria hiyo pia ilitaja mgawanyo, katika hiyo 10% ambayo ingetozwa basi 6.5% yake ingekwenda kwa

halmashauri zinazolima korosho na 3.5% ingeenda kwa Mfuko Mkuu wa Serikali *(Consolidated Fund). Finance Act* hii haiutaji Mfuko wa Korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende kwenye Mabadiliko ya Sheria ya Korosho ya 2009. Kupitia hii *Cashewnut Industry Act* ambayo ndiyo nimeona Wabunge wengi wanapochangia wanaanzia 2009, 2010 na kuendelea, lakini bila kurudi kwenye historia wakati mwingine kunaweza kutupatia shida na kujikanganya. Hii *Cashewnut Industry Act* ya 2009 iliifuta ile sheria ya 1984 lakini ikazibakiza zile Kanuni zilizotengenezwa chini ya sheria hiyo yaani zile Kanuni za mwaka 1996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi sheria hii mpya ya 2009 haikuanzisha wala kutaja mfuko wa korosho, ingawa kifungu cha 36 cha sheria hiyo kiliruhusu wadau wa korosho kuwa na ushirika, wanaweza kutengeneza ushirika wa wadau. Nieleze hapa kwa msimamo wa kisheria ushirika wa wadau sio mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huo huo 2009 ikatungwa hii sheria niliyoitaja *Crops Laws (Miscellaneous Ammendments) Act No.20.* Ilifuatana na ile nyingine ya *Cashewnut Industry* ambayo ni *Act No.18* ya *2009. Miscellaneous Ammendments* hii ilifuta vifungu vyote vya sheria za mazao ambazo zilikuwa zinawalazimisha wakulima kutozwa tozo mbalimbali kwa ajili ya kuhudumia bodi zao na ikasema bodi hizo zigharimiwe na Serikali. Kimsingi ilikuwa inafuata ule Waraka wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 sasa kukatengenezwa *Memorandum of Understanding* ya wadau wa korosho. Katika hiyo *Memorandum of Understanding* wadau hawa ndipo walipokubaliana kuanzisha Mfuko wa Korosho. Ukiisoma ile *MoU* inataja bayana vyanzo vya fedha itakayoingia kwenye mfuko huo. Niseme na itoshe kusema, kwa sababu ninazo *document* zote hapa, hata hiyo *MoU* haikutaja *export levy* kama chanzo chake kimojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 6 ya *Memorandum of Understanding* ndiyo inaanzisha *trust* yenyewe. Pia niseme hapa sasa mfuko ule umeanzishwa kama *trust* ukiwa na *trustees,* haujaanzishwa kwa Sheria ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka hapo tunakwenda *Finance Act,* tarehe yake ni 15/06/2010, ni mwezi mmoja hivi na kitu baada ya wadau wa korosho kuanzisha mfuko. Hii ndiyo nadhani inafanyiwa rejea mara kwa mara kwa sababu kifungu cha 17A kilichoongezwa kinataja *export levy* ya 15% na kinataja mgawanyo huo wa hiyo *export levy* kwamba 65% itakwenda kwenye *Cashewnuts Industry Trust Fund* na 35% itakwenda kwenye *Consolidated Fund (*Mfuko Mkuu wa Serikali). Pia, sheria hiyo ilimtaka Waziri atunge Kanuni kwa ajili ya kuiwezesha sheria ile kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nieleze changamoto za kisheria kwa sababu sheria hizi za korosho zimepita katika mchakato mwingi na nadhani katika mchakato huo pia kuna kujichanganya kidogo. Cha kwanza nikiseme msimamo wa Mahakama unabaki palepale na haujawa *challenged* kwamba makusanyo yote ya *export levy* ni fedha za umma na Serikali ndiyo yenye mamlaka ya kupanga matumizi ya fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, *Cashewnuts Industry Development Trust Fund* haijaanzishwa kwa sheria ya Bunge. Kwa hiyo, hata ilipotajwa katika *Finance Act* ya 2010, katika sheria tunasema ilikuwa ni *anticipatory* lakini kwa kweli ile sheria haikupaswa kufanya *reference* kwenye mfuko ambao sheria yake haijaletwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho *consequences* za haya yote ni nini? Serikali haiwezi kulipa fedha kwenye mfuko ambao haujaanzishwa kwa sheria iliyotungwa na Bunge. Naomba hapa nifanye rejea ya sheria nyingine, unajua shida ya sheria ni moja sheria zinaathiriana. Unaweza kusoma sheria moja ukafikiri umepata jibu na *position* lakini ukasahau kusoma sheria nyingine na nyingine na nyingine ambazo zinaiathiri hii. Nafikiri *Public Finance Act* ambayo inaongoza

masuala yote ya fedha za umma ilisahaulika. Hapa tunazungumzia mambo ya *special funds,* yaani kama hii *fund* ya korosho ni *special fund,* nini kilitakiwa kifanyike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kifungu cha 12(1) cha *Public Finance Act* ya 2001, kinasema:-

*"The Minister may by order published in the Gazette, establish special funds, who shall not form part of the Consolidated Fund."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni ni *Minister* gani? Ni *Minister of Finance.* Kwa hiyo, ni *Minister of Finance* ndiye alitakiwa kuanzisha ule mfuko ili ukubalike kisheria na pasiwe na mgongano na sheria nyingine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika mbili kwa sababu hii ndiyo sehemu muhimu kabisa. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Endelea kwa elimu unayoitoa, mimi ndiye ninayepanga muda, kaa chini wewe.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kifungu kidogo cha (2) cha Kifungu cha 12 kinasema:-

*"Any order made under subsection (1) shall-*

*(a) state the purposes for which the special funds is being established; and*

*(b) identify the Accounting Officer responsible for its operations."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na tatizo kwa sababu hii *fund...*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG,* hebu kaa kwanza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Anaongea uwongo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani, inaelekea una mpango wa kutaka kwenda nje na wenzio wakufuate. Mheshimiwa Katani nenda nje, askari toa nje huyo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio*

**MWENYEKITI:** Kama wengine mnataka kumfuata nendeni vilevile. *(Makofi)*

*(Hapa Mhe. Katani A. Katani alitoka nje ya Ukumbi wa Bunge)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walishangilia)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG,* endelea. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kifungu kidogo cha (2) kinasema, Waziri atakapotengeneza hiyo *order* ya kuanzisha hiyo *special fund* ni lazima kuileta Bungeni. Sasa hilo halikuwa limefanyika na kwa hiyo, hiyo *fund* haiwezi kuwa inatambulika kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba Waziri atatengeneza *regulations* kwa ajili ya kuelekeza uendeshaji wa ile *fund. Regulations* bado hazijatengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho pengine ambalo ni kubwa zaidi kuliko yote kabisa na nahitimisha hapa, twende sheria hiyo hiyo ya *Public Finance,* kifungu cha 13(2) kinasema:-

*"For the avoidance of doubt, the investment of such funds shall not constitute a withdrawal from the Consolidated Fund in terms of section 16 of this Act".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inamaanisha nini? Ni kwamba fedha zitakazoingia kwenye huu Mfuko wa Korosho hazipashwi kutoka kwenye *Consolidated Fund.* Nikirudi nyuma kidogo, sheria zilielekeza kwamba hii *export levy* ikusanywe na *TRA* na wakikusanya wanapeleka kwenye *Consolidated Fund*. Kwa hiyo, fedha iliyotoka kwenye *export levy* imeingia kwenye *Consolidated Fund*. Kifungu hiki nilichosoma cha 13(2) kinasema hakuna fedha itatoka kwenye *Consolidated Fund* kwenda kwenye *special funds*. Tukifika hapo ni kwamba Serikali imefungwa mikono na ikifanya kinyume na hapo imevunja sheria*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Tizeba ajiandae Mheshimiwa Prof. Mbarawa.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu. Nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu mambo mengi ambayo nilidhani nitahangaika kuyazungumza ameyatolea ufafanuzi mzuri sana. Kwa hiyo, nitazungumzia kipande kidogo

tu cha suala hili la korosho *in terms* wa upatikanaji wa viuatilifu. Kwa rekodi niliyonayo, nimesikia Wabunge wengi wanaotoka maeneo haya ya korosho wakipata wasiwasi kwamba labda mwaka huu zao litaanguka kwa sababu hatuna *sulphur* ya kutosha, hatuna dawa ya maji ya kutosha na kadhalika. Takwimu niliyonayo hadi jana tarehe 24 Juni, 2018, jumla ya tani 34,868 zilikuwa tayari zimeingiza nchini na zinaendelea kuzambazwa. Bado katika *order* tuliyonayo kupitia Bodi ya Korosho tani 24,000 imeagizwa na italeta nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, upatikanaji wa *sulphur* ni nzuri, wafanyabiashara peke yao wameingiza tani 26,000 na Bodi imekwishaingiza tani 8,000. Tumeitaka Bodi iingize *sulphur* kwa makusudi kwa sababu bei ya wafanyabiashara watauza kutegemeana na *demand* katika soko lakini Bodi ya Korosho imeingiza hizi *sulphur* ili iweze ku-*regulate* bei itakayo-*prevail* katika soko na hili jambo linatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tarehe 25 Juni, 2018 vituo 48 vinavyodhibitiwa na Bodi ya Korosho vinaendelea kuuza *sulphur*. Nitoe tu mfano pale *TANECU* iko tani 120 sasa ina wiki mbili na mifuko miwili tu ndiyo imenunulia mpaka leo ingawa inauzwa kwa bei ya chini kabisa katika soko. Kwa hiyo, hakuna *crisis* ya *sulphur*. Dawa ya maji imeingizwa paketi 320,000 hizi zote zipo watu wanaendelea kununua na kupulizia mikorosho yao. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hatutarajii zao la korosho kuanguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amezindua Programu ya Maendeleo ya Kilimo Awamu ya Pili. Katika programu hiyo, mazao yote hasa haya makubwa ya biashara yamewekewa mipango mahsusi na Serikali inayavalia njuga haya kuhakikisha yanakwenda vizuri. Hatutakubali kuona zao lolote katika mazao yote haya linakwenda chini kwa sababu zilizo ndani ya uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, leo nilisikia manung'unika kwamba labda vyuo vyetu vitakosa fedha kwa ajili ya utafiti na kadhalika. Chuo cha Utafiti cha Naliendele kwa mfano fedha tayari imekwishatengwa. Karibia shilingi bilioni 3 imetolewa na Hazina kwa ajili ya kuendeleza utafiti tukabiliane na tatizo la mnyauko ambalo kwa kweli hilo ndiyo tishio halisi la kuangusha zao la korosho na siyo upatikanaji wa kiuatilifu kinaitwa s*ulphur. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizo zitaenda kutumika kufanya *research* na sisi kama Wizara tulikwishatoa rai kwa wananchi kwamba kwa sababu kwa sasa hakuna nchi duniani iliyo na suluhisho la dawa yaani kwamba ipo dawa ama mbinu fulani inayofahamika nje na ukataji na uchomaji. Kwa hiyo, tuliwaelekeza wananchi maeneo yale ambako Mheshimiwa Naibu Waziri alikwenda kuzunguka kule akafika maeneo yote yale na kupeleka maelekezo mahsusi kwa uongozi na wananchi kwamba anayeona korosho inanyauka akate achome moto kulekule shambani ili korosho zile zenye ugongwa zisiambukize maeneo mengine. Kwa hiyo, fedha kwa ajili ya kusimamia zao hili inaendelea kutolewa na Serikali inazingatia vifungu hivyo vya sheria ambavyo amevisema hapa Mwanasheria Mkuu, hawawezi sasa wakafanya kinyume, Serikali iwe ya kwanza kuvunja sheria ambayo inapaswa kuisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la korosho nadhani halipo kihivyo, tuache Serikali ifanyie kazi mazao yote kwa stahili inayofanana. Tusingependa kuona kwamba kuna zao linakwenda hivi na zao lingine linakwenda vile, tunaonekana kama vile hatuko *consistent* au hatujui tunachotaka kufanya. Sisi tunajua tunachotaka kufanya, Waheshimiwa Wabunge niombe sana, hebu tuiache Serikali tutafanya kazi vizuri na korosho itaendelea kuwa vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine nililolisikia humu ndani la pamba kwamba mwongozo uliotolewa wa kuuza pamba unaleta tabu kwa wafanyabiashara. Yako mambo matatu ambayo ni lazima pia niyaseme hapa na leo nipeleke maelekezo mahsusi kwa

wanaohusika. Mwongozo ule ulisema usafirishaji uwe wa mchana tu, hili jambo siyo sawa. Saa 12.00 jioni kwa Mikoa ya Magharibi bado jua liko juu. Sasa ukiwazuia watu kusafirisha pamba saa 12.00 jioni unafanya ufanyaji wa biashara uwe mgumu zaidi. Wataingia *extra cost* wakati wangeweza kusafiri kilomita 5 mpaka 20 hizo na kupeleka ile pamba kwenye *ginnery*. Kwa hiyo, kama Mkurugenzi wa Bodi yuko hapa ananisikia hilo jambo marufuku, waacheni wasafirishe, *after all risk* ni ya kwake huyo anayesafirisha pamba siyo kwetu ya kwenu nyie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili la ujazo wa gari. Mwenye gari hawezi kuweka pamba ambayo itakwenda kugusa nyaya za umeme. Mita 3.5 ambazo *SUMATRA* wanaweka hizo zikizidi sasa ndiyo kweli wale polisi wanamkamata bila hata ninyi kuweka hayo maelekezo mliyoyaweka. Kwa hivyo na lenyewe naomba liachwe hilo, watu wasafirishe pamba akikutana na waya atajua mwenye kwamba akishusha hiyo pamba hawezi kuendelea kusafirisha pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni watu wetu wa ushirika ambao wameaminiwa na wafanyabiashara, pesa zimepelekwa kwao halafu wananchi wanapokwenda kuuza pamba waanzishwa Kiswahili kwamba unajua hela haipo, ukitaka *cash* tukulipe Sh.800 au tukulipe Sh.900. Hili jambo tunalifanyia kazi na naomba Wabunge niwaahidi kwamba tutakayemkamata huyo tutashughulika naye kweli kweli, tutamweka kwenye kundi la wahujumu uchumi, tutamfunga. Hatuwezi kukubali wananchi waibiwe waziwazi namna hiyo. Kwa hivyo, wale wote wanaofanya huo mchezo hasa Mkoa wa Mara, Wilaya ya Bunda viongozi mnaoshughulika na hili jambo naamini mtanisikia lifanyieni kazi mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mfumo mpya tulioui-*introduce* wa kuzuia uuzaji wa kahawa nje ya nchi moja kwa moja. Hili jambo ushirika uliokuwa ukijifanya unanunua kahawa kutoka kwa wakulima au wanachama wake tumesema ushirika hauwezi kununua

kahawa yake yenyewe kwa sababu ushirika ni wa wale wanachama walioko ndani ya ushirika. Kwa hivyo, wanakusanya kahawa kwa niaba ya wanachama wao wana-*process* wanapeleka mnadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambako kulikuwa na utaratibu wa kupeana *advance,* fedha kidogo ya ku-*process* hiyo kahawa ili ipelekwe mnadani ikishauzwa waje wakagawiwe pesa kutokana na mauzo waliyopata mnadani. Yako maeneo mfano Karagwe, Bukoba (Muleba), ushirika unakwenda unakushanya kahawa ya watu hela wamekwishapata benki, uhakika huo tunao halafu wanachukua kahawa bila kuwapa *advance* wakulima wanachama wake, hili jambo na lenyewe likome. Bei haijatajwa, narudia tena, hakuna katika *cooperative* yoyote ya kahawa ambako wanaruhusiwa kutaja bei kwa sababu bei itafahamika mnadani. Hicho wanachokitoa ni *advance payment* kwa makubaliano yao. Ushauri wetu ulikuwa kwamba wasitoe fedha nyingi halafu wakaenda kutengeneza mahesabu huko yasiyokuwa halali wakaja kuwaambia wakulima sasa hakuna cha kupata tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, zile *templates* za *cost* walizokuwa wametengeneza zote zilifutwa, tume-*engage* Bodi ya Kahawa na wadau wengine waende wakashughulikie kuona gharama halisi za uchakataji wa kahawa ili hicho ndicho kiwe kigezo kwa vyama vyote kutegemeana na eneo walililopo. Siyo kwamba katika wilaya moja vyama viko viwili wengine wanasema gharama ya uchakataji 1,800 wengine wanasema gharama ya uchakataji 900, tofauti haiwezi kuwa kubwa ya namna hiyo. Kwa hiyo, hili nalo tunataka tu-*harmonize* ili wananchi wapate haki yao kutengemeana na jasho lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, wako wakulima waliolima kahawa kwa mkataba. Hili la kupeleka mnadani moja kwa moja linaweza likakwaza huo uhusiano uliokuwepo. Hawa naelekeza wote waliokuwa kwenye makubaliano ya namna hii waende Bodi ya Kahawa wakaeleze *case by case,* hatutatoa *blanket statement*

kwamba sasa waendelee kufanya namna hii. Waende kwenye Bodi ya Kahawa waeleze *case by case,* ile itakayoonekana ina *merit* tutaifanyia kazi na ruhusa zitatolewa. Wengine hatutakubali, bado tutawataka waende mnadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nilitaka nizungumze niliarifu tu Bunge lako Tukufu, kwamba hii Programu ya Kilimo tuliozindua hivi tarehe 4 Juni, 2018 tunategemea tunaleta semina kwa Wabunge wote ili tuliweke Bunge na Serikali kwenye uelewa mmoja. Kamati yetu ya Bunge ya kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji tumekwishawapitisha kwenye mpango huu lakini tunaamini kwamba tukiwapitisha na Wabunge wote hata haya maneno ya mbegu za mafuta ya michikichi na kadhalika yote yatapata maelezo mazuri wakati wa semina hii. Semina hii tutaifanya kabla ya Bunge hili halijaahirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nakushukuru kwa wakati wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Prof. Mbarawa atafuatiwa na Mheshimiwa Mwijage.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rRehema kutujalia kukutana hapa tukiwa na afya njema. Pili, napenda kipekee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kuwasilisha vizuri bajeti ya Serikali na ina mambo makubwa ambayo tutakiyatekeleza naamini yataleta maendeleo makubwa kwa nchi yetu. Tatu, kabla sijaendelea naomba nitangaze rasmi kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja za aina mbili, hoja ya kwanza ilijikita sana kwenye sekta ya uchukuzi na hoja ya pili ilijikita kwenye sekta ya ujenzi. Hoja ya sekta ya uchukuzi ambapo na wewe ulichangia ilikuwa ni kuhusu Shirika la Ndege la Air Tanzania. Kwa mfano, ulisema kwa

nini Serikali tusinunue ndege aina ya Bombardier *Q400 new generation* ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda huko kwanza naomba nieleze tu Serikali yetu ya Awamu ya Tano imejipanga kuhakikisha kwamba tunakuza sekta ya usafiri wa anga. Sekta ya usafiri wa anga ni muhimu sana hasa katika kukuza sekta ya utalii. Kama tunavyojua, sekta ya utalii inachangia sana uchumi wa nchi yetu, ajira, pesa za kigeni na mambo mengine ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sekta ya anga inachangia sana kwenye mambo ya biashara na ukuzaji kwenye sekta ya viwanda. Serikali yetu tumejipanga kwa dhati kuhakikisha kwamba sasa tunakuza sekta ya usafiri wa anga. Kwa mfano mpaka kufika Machi, 2018 abiria waliopitia usafiri wa anga walikuwa takriban milioni 4.95 na tunategemea kwamba idadi hii ya abiria itaweza kuongezeka siku baada ya siku kutokana na hivi sasa tunavyoboresha Shirika la Ndege la Air Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Shirika la Ndege la Air Tanzania mpaka sasa hivi tumeshaanza kununua ndege saba, ndege tatu za Bombandier Q400 ambayo tunaita *new generation* zimewasili nchini na zinafanya kazi; ndege mbili *Boeing* 787 tumeagiza, moja tunatengea kuingia wakati wowote hapa nchini, ndege ya pili ya *Boeing* tunatengemea itakuja mwakani; na ndege mbili za *CA series* kila moja nyenye uwezo wa kuchukua abiria 132 tunategemea kufika mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege tuanzozinunua za Bombardier Q400 ni hizo ndege unazosema za *new generation* ambapo ndiyo ndege za kisasa za Bombardier za Q400. Naomba niwatoe wasiwasi Watanzania kila tunachokifanya tunaendana na teknolojia ya kisasa.Tuna wataalam wazuri ambao wana uwezo mzuri wa kuchagua ndege za kisasa ambazo zinakwenda na mazingira ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti hii iliyoisha juzi yetu sisi tumetenga takriban shilingi bilioni 495.6 kwa ajili ya kununua ndege mbili. Ndege ya kwanza tumeshatoa *order* ambayo ni hiyo Boeing 787 yenye uwezo wa kuchukua abiria 262 na ndege ya pili tunasema itakuja Bombardier Q400 *new generation* ambayo hii tutaifanya tofauti kidogo, tutapunguza abiria ili tuweze kuongeza mizigo zaidi kwa sababu tumeona *route* yetu ya kutoka Dar es Salaam kwenda Comoro inahitaji ndege yenye *space* kubwa kwa ajili ya mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua watu wengi wa Comoro wanategemea sana mizigo yao na bidhaa zao kutoka Dar es Salaam. Ndege hii ya Q400 tutaweza kuifanya iwe na abiria kati ya 50 mpaka 60 lakini sehemu kwa ajili ya mizigo iwe kubwa zaidi ili iweze kutoa huduma nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Shirika la Ndege la Air Tanzania linafanya kazi vizuri, sote hapa tumekuwa mashahidi, tunafaidi safari za Air Tanzania kutoka hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam. Sasa hivi tunafanya siku nne kwa wiki lakini hivi karibuni tutafanya siku tano kwa wiki, halafu tutafanya siku saba kwa wiki. Mwakani tutakuwa *route* mbili kwa siku kuonyesha kweli mji wetu wa Dodoma ni Mji Mkuu na sisi Waheshimiwa tunaoishi hapa pamoja na wananchi wengine wanapata faida hii ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijenga Shirika la Ndege lazima liendane na viwanja vya ndege. Serikali yetu tumejipanga kujenga viwanja vya ndege katika mikoa yote ya Tanzania ili kuhakikisha kwamba shirika letu la ndege sasa lilnakwenda kila mkoa hapa Tanzania. Kwenye bajeti iliyopita tumeweka takriban shilingi bilioni 215 pesa za Serikali kwa ajili ya uboreshaji wa viwanja vya ndege. Kazi inafanyika ambapo sasa hivi tunajenga jengo la abiria pale Dar es Salaam ambalo litagharimu takriban shilingi bilioni 560 ambayo tunaamini mapema mwakani jengo hilo litamalizika. Hatukuishia hapo tu, tunakwenda Mtwara kuhakikisha kule nako tunaanza kukuza utalii wa Mtwara ambapo tunatanua

uwanja wa ndege wetu ule kutoka ulipo sasa hivi mpaka kufikia kilomita 2.8 kwa gharama ya shilingi bilioni 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya kazi hiyo Shinyanga, Sumbawanga, Songea, Musoma na maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Nia ni kuhakikisha kwamba nchi yetu sasa inakuwa nchi ambayo Watanzania wengi pamoja na wageni wengi wanaokuja, wanatumia usafiri wa anga ili kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa ni kuhusu Bandari ya Bagamoyo. Bandari ya Bagamoyo ni muhimu sana kwenye uchumi wa nchi yetu. Bandari hii inajengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu ya Tanzania, *Reserve Fund* ya Oman pamoja na Kampuni ya Kichina ambayo inaitwa *China Merchant Port Holdings*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unategemewa utagharimu takribani Dola za Kimarekani bilioni 10.2. Utajengwa kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza, itahusisha uchimbaji wa lango la kuingilia kwenye bandari ile. Sehemu ya pili ya awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa gati yenye urefu kwa kilometa moja ambayo ni sawa na mita 1,000, pia itahusisha ujenzi wa kujenga *logistic park* na mwisho itahusisha ujenzi wa kujenga jiji la viwanda. Awamu ya pili ya gati ile, itahusisha ujenzi wa gati yenye urefu wa mita 700 na awamu ya tatu itahusisha ujenzi wa gati ya urefu wa kilometa 1.6 au mita 1,600. Mazungumzo yanaendelea vizuri. Hivi tunavyoongea leo, ujumbe wa kutoka China umekuja kuzungumza na timu yetu ya hapa Tanzania ili mazungumzo yaweze kukamilika na ujenzi uanze mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine zilizohusiana na sekta ya ujenzi. Kwanza Mheshimiwa Mtulia, Mbunge wa Kinondoni alitaka kufahamu Serikali imejipangaje kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Katika kupunguza msongamano kwenye Jiji la Dar es Saalam, kuna miradi mbalimbali inaendelea, kwa mfano, sasa hivi tunajenga *Flyover* pale *TAZARA* ambayo tunategemea Septemba, 2018 tutaifungua rasmi. Mradi ule umegharimu

takribani shilingi za Kitanzania bilioni 99. Pia tunajenga *interchange* ya Ubungo ambayo yenyewe itagharimu takribani shilingi za Kitanzania bilioni 177 ambapo kazi inaenda vizuri. Hatukuishia hapo tu, pia tunaendelea na ujenzi wa gati la *Surrender* ambapo kazi inaendelea vizuri na tunategemea hivi karibuni tutaweka jiwe la msingi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna mradi mkubwa *BRT* ambapo tumeanza *phase* ya I, II, III, mpaka ya IV. Yote hayo tunayafanya ili kuhakikisha kwamba tunaondoa msongamano kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa tumejenga barabara za pete kwenye Jiji la Dar es Salaam ambapo kwenye bajeti hii tuliyosoma juzi tumeweka takribani shilingi bilioni 20.5. Yote hayoa tunafanya ili wananchi wa Dar es Salaam au wageni wanaotembea Dar es Salaam waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kujenga uchumi wetu kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ndege niliyokwambia Q400 *new generation* inabeba abiria 96, ndiyo ndege mpya zinazotoka. Hizi ndiyo nimejengea hoja mimi, kwa hiyo, nendeni kwenye vitabu vyenu zitazameni, kama zinafaa zitapunguza gharama.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwijage ajiandae Mheshimiwa Kalemani.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia bajeti ya Serikali na nianze kwa kuunga mkono hoja. Kipekee nimpongeze Waziri wa Fedha na nimpongeze Naibu wake Mheshimiwa mama Kachwamba na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbali nisije nikasahau, kwa idhini yako naomba nichukue fursa hii kukualika wewe na Wenyeviti wenzako na Waheshimiwa Wabunge katika Maonesho ya 42 ya Saba Saba. Jambo la kipekee litakalofanyika, kwa ruhusa niliyopewa na Mkuu wangu wa kazi Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitaanza zoezi la kuuza matrekta 2,400 na nyie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuna utaratibu tufanya kusudi kuusambaza matrekta kwenye maeneo yetu. Matrekta hayo yanaitwa Nguvu kwa *Kipolish* na hiyo kampuni ilikuwa ikifanya kazi na *Massey Ferguson,* ni matrekta mazuri kwa mazingira ya Tanzania na yamehakikiwa na *CAMARTEC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango kidogo nikijaribu kujibu hoja za Wabunge. Tunajenga uchumi wa Taifa imara na ulio shindani. Tunataka kujenga uchumi ambao watu wake watakuwa na hali nzuri ya maisha. Tunataka nchi ya amani, utulivu na mshikamano lakini tunalenga nchi ya watu walioelimika. Imebidi niseme hili kwa sababu mwenye Ilani juzi aliniambia Mwijage hulisemi vizuri, kwa hiyo, tunataka kujenga *strong and competitive economy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili ujenge *strong and competitive economy* ambayo ina watu wenye amani lazima ujenge uchumi jumuishi ambao unajengwa na uchumi wa viwanda. Uchumi wa viwanda unataka kujibu swali tete ambalo limekuwa linaulizwa hapa kwamba mnasema uchumi unakuwa mbona hali za watu hazikui? Ni kwa sababu gani? Tulisema dhima ya Mpango wa II wa Miaka Mitano, ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Ili wewe uweze kupata chochote mfukoni lazima ushiriki kwenye mnyororo ule wa

uchumi wa viwanda, ushiriki kwenye kilimo, uvuvi na viwanda, mimi mtu wa viwanda nakua katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hilo, nijaribu kuwaeleza Wabunge ambao najua mnajua au wengine niwajulishe ni kwamba tunao mkakati mama unaoitwa Mkakati wa Fungamanisho la Maendeleo ya Viwanda. Chini ya mkakati huo kuna mkakati aliosema ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Chegeni, *Cotton to Clothing.* Tuna mkakati wa mbegu za mafuta na mtazisikia *tariff* zilivyokuja, tunaonyeshwa fursa kusudi uende ukalime kwa trekta utakalopewa uzalishe alizeti, tukazichakate hapa soko mmefungiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mkakati wa viwanda vya madawa. Katika kundi la viwanda lenye bidhaa tunazozitumia sana tumebaki na *item* mbili, tumebaki na viwanda vya madawa na vya mafuta ya kula na nina imani kwa mwaka huu tunavyokwenda tutafanya vizuri. Kuna sekta ya ngozi, nikushukuru Mheshimiwa Waziri, umewasikia wadau, tumeweka programu maalum namna ya kuwachochea hawa watu wa sekta ya ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapozungumza hii mikakati pesa zinatoka wapi, ndiyo linakuja lile suala tata la *the role of the private sector.* Tunapigana kujenga *private sector* ya Tanzania, hii mikakati itatengenezwa na *private sector.* Serikali tutaweka mazingira mazuri ya kuwekeza, *private sector* i-*pump in* pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Prof. Maghembe alizungumza anataka kupata *private sec*tor ya Kitanzania. Kama unataka kupata *private sector* Tanzania, ndipo unapokwenda kwenye ile dhana ya kiwanda kidogo sana, kiwanda kidogo, kiwanda cha kati, yaani utengeneze ile kitu kinaitwa *Business Graduation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linatupeleka kwenye suala la mazingira ya uwekezaji. Nashukuru Wabunge wengi wamezungumzia suala hili. Mheshimiwa Jitu Soni

amezungumzia suala la *Blue Print* na iko tayari, imepitishwa na chombo kinachohusika. Kuna mapendekezo na tumesharekebisha, tutaizindua. *Blue Print* ni kitu kimoja, utekelezaji unahusu suala tata lingine la kubadilisha mtazamo, *the change of mindset.* Waheshimiwa Wabunge mmelizungumza sana, unakutana na mtu, anakusimamisha, anaanza kupima gunia, eti gunia lako lina uzito gani, gunia ni la kwako, mnagombania uzito, hiyo ni *mindset.* Kwa hiyo, *Blue Print* iko tayari tutaizindua na tutakuwa na mkakati maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie miradi ya kimkakati. Nimshukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ameelezea suala l Bagamoyo. Bagamoyo inakuja, siwezi kuongeza zaidi Profesa amelizungumza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaelezee kuhusu kiwanda cha mbolea ambacho kimezungumzwa sana hapa. Mwenyekiti aliyeshikilia suala la kiwanda cha mbolea ni mimi, wawekezaji wapo, tunajadiliana. Tusifichane hapa, hakuna mtu ambaye angependa kiwanda kile kisiwekezwe Tanzania, tunakipenda kwa faida ambazo zinajulikana. Nina imani tutafuatilia maelekezo mliyotupa, hata na ile Kamati ya Gesi, maelekezo mliyotupa tutayafuatilia kusudi kiwanda cha mbolea kianze kwa *formular* nzuri ya *win-win*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipo Kiwanda cha Matairi cha Arusha. Kiwanda cha Matairi cha Arusha suala lililoko mezani ni kumtafuta mtu atakayekiendesha. Serikali hatuwezi kuingiza pesa kwenye Kiwanda cha Matairi Arusha lakini kiwanda kipo, *government* itakuwa na sehemu yake halafu tutakuwa na *operator.* Kwa sababu sisi faida tuliyo nayo ni ya soko na kitakapokuwa kimeanza tutakilinda kama tunavyolinda viwanda vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, kuna Mchuchuma na Liganga. Serikali imejasiria na wataalamu wako kazini, Mchuchuma na Liganga kila mtu anaona faida yake. Mbali na yale watu wanayoyaona, Mchuchuma na Liganga ikianza, faida za Mchuchuma na Liganga watu

hawazisemi. Mchuchuma na Liganga ikianza ina fursa kubwa ya kuajiri watu kiasi ambacho huwezi kukieleza. Kama tulivyoelekezwa tutahakikisha Mchuchuma na Liganga inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko dhana ya kulinda viwanda ambayo imezungumzwa. Taasisi zenu za *TBS* na *Fair Competition* zitaendelea kufanya kazi. Wakati nachangia bajeti hii, nina ombi moja, njia mojawapo ya kulinda viwanda ni kuvipatia soko. Tuendelee kuhimizana katika ile *shopping basket* yako jitahidi na wewe unaponunua, ununue bidhaa ya Tanzania. Ukinunua bidhaa ya Tanzania utakuwa umesaidia viwanda vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwepo suala la viwanda vilivyobinafsishwa vikafa. Maelekezo ninayoelezwa kwenye Ilani cha Chama cha Mapinduzi, Wizara yangu napaswa kuhakikisha viwanda vyote vilivyopo bila kujali mwenye navyo vinafanya kazi. Pili, ni kuhakikisha viwanda vilivyokufa, vinafanya kazi. Tatu, ni kushawishi viwanda vizaliwe, yaani viwanda vipya vijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vipya vimeanzishwa sasa hili la kuhakikisha vilivyokufa vinafanya kazi siliepuki. Nachotaka kuwaomba Waheshimiwa Wabunge hatuwezi kusimama, hayo ndiyo majukumu matatu, naweza kuwa nafanya vizuri sana kwenye A, B sifanyi vizuri. Viwanda vilivyokufa ambavyo havifanyi kazi napenda niwahikikishie kwamba *we are doing well,* viwanda 18 vimeshaingia kwenye maboresho. Nikushukuru Mheshimiwa Waziri umemleta *Treasury Registrar* kijana na ni mtalaam wa hesabu, tutashirikiana kuhakikisha viwanda vile ambavyo havitii, ameniambia ameshatoa *notice* na ukishapewa *notice* maana yake kinachofuta unakieleza, utakitambua. Huyu *Treasury Registrar* aliyekuja lengo ni kusimamia mahesabu, kuhakikisha kila kiwanda ambacho sisi tuna hisa zozote kinaleta gawio. Ndiyo maelekezo maalum aliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue fursa hii kuwaeleza na kumshukuru mwekezaji wa Kiwanda cha Ilulu,

Nachingwea, amekirudisha kiwanda yeye mwenyewe. Tumekaa chini tukamweleza namna ya kuwekeza, akakiri kwamba ngoma hii yeye haiwezi, amerudisha kiwanda. Tutakifanyia tathmini na kuchagua nani tumkabidhi kwenye *competitive way* ambaye haitaleta matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vivutio vya uwekezaji. Tunaendelea kushughulikia suala la vivutio na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mmechoka, Bunge lijalo tutawaletea Muswada mchana bila uchovu, tuweze kuangalia ile *Investment Act versus Finance Act* kusudi tuweze kujua wapi tunakwama. Hakuna mtu ambaye ana nia ya kukwamisha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia, malizia.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye anataka kukwamisha shughuli yoyote lakini hakuna mtu ambaye yuko tayari kufanya biashara ya tupatupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, naomba kuchukua fursa hii tena kuunga mkono bajeti ya Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kalemani ajiandae Mheshimwa Jafo na tutamalizia na Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naunga mkono kwa sababu kwa

kweli bajeti hii inatupeleka ambako uchumi wetu unalenga kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo makubwa manne, jambo la kwanza ni uzalishaji wa umeme hapa nchini. Nitumie nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kusema hali ya umeme nchini inaendelea kuimarika pamoja na changamoto za hapa na pale. Tunakubali ziko changamoto za miundombinu lakini kwa uhalisia hali inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 tulikuwa na jumla ya *megawatt* 1,336 na mwaka 2016 tulikuwa na jumla ya *megawatt* 1,472 na tangu Aprili, 2018 tumefikisha *megawatt* 1,517. Hii ni hatua nzuri baada ya miradi mbalimbali kuendelea kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja ya matumizi ya uzalishaji wa umeme mchanganyiko. Naungana na Waheshimiwa Wabunge kwamba lazima tuzingatie vyanzo vya kuzalisha umeme ambavyo kwa kweli vinapunguza gharama kwa shirika letu. Tulipoanza mwaka 2012/2013 tulikuwa tunatumia asilimia 5 tu ya gesi asilia tuliyonayo lakini hivi sasa matumizi yanaendelea kupanda kadri ya uzalishaji wa umeme kutumia rasilimali ya gesi unavyoongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa tumeshazidi asilimia 15 ya matumizi ya gesi kwenye kuzalisha umeme. Sasa tunatekeleza Mradi wa Kinyerezi II, tunayo matarajio makubwa kuanza kutekeleza Mradi wa Kinyerezi III mwakani na miaka miwili ijayo, hivyo matumizi ya gesi yataendelea kupanda zaidi. Mipango ya Serikali ifikapo mwaka 2020 - 2022 *megawatt* ambazo zitakuwa zimezalishwa na nishati ya gesi asilia, itakuwa imefika 2,870. Sasa hayo ni matumizi makubwa sana ya rasilimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matumizi ya gesi hayaishii kwenye kuzalisha umeme. Nimekuwa nikisema mara nyingi na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi. Viko viwanda vya kuzalisha mbolea na viwanda vya chuma vitahitaji gesi asilia. Kwa hiyo, matumizi ya gesi yataendelea kama

kawaida. Si kweli kwamba kuanza kuzalisha umeme kwa vyanzo vingine sasa tunaacha kutumia gesi. Matumizi ya gesi Waheshimiwa Wabunge yataendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazalisha umeme kwa vyanzo nafuu. Tunapozalisha umeme kwa kutumia nishati ya maji kusema ukweli gharama yake ni ya chini ukilinganisha na rasilimali nyingine. Leo ukitaka kuzalisha *kilowatt hour* moja kutoka kwenye nishati ya maji utatumia Sh.36 tu wakati kama unataka kuzalisha kwa upande wa gesi na vyanzo vingine ni zaidi ya Sh.147. Kwa hiyo, ni vizuri tukaangalia hili pamoja na kutumia vyanzo vingine. Niipongeze sana Serikali kwa kuamua kuanza kutekeleza mradi mkubwa wa Rufiji wa kuzalisha *megawatt* 2,100 kuanzia mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Kenya kwa nchi za Afrika Mashariki ndiyo wanaoongoza kwa kuwa na umeme mwingi, wana jumla ya *megawatt* 2,003. Sisi tutakapomaliza mradi huu tutakuwa tumewazidi Kenya mara mbili. Nchi nyingine kama Uganda wana *megawatt* 900, kwa hiyo, wako chini yetu na nyingine ziko chini ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge mlipopitisha kwamba mradi huu uendelee kujengwa. Ni matumaini yetu Serikali tutausimamia ili kusudi tuendelee kupata nishati ya kutosha. Hapo ndipo tutajenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozalisha umeme wa gesi na maji hatuishii hapo, tunahitaji kutekeleza miradi sambamba ya kuzalisha umeme mchanganyiko. Mwaka huu wa Fedha tunaanza kutekeleza Mradi wa Umeme wa Nguvu ya Jua wa *megawatt* 150 pale Ibadakuli, Shinyanga. Hii ni nishati nzuri mchanganyiko na ya gharamana nafuu. Kadhalika tutaanza kuzalisha umeme *megawatt* 100 pale Kisaki, Singida pamoja na Utaho kilometa 100 kutoka hapa. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba nishati hii mchanganyiko itatupeleka kwenye kujenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo ujenzi wa miundombinu wa kusafirisha umeme. Tuna changamoto kubwa kwa upande wa wakandarasi wetu lakini kama Serikali tumejipanga vizuri. Desemba mwaka huu wa fedha tunaanza kutekeleza mradi mkubwa wa kusafirisha umeme wa kutoka Iringa kwenda Sumbawanga kupita Tunduma, tunaupeleka Mpanda, Kigoma hadi Nyakanazi umbali wa kilometa 1,432. Huu ni umeme mkubwa wa kilovoti 400. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mikoa ya Sumbawanga, Katavi na Kigoma hivi sasa ina changamoto kubwa ya umeme. Kwa hiyo, kama Serikali tumejipanga mradi huu lazima tuutekeleze ili ukanda huu nao uweze kupata nishati ya kutosha kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Malagarasi. Mwaka huu wa fedha tutaanza kujenga mradi huu kwa ajili ya kupata *megawatt* 45. Mradi wa Malagarasi ni mkombozi sana kwa Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake. Hivi sasa mahitaji makubwa kwa wananchi wa Kigoma ni *megawatt* 11.2 lakini tutakapopata *megawatt* 45 tutaweza kuusafirisha umeme huo umbali wa kilometa 57 kutoka Malagarasi Igamba III kuupeleka mpaka Kidahwe Kigoma kupitia Kazuramimba, Kidea, Mazungwe, Mlenge hadi Karenge. Kwa hiyo, wananchi wa Kigoma ni matumaini yetu kwamba mara baada ya mradi kukamilika basi nishati hiyo wananchi wa Kigoma watapata nishati ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuunganisha miundombinu ya Makambako Songea. Hivi sasa maeneo ya Makambako, Ludewa, Songea, Mbinga pamoja na Madaba wanatumia umeme wa mashine za *generator*. Nishukuru sana Serikali pamoja na Waheshimiwa Wabunge, mradi huu unakamilika tarehe 20 Septemba, 2018. Kwa hiyo, ni matumaini yetu wilaya nilizotaja zitaacha sasa kutumia nishati ya mafuta mazito ambayo ni gharama kubwa sana kwa shirika letu. Nnitumie nafasi hii kusema kwamba miundombinu ikiimarika maeneo ya mikoa niliyotaja ujenzi wa viwanda

utakuwa ni mwepesi zaidi na kufikia lengo letu la kujenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi na Kigoma *REA III*, kweli kabisa hatujaanza lakini leo asubuhi nilitoa taarifa hapa kwamba kesho kutwa Jumatano mkandarasi anaripoti rasmi katika Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa *REA III*. Mwishoni mwa mwezi tunampeleka mkandarasi Mkoa wa Katavi na kwa Mheshimiwa wa Kavuu kule Majimoto na maeneo mengine ya Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini uko mradi wa *LNG*. Mradi huu ni mkubwa sana na ni kati ya mradi ambayo kwa kweli Afrika Mashariki hatujawahi kuwa nao. Ni kweli wenzetu wa Msumbiji wanautekeleza lakini tuko hatua moja. Hivi sasa hatua inayofanyika tunao wakandarasi watano wajenzi na kila mmoja yuko *dedicated* kutekeleza mradi huu. Kinachofanyika sasa ni kila mtu kufukuzia awe kiongozi wa kuujenga mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Serikali tunakaa nao na kujadiliana ili mradi huu uanze kutekelezwa kama tulivyopanga. Tarehe 11 Julai, 2018 wakandarasi watakutana na Serikali kuanza mustakabali wa kuanza kutekeleza mradi huu kwa *speed* kubwa. Ni matarajio yetu mwaka 2022 ujenzi utakuwa umeshaanza rasmi kwa sababu ni mradi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya *REA*, Waheshimiwa Wabunge kwanza niwapongeze sana, tumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye vijiji vya miradi ya *REA* kwa nchi nzima. Maeneo mengi yalirukwa lakini Waheshimiwa Wabunge mmetupa ushirikiano wa kutosha na sisi kama Serikali tumezingatia sana maoni na ushauri wenu. Badala ya kutekeleza vijiji 3,559 sasa tunakwenda kutelekeza vijiji 5,100 na kubaki na vijiji 2,272. Kwa hiyo, ni matarajio yetu mradi huu utakapokamilika viwanda vitakuwa vimesogea sana vijijini badala ya kukaa mijini peke yake. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwaalika Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Madiwani, waainishe maeneo ya ujenzi wa viwanda huko

vijijini kwa sababu sasa umeme unakwenda vijijini ili tutimize azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda kuanzia vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na mradi muhimu sana wa bomba la mafuta. Mradi huu wa kusafirisha mafuta kutoka Uganda ni mkubwa sana. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge mwaka jana mlipitisha hoja hii na tukaendelea kutekeleza. Hivi sasa tunakamilisha taratibu za kuanza ujenzi, maeneo ya kujenga matenki matano kule Chongoleani, Tanga umeshakamilika na Novemba tunaanza ujenzi rasmi. Mwezi unakuja tunakutana na wenzetu wa Uganda ili ujenzi uweze kuendelea. Miradi yote ikikamilika, ni matarajio yetu Tanzania itakuwa ni nchi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitumie nafasi hii kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda sana kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango, dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashantu pamoja na timu yote ya Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa sana waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyokuwa tukimfuatilia Mheshimiwa Dkt. Mpango akiwakilisha bajeti yake hapa, kwa kweli kwa kiwango kikubwa sana, watu wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Bajeti hii kwa kiwango kikubwa sana inaonekana inaenda kujibu changamoto mbalimbali za Watanzania katika suala zima la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mbalimbali ambayo watu wamechangia, kwamba jinsi gani bajeti hii itajielekeza katika miradi ya kijamii na hasa afya, elimu na miundombinu ya barabara. Kubwa zaidi mimi kwa upande wangu, kwanza napenda kuishukuru sana Wizara ya Fedha, katika Wizara ambayo kwa kweli mwaka huu imetendewa haki vya kutosha na wananchi kwa ujumla wake ni Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwezeshwa ujenzi wa miundombinu ya sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunafahamu tokea uhuru mpaka 2015 tulikuwa na vituo vya afya vya Serikali 515 peke yake lakini vilivyokuwa na uwezo wa kutoa huduma ya upasuaji vilikuwa vituo vya afya 115 pekee. Tumeshuhudia ndani ya kipindi kifupi vituo vya afya 208 vimejengwa na kuboreshwa ni jambo kubwa na la kihistoria sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo haitoshi, Serikali hii katika mipango tunaona kwamba si muda mrefu sana tutaenda katika programu ya vituo vingine 97 litakuwa lingine kubwa la kihistoria. Bajeti yetu inayokuja ya mwaka 2018/2019 ambayo hapa tunajua wazi kwamba lazima tumuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Mpango ili hizi fedha zipatikane, vilevile inaenda kutekeleza jambo lingine la kihistoria. Tokea tulipopata uhuru nchi yetu mpaka mwaka 2015 au mpaka hivi sasa hospitali za Wilaya za Serikali ni 77 lakini bajeti hii ambayo Mheshimiwa Dkt. Mpango amewasilisha hapa lengo kubwa ni kukusanya fedha kwenda kujenga hospitali mpya za wilaya 67 kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la kihistoria halijawahi kutokea. Imani yangu ni kwamba kwa sababu Wabunge tunafahamu wazi wananchi wetu wana shida kubwa ya sekta ya afya kesho tutashuhudia wote hapa tukisema agenda ya ndiyo kwa sababu lazima hospitali za wilaya na vituo vya afya vikajengwe ambalo ni jambo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hiyo haitoshi, katika mwaka wa fedha unaokuja kutakuwa na ukarabati mkubwa na ujenzi wa miundombinu katika sekta ya elimu. Zaidi ya shilingi bilioni 185 zitatumika katika kuimarisha shule kongwe na miundombinu mbalimbali. Tuna kila sababu ya kwenda kuwasaidia Watanzania ndiyo maana mwaka huu tumeshuhudia watoto waliofaulu wameongezeka zaidi. Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba Wabunge wote katika mpango wa bajeti ambao umeletwa hapa ambao ndani yake una kurekebisha shule za msingi, shule za sekondari, shule kongwe, sote tutaungana kwa pamoja kuhakikisha bajeti hii tunaiunga mkono lakini mwisho wa siku twende tukashirikiane kwa pamoja katika kuhakikisha kodi inakusanywa ili kupata mapato mengi ili Serikali yetu iweze kutimiza malengo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala zima la asilimia 10 ambayo ni asilimia 5 kwa vijana na asilimia 5 kwa akina mama. Ni kweli jambo hili kipindi kilichopita changamoto yake imekuwa kubwa zaidi. Kwa kauli mbiu ileile na agenda nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Mpango, bajeti mwaka huu imekuja na suluhisho kwa baadhi ya halmashauri ambazo zilikuwa hazitoi pesa za vijana na akina mama. Bajeti ya mwaka huu imeeleza wazi na katika *Finance Bill* sheria inatungwa mahsusi kwamba sasa tunaenda kusimamia asilimia 5 kwa vijana na asilimia 5 kwa akina mama mwisho wa siku watu hawa waende kujenga uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie ndugu zangu kama kulikuwa na tabia ambapo halmashauri ama Wakurugenzi wetu walikuwa wakifanya *business as usually* na hawataki kupekeleka hizi fedha bajeti ya mwaka huu inaenda kujibu tatizo hilo ambalo muda mrefu sana tulikuwa tukilipigia kelele. Kwa agenda hiyo, sioni sababu Mbunge yeyote aseme hapana kwamba yeye ina maana hahitaji vijana wake na akina mama waweze kupata fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi bajeti hii imejielekeza katika uchumi wa viwanda na kaka yangu Mheshimiwa Mwijage amezungumza wazi. Bajeti hii inaonekana jinsi itakavyoenda kulinda viwanda vya ndani lakini hata ukiangalia ongezeko la kodi kwa viwanda vya ndani limebaki pale pale kwa asilimia kubwa. Hii maana yake ni kwamba tunaenda kujibu ajenda ya uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Mwijage, tulipozindua ajenda ya pamoja ya viwanda 100 kila mkoa na ilipofika tarehe 20 Aprili, 2018 tulipata rekodi ya mikoa yote vimejengwa viwanda vidogo 1,280 sawa na utekelezaji wa lengo asilimia 49.4. Haya ni mafanikio makubwa, ndani ya *quarter* moja ya mwaka viwanda 1,280 *equivalent* na asilimia 49.4 vimejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajenda ya bajeti hii ya Mheshimiwa Dkt. Mpango inaenda sasa kurasimisha vizuri viwanda hivi baada ya kujengwa jinsi gani vitalindwa. Naomba niwasihisi Wabunge wenzangu, katika bajeti hii tuna jambo kubwa la kufanya kama wabunge. Jambo la kwanza, tumeona jinsi suala la mafuta limezungumziwa, leo hii ukienda Singida, Dodoma hapa na Kigoma tunaweza tukajielekeza katika suala zima la mafuta. Kama tunaongeza tozo katika mafuta haya, Wabunge na wadau wote kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha tuna-*capture* vizuri *gap* ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye nini? Tuna *short term* kwa kulima mazao ya muda mfupi. Jambo la kwanza tukubaliane na bajeti hii, nami naiunga mkono asilimia zote 100 lakini niwasihi Wabunge wenzangu wote ikiwezekana sasa tuwe vinara katika suala zima la uwekezaji katika mazao ya alizeti, karanga na mazao mengine. Tuzalishe alizeti ambapo ndani ya miezi sita tutakuwa tumevuna, tuzalishe karanga na tuhamasishe ujenzi wa viwanda vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Taasisi yetu ya *SIDO* inazalisha mashine mahsusi kwa ajili ya ukamuaji wa mafuta

ya alizeti. Inawezekana katika upandishaji wa kodi hii itakuwa fursa kubwa sana kujenga uchumi imara kwa wananchi wadogo wadogo na sisi Wabunge tukiwa vinara wa kwanza katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii kwa upande wangu nasema ni bajeti ambayo imejali sana maslahi ya nchi hii. Mheshimiwa Dkt. Mpango naomba nikwambie yale mawazo mengine yote yachukue kwa ajili ya kuyafanyia kazi. Niseme kwamba bajeti ni nzuri na *input*s za Wabunge hawa zichukue kwani lengo kubwa si kukosoa isipokuwa ni kuijenga vizuri. Naamini Serikali mwaka huu imekuja na bajeti yenye kuwajali wananchi wetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelipigia kelele ni suala zima la miundombinu ya barabara. Ndugu zangu miundombinu ya barabara ina changamoto kubwa sana lakini katika hilo hilo vilevile barabara hizi haziwezi kupatikana bila watu kulipa kodi. Bahati nzuri katika mpango wa bajeti ya mwaka huu tumejielekeza na mimi hapa nilizungumza mwanzo kwamba katika *strategic city* tuna miradi ya kujenga barabara, tunaweka taa na tunaweka madampo ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna miradi katika zile Manispaa na Miji yetu 18 tunafanya kazi kubwa sana na mnaiona. Tuna miradi ambayo inaendelea katika Halmashauri zetu kwa kupitia *TARURA*. Ndugu zangu bajeti hii inategemewa sana endapo kesho tutaipitisha. Katika watu watakaosononeka hatakuwa Mheshimiwa Dkt. Mpango nitasononeka mimi Waziri wa TAMISEMI kwa sababu katika maeneo yangu ndiyo naomba fedha kwa kiwango kikubwa kwenda kuwasaidia wananchi maskini ambapo bajeti yake tunaipitisha kesho. Nitajisikia vibaya leo hii kwako tunaenda kujenga vituo vya afya, shule, miundombinu ya barabara halafu kesho unasema hapana, nitakuuliza mara mbili mbili wewe nia yako nini katika mustakabali wa wananchi wetu na nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la busara ni kwamba tunapozungumza maslahi ya Taifa kwa pamoja na hasa katika mpango wa bajeti, naomba tuungane pamoja kwa sababu kwa kufanya hivyo ndiyo tunaenda kutatua matatizo ya wananchi wetu hatuna jinsi yoyote. Matatizo ya wananchi tutayatatua kupitia bajeti hii ambayo imewasilishwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu kubwa mchakato huu wa bajeti ambao mimi na jeshi langu la TAMISEMI, Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya lakini nyie Wabunge mkiwa wajumbe wa Kamati za Madiwani katika Halmashauri zetu tutaungana pamoja kuhakikisha suala zima la ukusanyaji wa kodi tushirikiane kwa pamoja kodi ipatikane miradi ikatekelezwe. Hata hivyo, jambo kubwa kuliko lote ni kesho kusema bajeti hii ya Mheshimiwa Dkt. Mpango tunasema ndiyo ipite katika asilimia zote 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yalikuwa ni hayo tu kuongezea. Kikubwa zaidi naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mpango na timu yake kwa kazi kubwa waliyofanya. Kwa kweli niseme bajeti ya mwaka huu inagusa wananchi wa kawaida. Imani yangu kubwa tutakapoungana kwa pamoja tutaenda kujibu matatizo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na kwa kweli kabla sijasahau nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii, hoja hii ni matunda mzuri ya utekelezaji wa Ilani ya

Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2015 imeanisha vipengele vingi vya kufanyiwa kazi na Ilani hiyo alikabidhiwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima niseme ukweli, Wabunge Wenzangu wa Chama cha Mapinduzi mtaniunga mkono kwamba Mheshimiwa Rais ameitendea haki Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Ni lazima niseme hatuna shaka tutakapoingia kwenye uchaguzi kuanzia mwakani katika nchi nzima ya Tanzania katika kila mkoa Ilani ya Uchaguzi imetelezwa na tutakwenda kuwaambia Watanzania ni kwa namna gani wanayo kila haki ya kuendelea kukiamini Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi zimechangiwa katika Bunge lako, niaanze labda na jambo moja. Serikali yetu inafanya kazi kwa umoja na ushirikiano kati ya Wizara moja na Wizara nyingine. Niseme tu unapoona mpinzani wako anakusifia ujue jambo hilo halijakaa sawasawa lakini ukiona mpinzani wako anakubeza ndiyo kamata hapo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imesemwa sana hapa na wenzetu wamejaribu kutuchonganisha sana na wananchi na hasa wakulima kwamba Serikali yetu haijafanya kitu kabisa kwenye sekta ya kilimo. Nikuombe sana huko mbele uchambuzi wetu wa bajeti ni lazima tuutizame kwa mapana yake kutoka sekta moja kwenda nyingine. Kwa mfano, ukiacha bajeti iliyotengwa kwenye Wizara ya Kilimo, Ofisi moja tu ya Waziri Mkuu na sisi pia tuna sekta ya kilimo na Wizara ya Maji ina sekta ya kilimo kwa maana ya miradi ya umwagiliaji. Sasa ukimjulisha hiyo yote naomba niwaambie wakulima wa Tanzania kwamba si kweli Serikali ya Awamu ya Tano imewatenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitayasema haya kwa kutumia *data* na sio propaganda. Ofisi ya Waziri Mkuu kwa bajeti ya mwaka 2017/2018 kwenye sekta ya kilimo ilipangiwa

takribani fedha za kitanzania zisizopungua shilingi bilioni 42.9. Mpaka tunafika Februari/Machi 2018, Ofisi ya Waziri Mkuu ilishapokea fedha za Kitanzania zisizopungua shilingi bilioni 40.9 kwa ajili ya miradi inayokwenda na kufanana na utekelezaji wa sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge ni mashahidi, Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria ni mashahidi na wameitembelea miradi hiyo Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Wameona jinsi miradi hiyo ilivyotekelezwa vizuri na kuwa ni kielelezo hata cha Muungano wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu niseme hiyo miradi michache tu ambayo ilikuwa imekwishakutekelezwa mpaka Machi 2018, nikiacha miradi mingi tu ya MIVARAF iliyotekelezwa kwa miaka iliyopita. Mbunge wa Ludewa atakubaliana nami tumeshakwisha kukamilisha ujenzi wa barabara Ludewa, Busega na Kilombero. Mtaniuliza barabara na kilimo wapi na wapi. Wabunge mmesema ili kuboresha kilimo ni lazima tukifungamanishe na miundombinu ya barabara, kazi hiyo imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga maghala na masoko ya kuongeza thamani ya mazao katika meneo yafuatayo. Tumemaliza ujenzi wa ghala Namtumbo, Busega, Mjini Magharibi, Makete, Longido, Rungwe, Tunduru, Kinyasini Zanzibar, Tibilizi Pemba na Micheweni. Nani anapata ujasiri wa kuitukana Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Tano imewadharau wakulima katika haya tunayoyasema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema subirini Mawaziri tutakapokuja tutaongea kwa *data* na hizi ndiyo *data* tunazowapa leo na Watanzania waelewe nini kinachoendelea katika nchi yao. Nataka kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge miradi hii niliyoisema hapa na hii miradi siyo miradi kiini macho. Mbunge yeyote ainue mguu kesho aende akaangalie Namtumbo, ghala lililojengwa

Namtumbo sio ghala tu la kuhifadhia mazao. Ghala hilo limewekwa na mashine za kuongeza thamani ya mazao ya wananchi ili kuwafanya wakulima waweze kujiajiri na kupata masoko. Hivyo hivyo katika maeneo mengi, nendeni mkaangalie mradi huu na ndiyo maana nasema mmesema ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Tizeba, mmemsema Waziri wa Fedha hajali wakulima, hizi ndio *data*, Serikali ya Awamu ya Tano inawajali wakulima wa Tanzania. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liliongelewa hapa suala la Serikali yetu kutofikiria na kutengeneza mfumo thabiti wa kuongeza ajira katika nchi yetu. Naomba niwaambie, tumeshafanya utafiti wa hali ya ujuzi katika nchi yetu na tumegundua wapi tupo katika suala zima la ujuzi. Tumefanya utafiti wa nguvu kazi katika nchi yetu ya Tanzania na tumefanya utafiti wa kujua ukosefu wa ajira ukoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge ukosefu wa ajira umepungua toka asilimia 11.7 mpaka asilimia 10.3. Kwa nini? Ukosefu wa ajira umepungua kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano imeamua kujikita kwenye miradi mikubwa ya kiuchumi ambayo itajenga uchumi wa nchi yetu vilevile miradi hiyo itasaidia kuondoa tatizo la ajira kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kazi hii imefanyika na naomba niwaambie vijana wakubali sasa hivi kubadili mtazamo wa kuajiriwa na Serikali tu. Waende wakaajiriwe kwenye miradi hii mikubwa ya kitaifa ambayo tumekwisha itengeneza. Miradi hii inafanya vizuri tu. Tuna Mradi wa Umeme Rufiji, mradi wa reli kwa kiwango cha kimataifa, miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege, mradi wa miundombinu ya barabara, viwanda, kazi hiyo inafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho lakini siyo kwa umuhimu nimuunge mkono Mheshimiwa Jafo. Waheshimiwa

Wabunge atakayeikataa bajeti kesho ana lake jambo. Historia ya nchi yetu ya Tanzania imeanza na Awamu ya Kwanza. Rais wetu wa Awamu ya Kwanza alijenga reli ya *TAZARA*; alijenga bomba la mafuta la kutuunganisha Tanzania na Zambia; na alijenga uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Akaja Rais wa Awamu ya Pili akajenga barabara ya Dodoma - Dar es Salaam, barabara ya Chalinze - Moshi na mambo mengine mengi. Akaja Rais wa Awamu ya Tatu akajenga Daraja la Mkapa, Daraja la Umoja, Uwanja wa Mpira na Mkongo wa Taifa. Akaja Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akajenga Daraja la Kikwete, Daraja la Rusumo, Daraja la Kigamboni, Daraja la Kibiti, *UDOM*, *JK Hospital* na Daraja la Malagarasi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo amekuja Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa muda mfupi amefufua Shirika la Ndege kwa kununua ndege; amewekeza kwenye mradi wa bomba la mafuta kati ya Tanzania na Uganda; na ameanza mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Njaaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Ujenzi wa mradi wa umeme Mto Rufiji; viwanja vya ndege, ujenzi wa meli mpya...

**MBUNGE FULANI:** Mlipe fidia viwanja vya ndege, hamjalipa fidia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Amehamasisha Serikali ihamie Dodoma; ameongeza bajeti ya dawa; ameleta elimu bure na umeme wa *REA*. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kazi hizi ambazo zimefanyika kwa muda mfupi Marais hao wakipokezana vijiti hiyo yote inaonesha ni ukomavu na ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi tu ndiyo inayoweza kuyafanya mambo haya katika nchi ya Tanzania. Niwaombe na hasa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi safari ndiyo inashika kasi na tutafika salama na gari hili likiongozwa na Jemedari wetu Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Makamanda wake Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, Mawaziri na Wabunge wote. Niwaombe sana Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tuwe pamoja kupigania Serikali yetu inayokwenda kuleta maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai kama Serikali yako maeneo ambayo Serikali bado inaona kuna changamoto tutaendelea kuyafanyia kazi. Nina uhakika tutakapofika mwaka 2020 Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi itakuwa imetekelezwa na wananchi wataichagua CCM. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niwapongeze Wabunge wote walioishauri vizuri Serikali na hasa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba Waheshimiwa Wabunge tuipigie kura bajeti yetu kesho. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walishangilia kwa muda)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hii ndiyo inaitwa mwanamke mashine jaza ujazwe. *(Makofi/Vigelegele/Kicheko)*.

**WABUNGE FULANI:** Wera, wera, wera.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha tena shughuli ya Mtukufu Agakhan iko sasa hivi. Mgeni Rasmi ni Mheshimiwa Waziri Mkuu na yeye sasa hivi anaelekea pale na wote tumuunge mkono, yeye na Spika watakuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne Tarehe 26 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*